# UHAKIKI WA <u>BINA-DAMU!</u> (2002) NA <u>MUSALEO!</u> (2004) NA K.W. WAMITILA.

NA

NYABUNGA, VINCE ARASA.

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library

0370264 4

AGOSTI 2005.

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

VINCE ARASA NYABUNGA

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo hiki.

DR. KINEENE WA MUTISO

Na

MUSYOKA, F. MWANGANGI

**TABARUKU**

Tasnifu hii naitabarukia marehemu mama mzazi, Beldine Basweti, aliyeaga dunia mwaka jana. Mama, "Tulikupenda lakini yule aliyekupenda zaidi alikuchukua wakati uliompendeza.Lala salama mama tutaonana asubuhi"

## YALIYOMO


Mada ........................................ i

Ikirari ........................................ ii

Tabaruku ........................................ iv

Yaliyomo ........................................ v

Shukrani ........................................ vii

Muhtasari ........................................ viii

SURA YA KWANZA.

1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1 Uhalisia, usasaleo na uhalisiajabu ........................................ 1

1.2 Tatizo la utafiti ........................................ 1

1.3 Madhumuni ya utafiti ........................................ 3

1.4 Nadharia tete ........................................ 4

1.5 Sababu ya kuchagua mada ........................................ 4

1.6 Upeo na mipaka ........................................ 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ........................................ 6

1.8 Misingi ya kinadharia ........................................ 9

1.9 Mbinu za utafiti ........................................ 16

1.10 Hitimisho ........................................ 17

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi ........................................ 18

2.1 Vipindi vya uandishi wa K.W. Wmitila ........................................ 18

2.2 Hatua ya mwanzo ya uhalisiajabu ........................................ 19

2.3 Kipindi cha uhalisia hakiki ........................................ 21

2.4 Kipindi cha uhalisia wa kijamaa ........................................ 22

2.5 Kipindi cha uhalisiajabu ........................................ 23

2.6 Utandaridhi ........................................ 24

2.7 Hitimisho ........................................ 28

## SURA YA TATU


3.0 Utangulizi ........ 29

3.1.0 Mukhtasari wa riwaya ya Bina-Adamu! ........ 29

3.1.1 Sehemu ya kwanza ........ 30

3.1.2 Sehemu ya pili ........ 31

3.1.3 Sehemu ya tatu ........ 40

3.2.0 Mukhtasari wa Musaleo! ........ 41

3.2.1 Sehemu ya kwanza (sura 1-19) ........ 54

3.2.2 Sehemu ya pili (Sura 20-30) ........ 54

3.2.3 Sehemu ya tatu (Sura 31-42) ........ 64

3.2.4 Hitimisho ........ 72


## SURA YA NNE


4.0 Utangulizi ........ 73

4.1 Matukio ya kiajabu ........ 73

4.2 Ndoto na uhalisia ........ 82

4.3 Uduara wa wakati ........ 84

4.4 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali ........ 89

4.5 Visasili ........ 90

4.6 Mitindo ya riwaya kazi hizi ........ 93

4.7 Hitimisho ........ 94


## SURA YA TANO


5.0 Hitimisho ........ 95

5.1 Matatizo ........ 100

5.2 Mapendekezo ........ 101

5.3 Marejeleo ........ 102

**SHUKRANI**

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunihifadhi na kuniwezesha kuanza na kuikamilisha shahada yangu. Moyo wangu waniongoza kuwashukuru wote waliochangia kwa hali zote kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Labda sitaweza kuwataja katika tasnifu hii kwani ni wengi mno, kwenu nyote basi ninatoa shukrani zangu za dhati.

Shukrani za kipekee nazimimina kwa wasimamizi wangu katika kazi hii, wahadhiri Dkt. Kineene Wa Mutiso na M. F. Mwangangi. Hawa walinipa wasia na mwelekeo wakati wote nilipohitaji msaada wao. Ushauri wao uliniwezesha kutia shime hadi kukamilika kwa tasnifu hii. Muda huo wote mlionitengea kunipa mwongozo katika utafiti wangu sitasahau kamwe, asateni sana. Pia ningependa kuwashukuru wahadhiri wengine katika idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa mawaidha yao nyakati tofauti nilipokuwa naishughulikia kazi hii. Hawa ni Dkt. K.W. Wamitila, Dkt. Mwenda Mbatia, Bi. Mwaliwa, Bi. Njuguna, Dkt.T, Olali, Dkt.A.Buregeya, Dkt. K. Mberia na H. Mogambi.

Hali kadhalika ninawashukuru wazazi wangu kwa juhudi zao zisizo na kipimo kunielimisha kwa miaka hii yote kufikia sasa. Ninawashukuru marafiki wangu wote walionifaa sana wakati wa masomo yangu ya uzamili. Hawa ni E. Bogonko, Sister Mwenda, Ndugu Osoro, Ndugu Fred, Ken Aungo na Ndugu Richard Magare. Hongera kwa yote mliyonitendea. Kadhalika ninawashukuru wanafunzi wezangu tulion'goa nanga pamoja katika safari ya usomi: J.M.Gichamba, N.Njiru, K.P. Mungai, M.P. Oichoe, N.D. Theuri, M. F. Kaviti, M.A. Mulila, R.H.Swaleh, M.M. Rapando, W. Were, L. G Nkonge, W.E. Karanja, K.Nguku, W.E. Wepoh, N.O.Basweti na bila kuwasahau wanafunzi wote wa idara ya Kiingereza. Heko kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

Siwezi kumsahau mke wangu mpendwa, Rose Mwikali Arasa na wana wangu: Howard Nyabunga na Joy BildineBasweti. Mlinipa muda wenu mwingi wakati nilipokuwa nikiandika tasnifu hii. Asante kwa kunifaa wakati wote. Mungu awabariki. Kwenu nyote, 'Nawatakia mema nyakati zote!'

## MUKHTASARI

Utafiti huu umeshughulikia suala la uhalisiajabu katika riwaya za fasihi ya Kiswahili. Riwaya zilizohakikiwa ni Bina-Adamu! (2002) na Musaleo! (2004) za K.W. Wamitila. Nadharia ilyoongoza utafiti huu ni kitengo kimoja cha mwelekeo wa usasaleo. Hii ni nadharia ya uhalisiajabu, matukio yanasawiriwa kiajabuajabu, ya kuogofya na kutisha. Matukio haya huashiria hali halisi ya maisha katika jamii. Uhalisiajabu ni mtindo wa riwaya wa hivi majuzi unaopiku njia za kimapokeo za uandishi wa fasihi ya Kiswahili na usawiri wa jamii. Kimapokeo, riwaya inapaswa kujengeka katika misingi ya uhalisia.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti. Hapa ndipo tumeshughulikia mada ya utafiti, malengo yake, sababu za kuchagua mada na yaliyoandikwa kuhusu somo hili. Aidha, tumejadili upeo na mipaka ya utafiti huu na misingi ya nadharia iliyotuongoza; mwishowe tumeeleza mbinu za utafiti.

Sura ya pili imejadili maisha ya mwandishi, K.W.Wamitila. Tumeonyesha vipindi mbalimbali vya uandishi wake. Uchunguzi huu umedhamiria kuonyesha mitindo aliyoitumia tangu aanze kuandika na kuonyesha ni kwenye kipindi gani cha uandishi aliingilia uandishi wa kihalisiajabu na kwa nini alifanya hivyo.

Sura ya tatu na ya nne zinachunguza namna riwaya hizi mbili zimetumia uhalisiajabu katika kuwasilisha ujumbe. Tumeonyesha mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu aliyoitumia. Mihimili hii ni pamoja na matukio ya kiajabuajabu, ndoto na uhalisia, uduara wa wakati, visasili, uvunjaji wa mipaka ya mahali na upekee wa mtindo wa riwaya ya kihalisiajabu.

Sura ya tano imehakiki na kulinganisha na kulinganua riwaya zote mbili kwa mujibu wa mada husika. Aidha, matokeo ya utafiti, matatizo yaliyokabiliwa katika utafiti na mapendekezo, yametolewa katika sura hii.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulikia tatizo la utafiti wetu. Tutatambulisha mada yetu ambayo ni kuchunguza jinsi uhalisiajabu unavyojitokeza katika riwaya mbili za K.W. Wamitila Bina-Adamu! na Musaleo! (2002 na 2004). Vile vile katika faslu hii, tutatoa madhumuni ya utafiti huu ili kubainisha malengo yetu. Hali kadhalika, tutashughulikia nadharia tete ya uhakiki ambayo ni mhimili wa utafiti huu.

Katika sehemu hii pia, tatafafanua sababu za kuchagua mada au somo hili. Kwa mfano, kazi hizi mbili ( Bina-Adamu! na Musaleo! Ni kazi ambazo zimevunja baadhi ya kaida za uandishi zilizoeleka katika uandishi wa Kiswahili. Kwa hivyo, huu ni uandishi mpya ambao unahitaji kufanyiwa utafiti.

Mpaka na upeo wa somo hili utajikita katika riwaya za Kiswahili ambapo tutachunguza riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo!. Yaliyoandikwa kuhusu somo hili pia tutayashughulikia ili kupata msingi mwema wa utafiti wetu. Hizi ni kazi anuwai za kilakiki kuhusu uhalisiajabu katika andishi wa Kiswahili kwa mfano Nagona na Mzingile. Mashetani, miongoni mwa zingine. Pia tutatoa mifano kutoka maeneo mengine ya ulimwengu pale ambapokutahitajika. Faslu hii itahitimishwa kwa kupendekeza njia au mbinu zitakazotumiwa kukusanyia, kuchanganua na kuwasilisha data ya utafifti huu.

## 1:1 UHALISIA, USASALEO NA UHALISI AJABU.

Kabla hatujaanza kushughulikia somo hili, ni vema kutoa maelezo kuhusu dhana ya uhalisia, usasaleo na uhalisiajabu.

Tutafanya hivi kwa lengo la kutaka kuzielewa kazi za Wamitila na tutapata kujua ni msingi gani au vichocheo vipi vilivyomsukuma kuanza kutumia mbinu ya uhalisiajabu katika uandishi wake huku Binadamu! (2002) na Musaleo! (2004) zikiwa vigezo vya ufafanuzi huu.

K.W. Wamitila (2002:114) anasema kuwa uhalisi ni mojawapo ya matapo maarufu katika ulimwengu wa fasihi na lenye athari kubwa sana.

Historia ya riwaya imefungamanishwa na suala la uhalisi, jambo ambalo hatuwezi kuhakiki kazi ya riwaya bi'a kulishughulikia. Kwanza uhalisia huashiria tapo la kipindi maalumcha kihistoria katika fasihi ya ulaya, na pili huelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambapo kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na na uhalisia. Kazi zinazoangaliwa kama za kihalisia zinatarajiwa kuwa akisiko la hali ya maisha katika jamii inayohusika. Kwa mfano inawezakuwa kitu, mhusika kihalisia, ikiwa yanafanana na maisha ya kila siku ya binadamu.Nadharia ya uhalisia illingia katika riwaya ya Kiswahili katika enzi ya S.A. Mohammed, Shafi A. Shafi na Mohammed S. Mohammed.

Dhana ya usasaleo ni dhana inayotumiwa kuelezea mielekeo ya kitamaduni na kisanaainayohusishwa kwa kiasi kikubwa na karne ya ishirini. Kimsingi, dhana hii hutumiwa kuelezea au kuzitambulisha sifa mpya za dhamira, tanzu, dhana na mitindo ya kifasihi inayohusishwa zaidi na miongo ya kwanza ya karne ya ishirini. Kipindi kinachorejelewa hapa ni Vita Vikuu vya Pili vya Uimwengu. Vita hivi viliathiri sana maendeleo na utamanduni wa binadamu. Katika hali hii, palihitajika namna na hata miundo mbalimbali ya kuangazia na kuelezea athari hizo. Dhana ya uhalisiajabu ni mojawapo ya miondoko ya usasaleo kama vile udenguzi wa lugha nadharia baada ya ukoloni na baadhi ya nadharia za kifeministi. Alexander (1990:127): uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasaleo inavyotulazimu kufikiria upya juu ya dhana za kimapokeo kuhusu riwaya ya uhalisia ya karne za kumi na nane na kumi na tisa.

Kutokana na kusoma kwetu kwa riwaya za K.W. Wamitila, Bina- Adamu! (2002) na Musaleo! (2004), tumegundua kwamba riwaya hizi mbili zina elementi za uhalisiajabu.

### 1:2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu utashughulikia kazi mbili za K.W Wamitila: Bina-Adamu! (2002) na Musaleo! (2004) kama kazi za kiuhalisiajabu. Pia utafiti huu unakusudia kuhakiki jinsi vipengele vya uhalisiajabu vinavyodhihirika katika riwaya hizi mbili. Vile vile, utafiti wetu utabainisha jinsi uhalisiajabu unavyoshughulikia kadhia zinazohusu maisha halisi ya watu wanaozungumziwa katika riwaya hizi mbili. Kutokana na jambo hili, tutaonyesha ni kwa nini uhalisiajabu ni njia mwafaka zaidi ya kusoma na kuzifahamu riwaya hizi mbili. Tatizo hili ni muhimu kushughulikiwa kwa vile mwandishi ametumia lugha ya kiajabuajabu, uhusika usiozoeleka na mandhari ya kisihiri, kusawiri kazi yake. Uandishi wa aina hii unahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha mwelekeo wa mwandishi huyu.

Pengo baina ya yale tunayajua na yale tunapaswa kuyajua katika uhalisijabu ni tatizo ambalo lahitaji kushughulikiwa kwa kina kupitia utafiti huu. Kwa hiyo, tunadhamiria kuziba pengo kati ya yale tunayajua kuhusu utanzu huu, huku tukiwa na lengo la kupanua uhakiki wa Kiswahili. Baadhi ya kazi za Kiswahili zenye sifa za uhalisiajabu ni kama vile: Walenisi (1995), Kusadikika (1951), Nagona (1990), Mzingile (1991) na Babu Alipofufuka (2001).

### 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Lengo la utafiti wetu ni kuzihakiki riwaya mbili za K.W. Wamitila (Bina-Adamu! na Musaleo!). kama kazi za uhalisiajabu. Utafiti huu unakusudia kuchunguza namna vipengele vya uhalisiajabu vinavyodhihirika katika riwaya za Wamitila, Bina-adamu! na Musaleo!. Aidha, utafiti huu utabainisha jinsi uhalisiajabu unavyoshughulikia kadhia zinazohusu maisha halisi ya watu wanaozungumziwa katika riwaya teule.

Pia tunadhamiria kuonyesha jinsi mwandishi huyu alivyoathiriwa na utanzu wa uhalisiajabu na kubainisha ni kwa kiwango gani riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo! zimefaulu kama kazi za aina hiyo.Utafiti wetu vile vile, unanuia kupima mwelekeo wa Wamitila, ambaye ni mmoja wa Waandishi wa kutajika na ambaye amechangia pakubwa katika fasihi ya Kiswahili. Kutokana na hayo, tutaonyesha ni kwa nini uhalisiajabu ni njia mwafaka zaidi ya kuzihakiki riwaya za Binadamu! na Musaleo!. Kwa ufupi, utafiti huu unalenga masuala:

(i) Kuchunguza ni vipi uhalisiajabu unajitokeza katika riwaya za Bina- Adamu! na Musaleo!.

(ii) Kubainisha ni vipi uhalisiajabu unavyoashiria uhalisia wa kimapokeo katika riwaya ya Kiswahili.

(iii) Kuonyesha ni vipi mukhtadha wa uhalisiajabu unatuwezesha kuzieleza zaidi riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo!

## 1.4 NADHARIA TETE

Utafiti wetu unaongozwa na kuendelezwa na nadharia tete kuwa kuna uhalisiajabu unaojitokeza katika riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo! na ni kwa namna gani unaashiria na kuzungumzia uhalisia wa kimapokeo katika kazi hizi mbili

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA.

Kazi hizi mbili (Bina-Adamu! na Musaleo!) ni kazi ambazo zimevunja baadhi ya kaida za uandishi zilizozoeleka katika uandishi wa Kiswahili. Jambo hili la uandishi katika fasihi ya Kiswahili linahitaji mtazamo na usomaji mpya. Uandishi huu tunapata kwamba umejitokeza katika riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo! Pengine kutungwa kwa riwaya hizi mbili kunaashiria kuzuka kwa mikakati ya kipekee ya kushughulikia matatizo yanayokabili mataifa ya ulimwengu wa tatu.

Utafiti huu pia utachangia uhakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa kumzingatia mwandishi (Wamitila) ambaye ni mwandishi chipukizi wa riwaya, kwa kuchunguza kazi zake za kimwendelezo (yaani riwaya ya Bina-Adamu! *ni* maendeleo ya Musaleo!). Uandishi wake katika riwaya hizi mbili, ni uasi dhidi jinsi ambavyo waandishi wengi wamekuwa wakiandika kwa muda mrefu.

Utafiti huu utachunguza ni kwa nini mwandishi huyu ameamua kutumia mtindo huu wa ukiushi wa kaida za uandishi katika kazi zake. Aidha riwaya hizi mbili tunazoshughulikia hazijahakikiwa kwa kina hapo awali.

Kwa mfano, M.J. Kagendo (2004) katika tasnifu yake ameshughulikia riwaya ya Bina-Adamu! (2002) kwa kuilinganisha na Babu Alipofufuka (2002) ya S.A. Mohammed. Kwa hivyo, utafiti huu unafaa kwani utakuwa unaziba pengo katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Uhalisiajabu ni uandishi wenye changamoto kubwa ambapo utunzi na uhakiki hukutani. Yaani ni mtindo wa kuandika na vile vile mtindo wa kuhakiki, kwa sababu wale waandishi wanaoandika ni hao hao wanaozungumzia kazi zao au nyinginezo zinazoshabihiana na zao.

Tutatalii na kuona ni kwa kiasi gani mambo hayo yanavyoingiliana na ni kwa nini Wamitila ameamua kutumia mtindo wa uandishi wa namna hii. Tunaamini pia kuwa, hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika, kwa sababu, wahakiki labda hutofautiana kwa mitazamo, misimamo na pia uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii, kulingana na wakati na katika maendeleo ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyingine huathiri maendeleo ya fasihi. Hii ndiyo sababu G. Hough (1962:6) akasema:

> Hakuna kazi yoyote ya uhakiki iliyokamilika wakati mmoja na ukawa ndio ukomo, kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii katika kila kipindi kipya cha historia, fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya – jinsi tunavyofasili maandishi mapya ndivyo fasihi zetu za yale ya zamani zinavyobadilika (TY).

Tunatumaini kuwa uhakiki wetu wa riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo! Utatoa mchango kabambe kwa fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu utaziba pengo katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Uhakiki wetu utajikita katika riwaya za Kiswahili tu ambapo tutachunguza riwaya za Wamitila (Bina- Adamu! (2002) na Musaleo! (2004). Mwandishi huyu ameandika riwaya zingine lakini hizi mbili zitatoshea kwa mahitaji ya utafiti wetu, kwa sababu kutokana na mapito tuliyoyafanya, riwaya hizi mbili zimeonyesha mwelekeo wa uhalisiajabu.

Inawezekana kuwa kuna riwaya zingine, tamthilia au mashairi yanayoweza kuhakikiwa kwa kutumia mihimili ya uhalisiajabu. Hata hivyo, hatutajishughulisha na hayo kwa sababu riwaya hizi mbili zina ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai yetu.

## 1:7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Katika fasihi ya Kiswahili, kuna waandishi watangulizi wa uwanja huu wa uandishi. Miongoni mwao ni Topan katika tamthilia ya Aliyeonja Pepo (1973) na Hussein katika tamthilia ya Mashetani (1971). Hawa watunzi wanakaribia kutumia mbinu ya uhalisiajabu. Hata hivyo, ingawa waliweza kubuni hali za kiajabuajabu, walifanya hivyo kwa kuchota mitindo yao kutoka katika malighafi ya utamaduni wa Kiafrika ambapo tunajua tangu kale dhana za miungu, mashetani, pepo na mengineo zimekuwepo.

Hata kama hadithi zao ni zenye uajabu, walijua kwamba kuna ujumbe fiche humo ndani.Aliyeoja Pepo ni hadithi kuhusu jinsi maisha yanavyoendelea baada tu ya mtu kufa.(Topan 1970:3). Hata hivyo, kiini ni kuhusu mhusika mmoja aitwaye Juma Hamisi anayeuawa na malaika wa kifo (Ziraili) kimakosa kupitia ajali ambapo Juma anapigwa dafrau na punda badala ya mtu anayestahili kufa anayeitwa John Houghton. Mushkili unatokea kwa

unachezwa katika jukwaa karibu na mbuyu (maskani ya mashetani inavyoaminiwa na Waswahili). Ni uigizaji unaomfunulia msomaji, mtazamaji na msikilizaji mahusiano yaliyopo baina ya viongozi na wananchi, uhuru na ukoloni mamboleo, ukoloni mkongwe, unyanyaswaji/ugandamiswaji wa Waafrika na mabwana Wazungu.

Vile vile mabwana Waafrika wenye madaraka sasa na hata wale waliokuwa na madaraka hapo mbeleni kabla ya kupokonywa. Shetani amesawiriwa kama kiumbe mwenye nguvu na uwezo wa kufanya mambo yasiyo ya kawaida kama vile kujibadilisha nafsi. Shetani anasema anaweza kujigeuza ndege, kuwa upepo na pia kuweza kurukia tawi (Hussein 1971:2).

Vile vile tamthilia ya Mashetani inaashiria uhalisiajabu pale ambapo sehemu ya pili ya mchezo inachezwa katika akili ya Kitaru (uk. 13).

Aidha, Kitaru anatuelezea kuhusu sifa nyingine ya uhalisiajabu anapomwambia Juma kuwa hajui kama alikuwa amelala au alikuwa anaota na kwa kweli mtu huona ukweli zaidi kwenye ndoto kuliko katika maisha ya kweli. Hiki ni kipengele muhimu sana cha nadharia hii.

Kezilahabi ni mwandishi na mwanafasihi mwingine mashuhuri anayetumia mtindo wa usasaleo katika kazi zake. Riwaya zake maarufu Nagona (1990) na Mzingile 1991) zimezua mijadala mirefu kati ya wasomi mbalimbali.

Mbatiah (1997) anasema kwamba kimsingi riwaya za Kezilahabi zinahusu maisha ya Tanzania na mandhari yake ni kisiwa cha Ukerewe. Anaendelea kusema kwamba katika Nagona na *Mzingile,* mwandishi anamgurisha msomaji kutoka mazingira ya kilimwengu aliyoyazoea na kumpeleka kwenye ulimwengu wa kindoto baina ya kifo na uhai, kuwa macho na kuwa ndotoni. Kwa kufanya hivyo, anamshirikisha msomaji katika safari ya kifikra ya kutalii ulimwengu ili kuujua ukweli wake. Safari hii inapindua kabisa mtazamo wa kawaida wa ulimwengu na maisha ya mwanadamu. Wamitila (1991) naye anasema kwamba, riwaya za Kezilahabi za awali zilihusu ulimwengu wa kimaumbile au jinsi ulivyo, kama tuujuavyo na kama tuuonavyo.

unachezwa katika jukwaa karibu na mbuyu (maskani ya mashetani inavyoaminiwa na Waswahili). Ni uigizaji unaomfunulia msomaji, mtazamaji na msikilizaji mahusiano yaliyopo baina ya viongozi na wananchi, uhuru na ukoloni mamboleo, ukoloni mkongwe, unyanyaswaji/ugandamiswaji wa Waafrika na mabwana Wazungu.

Vile vile mabwana Waafrika wenye madaraka sasa na hata wale waliokuwa na madaraka hapo mbeleni kabla ya kupokonywa. Shetani amesawiriwa kama kiumbe mwenye nguvu na uwezo wa kufanya mambo yasiyo ya kawaida kama vile kujibadilisha nafsi. Shetani anasema anaweza kujigeuza ndege, kuwa upepo na pia kuweza kurukia tawi (Hussein 1971:2).

Vile vile tamthilia ya Mashetani inaashiria uhalisiajabu pale ambapo sehemu ya pili ya mchezo inachezwa katika akili ya Kitaru (uk. 13).

Aidha, Kitaru anatuelezea kuhusu sifa nyingine ya uhalisiajabu anapomwambia Juma kuwa hajui kama alikuwa amelala au alikuwa anaota na kwa kweli mtu huona ukweli zaidi kwenye ndoto kuliko katika maisha ya kweli. Hiki ni kipengele muhimu sana cha nadharia hii.

Kezilahabi ni mwandishi na mwanafasihi mwingine mashuhuri anayetumia mtindo wa usasaleo katika kazi zake. Riwaya zake maarufu Nagona (1990) na Mzingile 1991) zimezua mijadala mirefu kati ya wasomi mbalimbali.

Mbaliah (1997) anasema kwamba kimsingi riwaya za Kezilahabi zinahusu maisha ya Tanzania na mandhari yake ni kisiwa cha Ukerewe. Anaendelea kusema kwamba katika Nagona na *Mzingile,* mwandishi anamgurisha msomaji kutoka mazingira ya kilimwengu aliyoyazoea na kumpeleka kwenye ulimwengu wa kindoto baina ya kifo na uhai, kuwa macho na kuwa ndotoni. Kwa kufanya hivyo, anamshirikisha msomaji katika safari ya kifikra ya kutalii ulimwengu ili kuujua ukweli wake. Safari hii inapindua kabisa mtazamo wa kawaida wa ulimwengu na maisha ya mwanadamu. Wamitila (1991) naye anasema kwamba, riwaya za Kezilahabi za awali ziihusu ulimwengu wa kimaumbile au jinsi ulivyo, kama tuujuavyo na kama tuuonavyo.

Hata hivyo, Wamitila anaziona riwaya za Nagona na Mzingile kuwa za kimetafizikia – yaani zilizopita ufahamu wetu wa ulimwengu kama ulivyo. Mwandishi anaendelea kueleza kwamba ingawa haina haja kujichosha kwa kujiuliza kwa nini Kezilahabi akajiingiza katika udhanifu au utopia, yeye (Wamitila) anaona kwamba picha yoyote ya kimaumbile inayopuuza utopia si picha kamilifu. Kwa mujibu wa Wamitila (1991), tunahitaji udhanifu ili kuwa na uhalisia. Uhalisia wenyewe huhusisha udhanifu. Anapendekeza kwamba riwaya hizi zichunguzwe upya labda kwa mtazamo wa kifalsafa (1991:66).

Mbali na mshabaha wa waandishi Topan (1970) na Hussein (1971) katika misingi ya uhalisiajabu, ni muhimu kutaja kwamba uandishi wao una tofauti kubwa na ule wa Wamitila (2002) na (2004) sababu hii ni ya kifalsafa. Ingawa watangulizi wa uhalisiajabu waliweza kubuni hali za kiajabuajabu, walifanya vile kwa kuchota kutoka kwa malighafi ya utamaduni wa Kiafrika ambapo tunajua tangu kale dhana za miungu, mashetani, pepo na zinginezo zimekuwepo.

Wamitila (2002 na 2004) anatumia uhalisiajabu kimakusudi kwa kutaka kuyaangalia masuala ya kijamii kwa njia ya kiajabu na ya kipekee. Topan, Hussein na Kezilabahi wanaweza kufahamika vyema kwa kutumia nadharia nyinginezo. Wamitila katika kazi zake za hivi karibuni anafahamika vizuri zaidi kwa kuzingatia uhalisiajabu. Tutachunguza ni kwa kiasi gani Wamitila amefaulu au kutofaulu kutumia mtindo huu.

## 1:8 MISINGI YA KINADHARIA

Nadharia tunayoamini inaafiki utafiti huu ni ya uhalisiajabu. Zamora (1995) unatuelea kwamba nadharia hii iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani mmoja aliyejulikana kama Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz Roh alitumia istilahi uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelezea na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uajabu uliomo kwenye uhalisi uliozoeleka na unaotokana na ujarabati.

Akielezea uhalisiajabu Mbatiah (2002: 60) anasema:

> Istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia. Yaani, kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Uhalisia wa kimaajabu huusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka bara la Afrika, Merakani ya Kusini na Asia.(TY)

Wamitila (2003:274) naye katika kutoa mchango wake kuhusu uhalisiajabu, anakubaliana na maelezo ya Mbatiah lakini anaongezea kuwa mpaka uliopo kati ya mambo yanaweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Kutokana na mawazo ya Mbatiah (2002) na Wamitila (2003), tunapata kuwa uhalisiajabu ni namna fulani ya kueleza uhalisia unaotuzunguka. Waandishi wametumia mtindo huu makusudi kwa kujua kwamba ni njia mwafaka ya kuyapigia mbizi masuala muhimu katika jamii. Tukiichunguza mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu inatosheleza uhakiki wa kazi yetu. Kwa kuzingatia mihimili muhimu ya nadharia hii tutaweza kuzielewa riwaya tunazozihakiki na hatimaye kufanikisha malengo yetu.

Amaryll katika Michelle (1993) anatueleza kuwa uhalisiajabu una sifa na mitazmo miwili inayokinzana lakini pia inayokubaliana. Mtazamo mmoja ni ule wenye msingi wa uhalisi ilhali wa pili una msingi wake katika imani kuwa uajabu ni kiungo muhimu cha ulimwengu wa kila siku. Kwa hivyo, kiini cha uhalisiajabu katika fasihi huwa ni msisitizo wa ushirikiano wa uajabu na uhalisi. Ingawa kuna matukio ya kiajabu katika kazi zinazozingatia uhalisiajabu, yanaunganishwa na ulimwengu 'halisi' na matukio haya, yana misingi yake katika uhalisi wa kijamii, uhalisi wa kihistoria na kisiasa.

Cooper (1998:16) ameshughulikia kwa kina uandishi wa kiuhalisiajabu hasa kwa kutilia maanani waandishi wa kutoka Afrika Magharibi. Anaelezea kuwa sababu za kiuchumi, kijamii na kisiasa ndizo zinazowachochea waandishi kutumia mtindo huu katika kazi zao.

Akiwarejelea Jameson na Anderson, Cooper (1998) anasema kwamba kuna uhusianb kati ya maendeleo ya kibepari na kuibuka kwa uhalisiajabu.

Jambo linalodhihirika kutokana na maelezo ya wasomi tuliowarejelea ni kwamba uhalisiajabu haujajitenga na hali halisi ya jamii zetu, bali kwa kweli umeibuka kutokana na hali mbalimbali za hizo jamii.

Kwa mujibu wa Alexander (1990:127) anasema:

> Uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasaleo inavyotulazimu kufikiria upya juu ya dhana za kimapokeo kuhusu riwaya ya uhalisia ya karne za kumi na nane na kumi na tisa. Aidha, uhalisiajabu umetulazimu kuwazia ufaafu wa baadhi ya mitindo ya uandishi kwa mada tofauti tofauti. (TY)

Baadhi ya maendeleo ya kusisimua katika mwisho wa karne ya ishirini ni kuwa kumeibuka waandishi wanaotalii uhusiano kati ya historia na masimulizi ya ubunifu. Kwa mfano, waandishi wa riwaya ya Marekani Kusini G. G. Marquez, Allende Isabel na Vargas Llosa miongoni mwa wengine, wameibusha na kutumia visasili vya kitaifa katika kazi zao. Visasili vya kitaifa ni visa vinavyojaribu kuelezea mustakabali wa taifa lote kwa ujumla. Drought (1993) naye anatoa yafuatayo kuhusu dhana ya uhalisiajabu:

> Ni dhana imehusishwa sana na uandishi wa kibunifu katika Marekani Kusini. Katika miaka ya 1940 huko Marekani Kusini, uhalisi wa kimajabu ulikuwa njia ya kudhihirisha fikra za kikweli za Wamerekani Kusini na kuunda mtindo mpya wa kipekee na huru wa fasihi. Hata hivyo, ni muhimu sana kuelewa kuwa tofauti kati ya uhalisiajabu katika sanaa ya uchoraji na uhalisiajabu katika sanaa ya uandishi hususan fasihi. (TY)

Roh (1925) vile vile alitumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kuelezea aina fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuupigia maswali yoyote uhalisia huo. Pamoja na hayo, uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia.

Kulingana na Ousbv (2002) anasema kuwa riwaya mashuhuri zaidi ya kiuhalisiajabu ni ile ya G. G.Marquez <u>One hundred years of Solitude</u> (1980). Riwaya hii ilichangia kutuzwa kwa

mwandishi huyo tuzo ya '*Nobel prize*' ya fasihi ya mwaka 1981. Uhalisia wa kimaajabu huusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka bara la Afrika. Marekani ya kusini na Bara Hindi. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika. Waandishi wanaoandika katika misingi hii hushikilia kuwa mtazamo wao wa uhalisia unawakilisha msimamo wa jamii zao. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi ya yasiyowezekana kuwepo katika ulimwengu huo huwa mdogo sana.

Hadi kufikia miaka ya sitini, fasihi ya Marekani kusini ilikuwa haitiliwi maanani na wasomi. Kulibuka kwa riwaya ya kisasa katika miaka hamsini na ya sitini kulibadilisha hali hii pakubwa. Aidha, kuibuka kwa riwaya za kubuni za usasaleo kulibadili hali iliyokuwepo hata zaidi (Williams 1995:1).

G..Marquez kama mwaasisi wa uandishi wa kisasaleo anafikiriwa na wasomaji wengi wa kimagharibi kuwa mwandishi wa kifantsia. Kinyume na madai haya, yeye mwenyewe amedai mara nyingi kuwa ni mhalisia ambaye anajaribu kuelezea jinsi hali ilivyo nchini mwake Colombia kwa njia ya kweli iwezekanavyo. (Williams 1995:5).

Kwa mfano, kwa mujibu wa Williams (1995), katika riwaya ya One Hundred Years of Solitude (1980), Marquez anaelezea kuhusu wafanyakazi wa Macondo ambao wanaandaa mgomo. Baadaye uvumi unaenezwa kwamba serikali imewaua mamia ya wafanyakazi. Kisa hiki kimetajwa kuwa cha kifantasia kuliko vingine kwa sababu tukio la kihistoria linapuuzwa na kuwasilishwa kama uvumi tu.

Wanahistoria na wasomi wamekubaliana kuwa hadithi hiyo ina ukweli wa kihistoria na yenye ukweli kuliko zingine, kwa sababu inarejelea mauaji ya wafanyakazi wa mashamba ya ndizi katika sehemu iliyojulikana kama *Cienaga* nchini Colombia mnamo mwaka wa ishirini na nane. Ni wazi basi kuwa riwaya hii ya Marquez ni yenye ukweli unaoshabiana na matukio halisi ya Kihistoria (Williams 1995:6).

Williams (1995) akimnukuu Fuentes ambaye ni mwandishi wa kihalisiajabu, anasema kwamba wanahistoria wa Marekani Kusini wamebadili vile ukweli umekuwa ukitazamwa. Ukweli ulikuwa ukipuuzwa. Kwa sababu hiyo, riwaya za usasa na usasaleo za Marekani kusini zimetoa hali tofauti ya ukweli. Fuentes anadai kwamba ni jukumu la waandishi wa riwaya ya Marekani Kusini kuuelezea 'ukweli (kivyao) wanavyouelewa'.

Katika miaka ya sitini vile vile, Julio Cortazar na Carlos Fuentes walipigia swali jitihada za falsafa za kimagharibi katika kufuta ukweli uliofanana, lakini ulioko katika mazingira tofauti. Yaani kulingana na Wamagharibi, ukweli ni bia. Fuentes na Cortazar wanasema kwamba jitihada ya utafutaji wa 'ukweli' kila wakati ni ya kimagharibi na yenye kupendelea mitazamo ya kimagharibi.

Nchini Chile, Allende ndiye mwandishi aliyeandika kazi zake za kwanza kwa kuiga mtindo wa uhalisiajabu uliotumiwa hapo awali na Marquez. Alitumia mtindo huu kuandikia riwaya ya The House of the Spirits (1981) inayohusu familia inayopitia katika mabadiliko ya kisiasa. Kama mtangulizi wake, anatumia uhalisiajabu kuyaangazia maswali ya nchi yake yakiwemo siasa (Encarta Encyclopedia 2002).

Nchini Cuba kazi za Alejo Carpentier zina mchango mkubwa kwa uandishi wa kisasa. Katika kazi zake The Kingdom of this World (1949) na The Lost Steps (1979), Carpentier anatumia mtindo wa usasa kuelezea historia na utamaduni wa Cuba kibunifu. Waandishi wengine kutoka Cuba waliotumia uhalisiajabu ni kama vile Miguel Angel Astrurias na Juan Rulfo.

Mwandishi mwingine anayetumia uhalisiajabu katika kazi yake ni Mario Llosa Vargos kutoka Peru. Riwaya moja aliyoandika kwa mtindo wa uhalisiajabu ni The Time of The Hero (1963) inayozungumzia maisha yalivyokuwa katika chuo kimoja alichohudhuria nchi yake ilipokuwa ikiongozwa na makadeti, ikilinganishwa na uhuru uliokuwa nje ya chuo hicho. Riwaya nyingine maarufu aliyoiandika Lloa ni Green House (1969) inayolinganisha maisha ya jangwa la Peru na maisha katika mazingira ya kimji ya Peru (Wamitila 2002).

Salman Rushdie ni mwandishi wa riwaya wa Kiingereza, mzaliwa wa India ambaye ametumia mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya zake. Riwaya ya Midnight's Children (1981) inahusu maendeleo ya kisiasa nchini mwake India, katika miongo iliyofuata kupata uhuru kwa nchi hiyo kutoka kwa Waingereza (Alexander 1990:127, 138-139).

Riwaya nyingine aliyoiandika katika mtindo huu ni ile iliyojaa ubishi mwingi ya Satanic Verses (1988). Alexander (1990) akinukuu maneno ya Rushdie alipokuwa akihojiwa kuhusu riwaya hii Rushdie alisema:

> Jambo moja mwandishi analoweza kusema ni hili: Hivi ndivyo unavyopaswa kuutazama ulimwengu, hata hivyo kuna pia njia zingine za kuutazama. Hebu tusiwahi kuamini kwamba jinsi watu walio uongozini watuambiavyo tuutazame ulimwengu ndiyo tu njia ya pekee kwa sababu tukifanya hivyo itakuwa ya kujiwekea vikwazo sisi wenyewe. (TY)

Kwa hivyo, tunaona kuwa Rushdie anapendekeza kwamba watu katika nchi yake wasijifunge kwa kila waambiwalo kuwa ndilo kila siku bali watazame na kuona linalowafaa wao wenyewe.

Katika bara la Afrika, wengi wa waandishi waliotumia uhalisiajabu ni wa kutoka Afrika Magharibi. Waandishi hawa ni kama CheneCoker wa Sierra Leone, Okri wa Nigeria na Kojo Laing wa Ghana (Cooper, 1998:1).

Oka (2002:90) akiielezea riwaya ya Ikri ya The Famished Road (1991) aliyomwezesha kutuzwa tuzo ya *"Booker"* (1991), anasema kwamba Okri anakagua kwa upekuzi maisha ya wananchi wa Nigeria. Anatueleza kwa undani historia ya nchi ya Nigeria kuanzia wakati wa ukoloni hadi wakati wa uhuru na maajilio ya utawala wa kijeshi. Kuzaliwa na kufa kwa mhusika Azaro mara tano kunasimamia miongo mitano ya utawala wa kijeshi, jamhuri ya pili na hatimaye utawala wa kijeshi tena. Oka (2002:90) anasema kuwa hadithi ya uhalisiajabu ya Azaro ni kielelezo cha hali ya umaskini na siasa za nchi ya Nigeria. Okri (1990:vii) anasema:

> Uandishi wangu ulikuwa zao la hasi umaskini ulionizunguka na mwelekeo mbaya wa serikali kwa mateso ya wananchi. Ulikuwa wakati wa ufisadi mwingi nchini Nigeria.

Kuwa mamlakani na uongozi na kuwa na nguvu kisiasa kulimaanisha kujinyakulia pesa kwako na jamii (kabila) lako. (TY)

Kwa muhtasari, ifuatayo ndiyo mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu:

(i) Matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.

(ii) Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na utohalisi katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo tumo ndotoni.

(iii) Mipaka ya kijamii, kitaifa ya kimataifa huvunjwa. Maanake ni kuwa wanahalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.

(iv) Wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaloweza kufanyika wakati mmoja (ambalo linaweza kuwa si la kwanza) linaweza kujiirudia kwa sura nyingine mahali pengine.

(v) Uhahalisiajabu umefungamana na sanaajadi kama vile visasili na hadithi. Visasili ni hadithi zinazoeleza asili ya watu na matukio fulani.

(vi) Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.

(vii) Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa.

(viii) Vilevile mimea, mito, maziwa na habari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.

(ix) Uhalisiajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbalimbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na wenyeji tamaduni huonekana zikiingiliana (Danow 1995:74), Cooper (1998), Zamora (1995), Drouart (1993) na Encarta Encyclopedia (2002).

Ni muhimu kutaja kwamba katika utafiti huu si mihimili yote itakayotumiwa. Itakayotumika ni ile itakayofaa zaidi kufafanua riwaya tunazozichunguza ili kuweza kuangazia hali zetu kijamii, kisiasa, kuchumi na kihistoria. Waandishi wanaitumia kwa muktadha wa kisasa na kupingana moja kwa moja na uhalisia wa kimapokeo uliozoewa.

## 1:9 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wetu utajikita katika maktaba. Sababu ya kwanza ya kufanya hivi ni kuwa hapa ndipo tutapata vitabu vinavyohusiana na riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo!. Vile vile, katika maktaba tutapata kazi za kusoma zinazokuhusiana na nadharia ya uhalisiajabu tutakayotumia katika kuhakiki kazi yetu.

Hatimaye, tutamhoji mwandishi wa riwaya hizi mbili, kwani jambo hili litatusaidia pale ambapo kutahitajika. Zaidi ya hayo, tutashirikisha maoni ya wataalamu katika taaluma hii hasa kuhusiana na mada na nadharia ya utafiti.

## 1.10 HITIMISHO.

Katika sura ya kwanza tumetambulisha utafiti wetu na kuonyesha unahusu nini. Mada ya utafiti, yale yaliyoandikwa kuhusu mada yetu, masuala na malengo ya utafiti, nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu, na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili, tutashughulikia vipindi vya uandishi wa mwandishi, K.W.Wamitila, hatua yake ya mwanzo ya uhalisiajabu,

## SURA YA PILI

## 2:0 UTANGULIZI

Katika sura ya kwanza tulitambulisha mada ya utafiti wetu ambayo ni kuchunguza jinsi uhalisi ajabu unavyojitokeza katika riwaya za Wamitila: Bina-Adamu! (2002) na Musaleo! (2004). Tulishughulikia masuala na malengo ya utafiti huu, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu, sababu za kuchagua somo hili na pia kuelezea upeo na mipaka ya utafiti wetu.

Katika sehemu hii ya pili ya utafiti wetu, tutashughulikia dhana za uhalisiajabu. Katika kufanya hivyo tutaweza kuelewa amekuwa akiandika kwa kutumia mitindo ya uhalisia hakiki na utandawazi, na ni kwa nini ameshughulikia kazi zake kwa kutumia mitindo ya uhalisiajabu.

## 2:1 VIPINDI VYA UANDISHI WA K.W. WAMITILA

Wamitila ni mwandishi, mwalimu, msomi na mhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Katika maisha yake ya awali alikulia Arusha nchini Tanzania. Alisomea shahada ya B.A na M.A katika chuo kikuu cha Nairobi. Baadaye alisomea shahada ya Ph.D katika Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani. Wamitila amechapisha makala na tahakiki za fasihi ya Kiswahili katika majarida mengi ya kitaaluma barani Afrika, Ulaya, Asia na Marekani. Baadhi ya vitabu vyake vilivyochapishwa ni Wingu la Kupita (1999), Nguvu ya Sala (1999), Bina-Adamu! (2002), Pango (2003) na Musaleo! (2004). Baadhi ya kazi zake ambazo hazichapishwa ni tamthilia ya Sumu ya Bafe, riwaya ya Kovu la jana, Wana wa Bundi na Mchezo wa Mende.

Mwandishi alinifahamisha wazi wazi kuwa ana vita vikali dhidi ya masuala ya utandaridhi (*Globalization*), jambo ambalo analipiga vita ni jinsi nchi za magharibi zinadhibiti na kujinufaisha na utandaridhi. Waafrika ndio wanaoumia wakati Ulimwengu mzima unajulikana kama *kijiji*. Kuwepo kwa utandaridhi na ulimwengu kuwa kijiji kimoja ni kwa manufaa ya Wamagharibi tu.

Mataifa ya ulimwengu wa kwanza ndio yanayofaidika kutokana kutandaridhishwa kwa ulimwengu. Riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo! Zinadhihirisha masuala hayo wazi wazi.

## 2.2 HATUA YA MWANZO YA UHALISIAJABU

Wamitila (2002: 117-118) anasema kwamba kazi za kihalisiajabu zimekiuka muundo wa kikawaida wa utanzu kama njia ya kuzuka na istiara ya miundo ya mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya ulimwengu. Sababu ya kufanya hivi ni kufanikisha kile ambacho kinaitwa "Ungamuzi wa kisiasa." Je, Uhalisiajabu unahusu nini? Kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu. Kwa mfano, wahusika wanaopatikana kwenye riwaya ya Marquez One Hundred years of solitude (1980) ambao huishi chumba cha choo bila kutambua, hupaa angani na shuka ya jirani. Wahusika wengi wa Juan Ruffo katika Pedro pramo (1959), ni wafu. Kwa mfano, msimulizi wa hadithi anaendelea kusimulia hata baada ya kufariki. Mfano mwingine ni ule wa msichana Rosa katika riwaya ya The House and the spirits (1981); Huyu msichana alizaliwa akiwa na nywele ya kijani na rangi ya uso ya majano.

Tunapata waandishi wa kazi hizi wanayakiuka matarajio ya uhahisia wa kisimulizi kimakusudi. Mpaka uliopo kati ya yale yanayowezekana unafutwa. Kazi hizi zinavunja muundo wa kikawaida wa utanzu kama njia ya kuzuka na istiara ya miundo ya mifumo ya kisiasa.Hii ni sifa inayoonekana katika Bina-Adamu!, Musaleo! na Zimwi wa Leo (2002). Kazi hizi zote zinaonyesha kwamba tangu mwanzo, uandishi wake (Wamitila) umekuwa na dalili au elemendi za uhalisiajabu.

Zimwi Wa Leo (2002) ni hadithi inayohuhusu zimwi moja ambalo linatoka mahali kusikojulikana na kukutana na watu waliokuwa wakiishi kwa amani na upendo. Watu hawa ni wenye moyo safi na wanapoona kuwa zimwi linakitamani chakula wanachokila, wanalikaribisha kwa mikono miwili. Tatizo ni kwamba zimwi hili halionekani kushiba, inabidi

watu hawa wafanye kazi kwa bidii sana ili kuweza kutosheleza mahitaji ya zimwi hili. Kwa upande wake Zimwi linawaona watu wanaoweza kulisaidia kujifaidi. Linawaza:

"Hawa wanaweza kunifanyia kazi nzuri sana' (Wamitila 2002:13).

Zimwi hili linawaza sana jinsi linavyoweza kuwashawishi hawa watu kulifanyia kazi. Hatimaye linajiwa na wazo kwamba likiwapa watu nguo nyingi na zawadi watashirikiana nalo. Zimwi hili linaendelea kutumia kutojua na wema wa watu wa jamii hii na kuanzisha mambo mengi ambayo wantu (kama vile walivyoitwa) waliyakubali bila kung'amua hatari iliyokuwepo. Kwa ufupi, Wamitila (2002) anaeleza kifumbo jinsi wazungu walivyoingia barani Afrika. Waafrika waliwakaribisha wazungu kwa moyo safi na bila tuhuma yeyote. Wazungu walitumia wema huo na kuchukua mashamba yao, na kuwafanya watumwa katika nchi yao wenyewe. Mwandishi anatupitisha kwenye vipindi mbalimbali kuanzia pale zimwi linapofika Afrika. Kwa sababu ya ile tabia yake ya 'kukaba' chakula tu bila kujali kilitoka wapi pamoja na hila zake, Wantu walianza kuliita 'kabaila' (Wamitila 2002.15).

Baadaye yule kabaila anabadilishiwa jina na Wantu. Kiini cha kumbadilishia jina ni baada ya kuanzisha viwanda, ajipatie pesa zaidi kutokana na kodi anayowatoza Wantu huku wao wakiendelea kuteseka tu. Aidha, kabaila anawafunza mchezo wa kamari ili Wantu wajipatie pesa nyingi, lakini kabaila ndiye anashinde karibu mara zote. Wantu wanapoona tabia hii ya kubeba na kuparia wanaanza kumwita ***Kabaila Bepari.*** Jambo moja linalostaajabisha kuhusu mchezo wa kamari ni kwamba kila anayeucheza na kushinda anabadilika kwa sura, tabia, na umbo. Anaanza kuota mikono na viungu vingi kama bepari. Kitabia anaanza kuwachukia wenzake polepole. Walichukua hii mienendo. Hawa ni wale waitwao *wazungu weusi.* Walichukua mienendo ya wazungu na kuanza kuwatesa wenzao. Wamitila (2002:29) anasema:

> Wantu waliopata pesa hawakuwa watu tena bali vizimwi vilivyokuwa
> na mikono kama ubepari. Vizimwi hivyo vilikuwa tayari kuvitumia vikono
> vyao kuua kama Bepari ili vipate pesa.

Bepari linakuwa halifanyi kazi ila kukaa tu na kula. Hali hii inalifanya linoneane na *kushindwa* na kazi yake ya awali ya kupitapita ili kuona kama Wantu wanafanya kazi. Vinawatumia vizimwi na vibepari vinavyofanana naye riale kwa ya pili kufanya hivyo. Hawa ni vibaraka *Wazungu-weusi* waliotumiwa na Wazungu ili kufanikisha lengo lao. Kwa sababu ya kule kutooga na kunoneana kwa Bepari, linaanza kutokwa na harufu mbaya sana kama ya beberu. Harufu hii inatanda kila mahali kama upepo wa msimu wa mvua. Tangu siku hiyo Beperu alipewa jina jingine. Wantu wanaliita beberu. Wamitila (2002:33) anasema kuwa hata baada ya kuondoka mnuko ulibakia ukienea .Waliokwenda viwandani walikumbana na mnuko wa Beberu. Hata pesa zenyewe zilikuwa na mnuko huo. Kila kitu kinanuka Beberu.

Mwandishi anataka kutujulisha kwamba hata baada ya wakoloni kuondoka, alama zake bado zipo. Athari za ukoloni bado zipo kupitia jinsi nchi nyingi za Kiafrika zinaendelea kutegemea nchi za Kimagharibi kwa misaada ya pesa, mikopo, madawa na hata vyakula.

## 2:3 KIPINDI CHA UHALISIA HAKIKI

Huu ni uhalisia ambao ulihusisha uchunguzi wa kihakiki wa hali ya kijamii, matatizo yanayoikabili jamii hiyo lakini hautoi suluhisho ya matatizo hayo. Uhalisia wa kihakiki unaelekea kuchukua msimamo wa ubaki fulani wa kuendelelezwa kwa hali kama ilivyo. Kwa mujibu wa Wamitila (20003:274), huu ndio mojawapo ya upungufu wa uhakiki huu. Kipindi hiki cha uandishi kinahusisha uandishi unaoshambulia maovu ya kijamii bila kuzingatia itikadi ya kijamaa.

Katika uandishi wa aina hii mwandishi huchora jamii jinsi ilivyo nzuri. Hata hivyo, katika jamii hiyo hutokea watu ambao huharibu uitaratibu ama kukiuka maadili ya kidini na kutatiza hali nzuri inayotarajiwa katika jamii husika. Upungufu wa mtindo huu wa uandishi ni kwamba utatuzi wa matatizo yaliyowakabili wanyonge hutegemea huruma ya wenye nguvu. Ina maana kwamba anayenyanyaswa asipohurumiwa na mnyanyasaji hali yake ya maisha haitabadilika.

Wanajamii wanategemea majaaliwa. Mtindo huu wa uandishi hauleti mapinduzi ya kimsingi. Jambo hili linafafanuliwa zaidi na mwandishi wa Kirusi Maxim Gorky. Ni mmoja wa wale wanaopinga mtazamo wa uhalisia hakiki na kuunga mkono nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Akielezea upungufu wa nadharia ya uhalisi wa kihakiki (Khaemba katika Gorky 1990:14) anasema:

> Uhalisia hakiki ni muhimu tu kwa kadri unvyoangazia kujimudu kwa zamani na harakati za mwanajamii kupambana dhidi ya hali dhahiri ---- Uhalisia wa kijamaa, kwa upande mwingine, hupambana kwamba maisha ni vitendo na uzalishaji ambao lengo lake ni maendeleo bila kizuizi cha uwezo wa binadamu dhidi ya nguvu za mazingira.( TY)

Maxim Gorky, anaendelea kusisitiza kwamba ingawa uhalisia hakiki ulionyesha matatizo na uozo wa jamii na kumulika maisha na matatizo ya mtu binafsi pamoja na mafunzo ya imani za kidini na sheria dhalimu za nchi, haukuonyesha jinsi ya kujinasua kutokana na hali hii. Pengine hapo ndipo Wamitila aliona wahusika wake walibaki pale pale wakiwa wamekubali nafasi yao. Labda haya ndiyo yaliyomfanya mwandishi kubadilisha mtazamo wake na njia yake ya uandishi. Lengo la Wamitila la kufanya hivyo likawa la kuwaumba wahusika wachochole, lakini waliokuwa na nia na ari ya kuzibadilisha hali zao kwa kupigana na utabaka na unyanyasaji. Wahusika walio na uwezo wa kuangalia hali yao ya maisha kama ilivyosababishwa na historia wala sio majaaliwa.

## 2:4 KIPINDI CHA UHALISIA WA KIJAMAA

Kwa mujibu wa Suchkov katika Khaemba (1999), nadharia ya uhalisia wa kijamaa ilizuka pale wanajamii waling'amua kwamba mahitaji ya jamii yanatawaliwa na mahitaji ya kiuchumi na wala si fikra za watu ama majaaliwa. Uhalisia wa kijamaa uliiona jamii jinsi ilivyo na ukaonyesha mikinzano iliyomo na chanzo chake.

Nadharia hii inapendekeza namna ya kutatua matatizo ya kijamii ili kuunda jamii mpya itakayokuwa bora zaidi na ikawa sharti kanuni za nadharia hii zizingatiwe na waandishi na wahakiki. Baada ya kongamano la waandishi lililofanyika mnamo mwaka thelahtini na nne (1934) nchini Sovieti ya zamani, uhalisia wa kijamaa ilipendekezwa kuwa msingi wa fasihi ya Kisovieti. Ilipendekezwa kuwa mwandishi wa fasihi katika Usovieti anapaswa kusema ukweli kuhusu jamii yake bila kuficha chochote. Katika kazi za fasihi, pia kulihitajika kuonyesha kipindi mahsusi cha kihistoria. Kwa kulichangia wazo hili, Lukacs (1963:91) anasisitiza umuhimu wa jambo hili kwa kuliona katika misingi ya uhalisia. Anendelea kusema kuwa sanaa ya kijamaa ni sanaa ya kitaifa kwa kuwa haiangazii mazingira mahsusi ya kihistoria ambamo jamii fulani imepitia. Tunaweza kusema kuwa kipindi hiki kilimwathiri Wamitila katika uandishi wake. Mtazamo huu hujaribu kuweka mkazo kwa uwasilishi wa uhalisia wa maendeleo ya kihistoria, yanachanganua mikinzano iliyomo katika Usoshalisti. Katika kipindi hiki mwandishi anachanganua kimakusudi itikadi ya kijamaa kuuelekeza uandishi wake. Lengo kuu hapa ni kuwa itikadi ya kijamaa inaweza kumsaidia kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na hata ya kisiasa.

## 2:5 KIPINDI CHA UHALISIAJABU

Wamitila (2002) katika Bertoncini (2004:1) anasema:

> Nimeamua kuandika riwaya hii (<u>Bina-Adamu!</u>) hivi ili kuweza kuzungumzia suala ambalo nahisi nisingeweza kulizungumzia kwa njia ya kawaida(kwa riwaya za kihalisia). Pili nimependezwa na mtindo wa waandishi wa Marekani ya Kusini ambao wanatumia mitindo sawa kama Juan Rulfo, Carlos Fuentes Gabriel na wengineo; na wametumia mtindo wa uhalisiajabu katika kazi zao.

Bertoncini anaendelea kuelezea kwamba ni baada ya karibu mwongo mmoja kupita tangu Kezilahabi kuandika riwaya zake mbili <u>Nagona</u> (1990) na <u>Mzingile</u> (1991), ambapo riwaya zingine kutokea. Kwa mfano, <u>Babu Alipofufuka</u> (2001) ya S.A.Mohammed <u>Bina-Adamu!</u>

(2002) na Musaleo! (2004) za K.W.Wamitila. Waandishi hawa wawili wameenda nje ya uhalisia, wametumia mbinu ya usakaji na wote wanaangalia dhana ya utandaridhi kwa jicho la ndani na pekuzi kwa sababu ya athari zake zinazotishia kuangamiza bara la Afrika. Ninamuunga mkono Bertoncini kuwa K.W.Wamitila ametumia mbinu ya uhalisiajabu katika uandishi wake. Akitoa ushahidi kuhusu jambo hili Gromov (2003:11) anaona kuwa mtindo wa usasaleo katika fasihi ya Kiswahili katika miaka ya themanini, waandishi wanaotumia mtindo huu walikuwa wa kwanza kuhisi kwamba uhalisia ulikuwa umeibuka kama mtindo wa kisanaa. Waliona kuwa uhalisia haukuweza tena kuyaakisi maswala ya jamii.

## 2:6 DHANA YA UTANDARIDHI

Kutengwa au kuwekwa pembeni kimaendeleo na kuzuka kwa mataifa yenye uwezo mkubwa kupita kiasi ni matatizo mawili ya utandaridhi. Makundi haya mawili ni matokeo ya utandaridhi. Utandaridhi umeleta utabaka katika ulimwengu, yaani Ulimwengu wa Kwanza na Tatu; Ulimwengu wa Kwanza unawakilishwa na bara la Afrika na baadhi ya nchi za bara Asia. Kuzuka kwa mfumo mpya wa kiuchumi ulimwenguni ni kutokana na utandawazi. Utandawazi umeleta mabadiliko yenye shauku kwa miongo michache iliyopita. Watandaridhi wanaona kwa mapana na marefu mabadiliko haya yamesaidia kueneza na kusawazisha utajiri ulimwengu kote. Lakini kwa wale wanaoupinga, wanaona kuwa umeleta madhara aina mbili:

Kwanza umeleta umaskini wa kupita kiasi na pili umeleta utajiri wa kupita kiasi. Matatizo haya yanaonekana sana katika ulimwengu wa tatu.

Kwa mfano, biashara ya kigeni ya Marekani inachukua asilimia mbili tu, jambo ambalo linadhihirisha jinsi mataifa ya Ulimwengu wa Tatu yanavyopuuzwa. Mataifa ya Ulimwengu wa Kwanza hayana ajenda kuu juu ya mataifa yanayoendelea isipokuwa kutaka kuwanyonya tu! Kutokana na asilimia hii ndogo, nafasi chache hutengewa watu wa nchi za Afrika na kwa hiyo kupata pato la kujiendeleza huwa vigumu. Mfano mwingine ni wa nchi ya Bolivia, ambapo

shirika au kampuni moja kutoka Marekani, *Bechtel*, ilipewa mamlaka ya kutawala maji ya Bolivia ambao ni malighafi ya nchi hiyo. Kubinafsishwa kwa haya maji ya Bolivia kulitokana na masharti makali ya Benki Kuu ya Dunia kama njia moja ya kuiondolea deni nchi ya Bolivia mnamo mwaka wa tisaini (1990).

Benki Kuu ya Dunia ililazimisha nchi hiyo kubinafsisha mtambo wa maji wa mji Mkuu wa *Cochabamba*. Benki Kuu Ya Dunia ilitoa vitisho vya kuzuia misaada ya maendeleo kwa nchi hiyo. Kampuni ya Bechtel, baada ya kufanikiwa kumiliki haya maji, walitoa masharti makali kwa wenyeji (PR Newswire). Wenyeji walilazimika kutoa kodi kwa kampuni hiyo ya kigeni. Hali hii ni mfano mzuri unaotuonyesha jinsi utandaridhi umeathiri ukuaji wa maendeleo wa nchi changa.

Kwa upande mwingine, utajiri usiokidhiri unaweza kukwamiza maendeleo. Tatizo hili linaweza kuonekana katika mazingira ya mijini, mahali kuna uharibifu wa mazingira, mioshi kutoka viwandani, utupaji ovyo wa taka, na uchafuzi wa hewa kwa jumla, huwa kitisho kwa maisha ya watu wanaoishi katika miji mikubwa na maeneo ya karibu.

Nchi ya Kenya inaweza kuwa mfano mwema kuonyesha jinsi suala la utandaridhi linavyoathiri mataifa machanga yanayokua kimaendeleo. Utandaridhi ni njia moja ya kudhoofisha uwezo wa nchi mbalimbali.

Pia unaonyesha jinsi maisha ya mtu binafsi yanaweza kubadilishwa na nguvu za utandaridhi. Vile vile unaweza kumtangamanisha na maeneo mengine ya dunia. Kwa hivyo, utandaridhi unaweza kumwaathiri mtu binafsi kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni kutokana na mabadiliko yanayotokea ulimwenguni.

Dalili za kuonyesha kuwepo kwa elementi za utandaridhi katika nchi, ni wakati taifa au kingozi ana tatizo na tatizo hilo linaweza kutatuliwa kutoka nje. Kwa mfano, Slobadan Milosevic alikamatwa na kufanyiwa mashtaka ya kimataifa. Kuna utandaridhi wa aina mbili:

Kwanza ni ule wa kutoka juu na wa pili ni wa kutoka chini. Utandaridhi kutoka juu ni ule dola moja linakalia lingine.

Kwa mfano kukaliwa kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Katika mfumo huu tabaka la wasomi linaloundwa na mashirika makubwa, yanaanza kuagiza bidhaa kama vile magari, bidhaa na njia zingine tofauti za kimaisha kutoka nchi zilizoendelea.

Kuzuka kwa makundi ya kupigania haki za wanawake katika nchi za ulimwengu wa tatu na mashirika kama vile *Grassroots Africa Watch, Amnesty International na People against Torture* ni mfano wa utandaridhi kutoka chini. Utandaridhi tunapata kuwa una misingi ya kibepari. Jambo hili linamaanisha kwamba elimumwendo ya utandaridhi ni ubepari wa ulimwengu wenye misingi ya kiuchumi. Wabepari wanapapia uzalishaji wa mali kwa njia rahisi au za mkato, kama vile kupata wafanyakazi wa mshahara duni na malighafi rahisi kutoka hasa nchi zinazoendelea. Hali hii inaonyesha kutanda kwa utandaridhi ulimwenguni kote. Ubepari mkongwe ulitumia nguvu nyingi, unyonyaji, mamlaka makuu yanayoambatana na ukoloni. Tofauti kati ya ubepari mkongwe na ubepari-mamboleo ni kuwa, huu wa leo unatumia maafikiano na ukubalifu au mapatano juu masuala mengi.

Mifano ya utandaridhi nchini Kenya ni kama vile utegemeaji wa misaada inayotolewa kwa masharti ya kiuchumi yanayoathiri chumi za nchi maskini ni kama hatua ya mwisho. wahusika wakuu katika kuendeleza utandaridhi ni mashirika makubwa yanayofanya maamuzi yanayohusu maendeleo, mizozo ya kisiasa inakuwa ndiyo soko na suluhu kwa nchi za kimagharibi. Kwa mfano, utawala wa Mugabe, Zimbambwe, ulilaumiwa na mataifa ya Kimagharibi. Mauaji ya Jones Savimbi, aliyeuawa na wakereketwa wa kikomunisti huko Angola, na hata kundi la kuleta amani huko Afghanistani.

Vile vile masuala ya kidemokrasia yamekuwa ya kitandaridhi. Mataifa ya kimagharibi yanaamini kufaulisha ubepari ni kupitia sera ya demokrasia. Kubadilishana mambo ya kitamaduni pia ni hali moja ya kufaulisha utandaridhi. Mikutano ya pamoja ya kuweka

mapatano ya kimataifa kama vile kuharibika kwa utandu wa 'Ozone' ni njia nyingine ya kuendeleza utandaridhi. Vile vile sifa nyingine ya utandaridhi ni uhuru wa masoko huria, ambao umeleta kulundikana kwa bidhaa sokoni na utupaji wa bidhaa duni katika ulimwengu wa tatu. Vile vile utoaji wa kandarasi kwa watalaamu wa kigeni kusimamia kutekelezwa kwa mabadiliko haya ya kiuchumi ni mfano mwingine wa utandawazi. Sifa hizi zote za utandaridhi zimejadiliwa kwa mapana na marefu katika kazi hizi mbili za Wamitila. Amejaribu kuyaangazia kwa njia ya kistiari. Kwa hivyo hali hii ya utandawazi ndio imemwathiri sana huyu mwandishi wa kazi hizi mbili, Bina-Adamu! na Musaleo!. Hebu sasa tupate mifano michache kutoka kazi hizi teule.

Chagina katika Bina-Adamu! ametuchorea dunia kama mahali pa fujo. Kila kitu kimeumbwa na kanuni zake. Kila siku kuna watu wajanja, waliokaa mifuko wazi kungojea kuingiza utajiri unaotoka kwa mabwege walio tayari kufungua bongo kuzisokomeza undanganyifu unaoitwa *dhana za kilimwengu*. Lugha inayozungumzwa ni tamu: "*globalization*" uhuru wa kibiashara, lakini uhuru huo umo katika mshawasha wa vyombo wanavyomiliki na udhibiti wao.

Mnarejeshwa nyuma kwenye ule uliokuwa ukiitwa ushenzi kwa kile kinachoitwa usasa na fesheni. Na ubaya wa mambo hayo yote mnayanunua kwa bei hasi au duni kwa sababu mifuko yenu i mitupu, tayari kufanya dhambi yo yote ile kuigundua fedha ya kununua. Katika Musaleo! (2004:90), mwandishi anasema kuwa utandaridhi umekuwa wimbo unaoimbwa na kila mmoja au na kila mtu. Kuna wale wanaodai kuwa wimbo huu ulisababishwa na upepo wa mwisho unaoitwa *Ikti-saad* ya masoko huru (Free *Market Economy)*. Wengine husema hayo yote yalisababishwa na sayansi. Utandaridhi umevunja mipaka na kuvunja majimbo, unakata masafa marefu na kuufanya ulimwengu kuelekea kuwa kijiji.

Chagina anatoa sauti kwa kusema kuwa jamii inahitaji kujielimisha upya kuanzia chini hadi juu, mtoto hadi mzee, wote. Huu ndio ukombozi ufaao; matakwa ya jamii yawekwe mbele.

Kumbuka siku za ukombozi kuletwa na mtu mmoja zimepita!—Unganeni kiuchumi, kisiasa na kijamii. Umoja ni nguvu (154-155).

## 2:6 HITIMISHO

Katika sura hii ya pili tumejadili historia ya uandishi wa K.W.Wamitila (2002 na 2004), na tumeonyesha vipindi ambavyo mwandishi amepitia katika uandishi wake hadi kufikia kuandika katika mtindo wa uhalisiajabu. Kwa kweli tumeonyesha vipindi hivi kwa lengo la kubainisha ni kwa nini mwandishi huyu akaasi mitindo ya kimapokeo na kuanza kutumia uhalisiajabu. Katika sura hii pia, tumejadili dhana ya utandaridhi na kutoa mifano kutoka maeneo mbalimbali ili kuifafanua mtazamo wa mwandishi.

Ni bora kuielewa dhana hii kwani ndio imejitokeza kwa kiwango kikubwa katika kazi hizi mbili, Bina-Adamu! na Musaleo!.

Kwa hivyo, tunaweza kudai kwa dhati kuwa Wamitila aliandika kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu kimakusudi. Alijua kuwa kuna njia nyingi za kuandika, lakini aliamua hivi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ifaayo zaidi, kupitia uhalisiajabu. Katika sehemu inayofuata, tunadhamiria kutoa muhtasari wa riwaya hizi mbili Bina-Adamu! na Musaleo!, vile vile kujadili vipengele vya uhalisiajabu vinavyojitokeza katika riwaya hizi. Baadhi yavyo ni kama vile matukio ya kiuhalisiajabu, kuchanganyika kwa ndoto na uhalisia, uduara wa wakati, uvunjaji wa mipaka, upekee wa mtindo wa riwaya na nafasi ya visasili katika riwaya za kihalisiajabu.

## SURA YA TATU

### 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tulichunguza historia ya mwandishi K.W.Wamitila ili kubainisha muktadha uliomfanya kutumia mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya hizi mbili. Kutokana na uchunguzi wa uandishi wa Wamitila, imedhibitika kwamba mwandishi huyu aliandika katika mtindo wa kiuhalisiajabu, si kwa kutofahamu anachokifanya au kushurutishwa; alifanya hivi kwa sababu muktadha aliokuwemo ulimfanya kutumia uhalisiajabu katika utunzi wake. Ushahidi wetu umepatikana katika usomaji wa kazi zake, tahakiki za kazi zake na mazungumzo ya ana kwa ana. Katika sura hii tunadhamiria kutoa muhtasari wa riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo! Tutatoa maelezo ya hadithi katika kazi hizi mbili kuanzia mwanzo hadi mwisho wao ili kutoa mwanga wa hadithi hizo kwa jumla. Tutaanza na riwaya ya Bina-Adamu! Kisha tutashughulikia Musaleo! Hii ndiyo itakuwa sura ndefu sana katika kazi yetu.

### 3:1 MUKHTASARI WA RIWAYA YA BINA-ADAMU!

Bina-Adamu! ni riwaya inayotumia sitiari ya kijiji kuangalia hali ya mataifa ya ulimwengu katika kipindi hiki ambapo hali za kijamii, kisiasa na uchumi inadhibitiwa na ubepari wa mataifa yaliyoendelea. Riwaya hii inahusu hadithi ya mtu mmoja anayeanza safari ya ujisakaji. Jukumu la Bina-Adamu Msafiri ni kuwasaka na kuwakamata huntha watatu waliotoweka ili kuondoa laana na misiba inayowafika watu wa kijiji chake. Katika safari yake, Msafiri anapitia mahali mbalimbali na kuona watu mbalimbali. Msafiri hata hivyo, hawapati huntha hao kwa sababu hawako dhahiri bali akilini tu. Licha ya haya anafanikiwa kukutana na P.P. Huyu ni kiumbe anayeonekana kutawala ulimwengu mzima.

Ajabu ni kwamba huyu P.P. si kingine bali jitoto tu (Peter Pan). Sehemu ya kwanza ya riwaya ya Bina-Adamu! ni maelezo juu ya kijiji ambamo Msafiri alizaliwa. Kuna imani kadha zinazotawala kijijini humu.

Mojawapo ni kwamba hakuna mtu anayepaswa kwenda kwenye kiini cha kijiji. Licha ya imani hizo, Bina- adamu anazipuuza na kwenda huko. Huu unakuwa ndio mwanzo wa safari yake ndefu.

### 3:2 SEHEMU YA KWANZA

Sehemu ya kwanza ya riwaya hii ni sura ya kwanza ambapo Bina-Adamu anasimulia kuhusu kijiji chao. Anasema kwamba, alipozaliwa aliwakuta watu wakiogopa kiini cha kijiji chao na mpaka wa leo wanakiogopa (uk 7). Kijijini mwao kulikuwa na wakazi watatu tu. Mmoja ni mhubiri aliyetorokwa na mkewe, kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Mkazi wa pili ni Kichaa aliyeishi kwenye kibanda. Wanakijiji wanasema kwamba Kichaa huyu alikuwa mganga kabla ya wao kumbatiza Kichaa. Mkazi wa tatu, alikuwa hajulikani kwa jina na watu wengi kijijini. Hata hivyo, alikuwa na watoto watatu huntha walioondoka zamani na haijulikani walikozamia. Kichaa alitumia wakati wake mwingi kuwatafuta. Wanakijiji wanaamini kwamba wakipatikana wataleta matumaini kijijini. Huntha hawa walikuwa wamelaaniwa. Ili kuondoa laana hii ni lazima hawa wajalaana waondolewe ulimwenguni ili kuiondoa laana iliyotanda juu ya anga ya kijiji. Hivi ndivyo Bina-Adamu walivyosimuliwa kila wakati walipokuwa wakikua. Mageuzi haya yakifanyika Bina-Adamu ataishi alivyotakiwa tangu hapo (uk 8).

Bina-Adamu anaanza safari yake kwa kupuuza imani ya hapo kijijini, kwamba hakuna mtu anayekaribia kiini cha kijiji hicho kwa sababu anaweza kupatwa na madhara makubwa. Jagina hakuamini jambo hili, kwa sababu nyanya yake alikuwa na uzoefu wa kudanganya sana.

Mwanamume atakayeenda huko anaweza kushtukia amebadilisha jinsia na kuwa mwanamke, kwa kuwa ni lazima alizunguke jabali kubwa lililoko hapo (uk.9).

Ingawa anaanza safari yake bila kukadiria ukubwa wa jukumu lake, mara tu anapotambua anachohitajika kufanya anakubali jukumu hilo na kuendelea na hii safari.

### 3.3 SEHEMU YA PILI

Sehemu hii inaendelea hadi sura ya ishirini na tatu. Hii ni sehemu refu sana kwa sababu inahusisha safari nzima ya Bina-adamu. Msafiri anao wasaidizi katika safari yake. Mmoja ni msaidizi asiyeonekana ambaye daima humwongoza kwa kumpiga makofi na mateke. Mwingine ni mwanamke anayejulikana kama Hanna, ambaye anamkumbusha Msafiri bibi yake kwa sababu anafanana naye sana. Bina-Adamu anapokuwa amesimama huku anawaza kuhusu jambo hilo, anapigwa teke na kuambiwa aanze safari yake ya uvumbuzi .

Anafuta viunzi vinavyokuwa vikitoa mwangaza kwa sababu giza jingi mno ndani ya pango wanamoingilia. Katika kibao alichokiona kilikuwa kimeandikwa 'Njia ya uhalisi.' Anapoendelea anainusa harufu ya beberu na kusita kidogo. Mara analiona jitu nene lilikuwa limeandikwa **EURO-JAPA**. Lilifuata ghafla na kufuatwa na kicheko kikubwa (uk 2002:14).

Mara wanatumbukia kwenye mto uliokuwa na maji mengi ajabu. Ajabu ni kwamba mkondo wa maji uliwavuta wakawa wanarudi nyuma nyuma tena kwa kazi ya ajabu. Mahali anapojikuta ni nchi ya Zakongwe. Akiwa huku anabadilika na kuwa mtoto mdogo. Anahimizwa na babu ajiunge na watoto wenzake kucheza michezo kama vile mwajificho, kuchunga ng'ombe, kufukuza wanyama wadogo msituni na kusikiliza hadithi za babu jioni. Msafiri anafurahia maisha ya huku, sababu ni kuwa huko ni 'jana' ambapo maisha ni ya raha na upendo.

Hata hivyo, ni lazima aendelee na safari, ili kukamilisha jukumu lililo mbele yake. Kabla ya kuondoka, babu anampa mfuko ambao anamwambia autunze sana kwa sababu ndani yake mna "utu, mapenzi na kiini cha kuwako kwake." Kwa bahati mbaya anachukuliwa kimiujiza na kutoka bila kutarajia na anaucha huo mkoba. Tukio hili linatokea siku moja wanapokuwa wakicheza mwajificho na watoto wenzake. Karibu na mto analiona joka kubwa na anapokuwa

akitoroka anaanguka majini na mawimbi yanambeba. Bina-Adamu anajikuta kwenye mto wa ajabu. Hajui kuogelea lakini anajipata akielea majini!

Safari yake ya majini inakatizwa na kisiki kikubwa kilichokingama mtoni. Kisiki hiki kinamgonga na ghafla kinamviringisha juu juu kama mpira na anaanguka nchi kavu. Hapo ndipo anakutana na msaidizi wake Hanna kwa mara ya kwanza. Wanapokuwa wakitembea wanatokezea mahali ambapo kuna majengo ambayo hayajakamilika. Sababu ni kuwa wanaume wote wenye nguvu wamesombwa na kuchukuliwa na Umero-Japa (uk.28). Jambo hili linaonyesha madhara yaliyotokana na muungano kati ya Uropa, Marekani na Japani. Msafiri anakumbuka jitu alilokuwa ameliona mbeleni lenye maandishi Umero-Japa (Bertoncini 2004:3). Kituo kingine wanakokwenda kina machimbo ya madini. Hakuna mmea hata mmoja ila bundi wengi walioko katika mapango hayo. Anajulishwa kwamba hayo machimbo yalikuwa na dhahabu, fedha na ulanga. Watu walihimizwa kuchimba kwa ahadi ya kulipwa lakini hawakupata kitu. Waliofaidi ni waliopora madini yenyewe (uk.29). Msafiri anaendelea kupita mahali mbalimbali ambapo ingawa hakutajwi kwa jina, kunatambulika.

Katika riwaya hii, bundi anaashairia mambo yanayopingana. Katika mapokeo ya kimagharibi anaashiria hekima na werevu. Bina-Adamu anapomwona mwanamke mmoja akiwa na huyo bundi anauliza kwa nini amembeba na anaambiwa kwamba kule Ropa bundi ni ishara ya busara (uk.33). Ikiwa hivyo, bundi hawezi kufasirika kwa njia moja. Ikiwa ndege huyu huashiria bahati nzuri au mbaya, jambo hili basi humsaidia mhusika kutumia uamuzi wake kuhusu jambo zuri au baya.

Nchini Ujerumani anawapata watu walioshika tama. Nyuma yao pana jengo kubwa ambalo halijakamilika na ambalo hawataki kuliangalia. Jengo hili liliharibiwa wakati wa Vita vya Pili vya Ulimwengu (Vita vya Vyura au Hitler). Watu hawataki kulitazama jengo hilo kwa sababu linawakumbusha jana (ambayo hawataki kuikumbuka). Aidha, hawataki kulibomoa kwa sababu

hawataki kufuta jana yao (uk.36). Huko huko Ujerumani Msafiri anashuhudia visa vya ubaguzi wa rangi.

Msafiri anajiambia kwamba ubaguzi wa rangi huenezwa na utandaradhi. Aidha, anakumbana na Joseph Mengele, ambaye ni maarufu na madaktari wenzake. Kazi ya Mengele ni kuchunguza watu wasio na mbegu zifaazo za uzazi kisha kupendekeza njia za kuwaangamiza. Angeweza kuitwa daktari wa kifo. Dhamira ya kufanya hivi ni kuhakikisha kwamba jamii inayokua huko ni jamii inayoweza kuendeleza sifa nzuri; yaani watu wenye akili stadi na wasiokuwa wanyonge! Jambo ili linatukumbusha jamii kamilifu aliyotaka kuianzisha na kuiimarisha Hitler wakati wa utawala wake. Aidha, tunakumbushwa nia ya Hitler ya kuwaangamiza Wayahudi wote kutoka ulimwengu alipokuwa dikteta. Hatimaye, kusudi la kuwafanya wanadamu wote watawaliwe kwa mfumo mmoja (wa ulimwengu) wa kiuchumi na kijamii, unawasilishwa katika dhana hii. .Ulimwengu unalazimishwa kuwa kijiji. Msafiri anagundua kwamba, huko Uropa, makanisa yamegeuzwa kuwa hoteli. Huku kunaonekana foleni refu za vijana wanaongojea kutazama sinema za kimarekani kama vile *Star Wars, Rocky V* na *Missing in Action.* Msafiri anambiwa kwamba hawazitamani sinema za kwao. Jambo hili linatuonyesha jinsi ambavyo Waafrika walivyokengeuka. Hawajiamini na hawaoni kuwa kitu chao ni kizuri. Jambo hili tunaliona sio kwa sinema tu bali hata vile wengine hupendelea mitindo ya nguo za kigeni, na hata kuongea.

Si ajabu basi Waafrika wanaogopa kuchukua nafsi yao katikati mwa kijiji (ulimwengu) na kutosheka kukaa pembeni. Ni wazi kwamba Waafrika wana jukumu kubwa katika kuamua watakaa wapi, pembeni au kwenye kitovu ?

Nchini Urusi ingawa watu ni maskini ni wenye bidii na mkono wazi. Msafiri anashuhudia katika nchi hii. Pia ni wenye matumaini. Msafiri anapewa mfuko uliojaa vitu kama zawadi. Kimojawapo cha kitabu anachopewa kinahusu hadithi ya mzalendo anayejulikana kama **Che**.

Ni hadithi ya ukombozi na ufahamu. Che ni jasiri anayesimama wima kupambana na Yanguis-ngavu kuu katika ulimwengu (uk.81).

Baadaye tunamwona Bina-Adamu akiwapatia kitabu hiki watu wa mojawapo ya nchi anazozizuru ambao anaona kwamba wanahatiji ukombozi na viongozi kama Che. Urusi ni tofauti na kwingine ambako watu waelekea kipindi cha ukimya kwa sababu kila mtu atakuwa anategemea teknolojia ya mashine na kwa hivyo hatakuwa na haja na binadamu mwenzake.

Japani ni kwengine Msafiri anapokwenda. Huko kuna ishara ya maafa yaliyowapata watu. Wengi wamelemaa mikono na miguu. Watoto wengi anaowaona wana alama alama kama waliomwagiwa kitu fulani kilichowababua ngozi. Inasemekana kwamba P.P. (Marekani) alitupa bomu fulani na watu wengi wakafa na wengine kuathirika vibaya sana. Tangu wakati huo watoto wanaozaliwa ni vilema. Huko Japani anaona magari mengi ambayo hayatumiki tena lakini ambayo anaambiwa yana soko kubwa upande wa chini kwa sababu huko ndiko wanapotupa vile vitu ambavyo hawavihitaji tena. Anajulishwa kwamba hapo karibuni hata samaki wabichi watakuwa wakiuzwa huko kwa sababu ingawa kuna maziwa mengi ya kuvua, wale wanaouziwa (Waafrika) hawana idhini ya kuvua kwenye *International waters*. Msafiri anashangaa kama hiyo ndiyo maana ya *free market economy* na *llberalisation*. Anashangaa kama hayo ndio maendeleo na kama ndio maana ya ulimwengu kuwa kijiji.

Msafiri anapotembea kutoka bara moja hadi lingine anakumbana na watu ambao wamekuwa maskini kwa sababu ya uchumi unaitwa wa soko huru. Watu kama hawa wanamwita Bina-Adamu mkombozi wao na kumtuma kwa P.P., wengine wanamwambia amwambie P.P. kwamba hawajasahau mabaya yote aliyowatendea.

Jagina anatembelea kijiji chao ambacho kinawakilisha Bara la Afrika. Anapumzika huku kwa muda mrefu. Katika kijiji (Bara la Afrika) kuna nyumba (nchi) zifikazo hamsini na mbili. Nyumba nyingi zimeinamiwa na miti mbalimbali ya matunda kama vile miembe, mipaipai, michungwa na mingine mingi.

Kila kiongozi anakaa juu paani anakochana matunda kwa urahisi na kuwatupia watu walioko chini ambao ndio waliomshikia ngazi ya kupanda juu. La kusikitisha ni tabia ya wengi wa viongozi wa nchi hizi. Baada ya kula na kushiba, wao huyatua makokwa na maganda huko chini yanayong'ang'aniwa na umati mkubwa ulioko chini. Baadhi yao hata huiba matunda na kuyahamisha kwingine, labda ughaibuni. (Uk.67-68).

Hawa viongozi wa Kiafrika wanao uvimbe kwenye nyuso zao. Uvumi unasema kwamba walipigwa kwa jiwe lililotupwa na Goliath! Ajabu ni kwamba kisa cha Biblia husema kwamba Daudi ndiye aliyempiga Goliath (uk 70-71). P.P., kama anavyowahangaisha watu kwingineko ndiye aliyehusika na uvimbe huo. Mwandishi anadhamiria kuonyesha kwamba wengi wa viongozi wa Kiafrika wameambukizwa tabia ya unyanyasaji na dhuluma kwa wanyonge. Ukweli ni kwamba huyu Jagina anaelezewa kwamba matatizo yanayokabiliwa na nyumba za kijiji hiki yanafanana lakini wakazi wake hawashirikiani ili kuyatatua. Wanasema kuwa kila nyumba ina kiongozi wake na hawataki kuingilia kati (uk.72)

Hapa Msafiri anairejelea mikataba mibaya kati ya nchi mbalimbali za bara la Afrika. Licha ya kwamba nchi za Ulaya zinaendelea kuungana. Waafrika nao wanaendelea kutengana kwa sababu za kibinafsi, ufisadi na ulafi wa viongozi.

Jagina anapokuwa hapo anashuhudia kisa kama hiki moja kwa moja. Alikuwa mtoto mdogo ambaye alikuwa ameumia katika harakati za kutoroka nyumbani (nchini) baada ya vita vya kung'ang'ania kukwea paani. Jagina anajulishwa kwamba hayo ni matukio ya kila wakati. Kila mmoja hutaka kukwea na akishindwa huichoma nyumba (2002:73).

Nyumba (nchi) nyingine ambayo Jagina anaitembelea ina maajabu yake. Kiongozi wa hii nyumba ambaye ni dikteta anaigopa historia. Nchini humu, Jagina anayaona magofu. Anapouliza hayo magofu ni ya nini anaelezwa na mzee mmoja kwamba ni ya kituo cha usomi kilichofungwa, kwa sababu walisema malengo yake ni mabaya.

Baadaye hospitali inaanzishwa lakini pia inafungwa baada ya dawa kuuzwa na wanasiasa ili wapate pesa za kufanyia biashara! Wanapoulizwa kwa nini wanafanya vile, wanasema kwamba sio neno. Eti hayo ni matatizo ya kawaida yanayompata kila mtu katika dunia nzima wanayoita kijiji, *global village*! (2002:87).

Mzee huyu anaendelea kumjulisha Jagina kwamba kwa kweli harakati ambazo zinaendelea siku hizi katika hali yake ya sasa ni maangamizo. Hamna cha *global village* tena bali ni uharibifu wa sayari yenyewe pamoja na wakazi wake. Kulingana na huyo Mzee, hiyo ni *global village* (yaani uporaji wa ulimwengu).

Mzee huyu pia analalamika kuhusu Shirika la Fedha la Ulimwengu (IMF). Anasema kwamba jamii zimekosa uhuru wa kuamua kesho na hatima yao kwa sababu uwezo huo umeingiliwa na mtaji unaoweza kuingia na kutoka utakapo. Yaani nchi zinazotegemea fedha za IMF haziwezi kujipangia mambo yao kwa sababu hawajui ni lini watapata pesa (2002:87).

Jagina anapokuwa anatembelea karibu na ukingo wa bahari anakutana na watu wanaolalamika kwamba mafuta yamemwagwa baharini na kuwauwa samaki wote. Kwa kufanya hivi wale waliomwaga mafuta watapata sababu ya kuuza samaki wao wa makopo. Hawa ndio wanaotupa nyuklia huko juu.

Jagina anapoulizwa kwa nini watu hawashirikiani na kupinga vitendo kama hivi anaambiwa kwamba tatizo ni ubinafsi. Kila nyumba ina mwelekeo wake. Ubaya ni kwamba kidole kimoja hakivunji chawa. Tatizo la pili ni kwamba hizi nyumba (nchi) zinashindwa kujitoa kwenye pingu za wadhamini kwa sababu wao ndio waaribifu wakuu.

Nchi nyingine ambayo Jagina anaitembelea imekumbwa na tatizo la uzungu weusi. Watu wanalalamika kwamba ndugu yao, mwenye rangi kama yao anawabagua. Ndugu yao anakwea juu ya mti wa matunda na kuanza kula matunda peke yake na wenzake wachache. Ndugu zake wanalia kwamba huyu ndugu yao anaiba hata na mbegu. Wangekuwa na mbegu wangepanda na kuiongeza idadi ya miti na angaa kuhakikisha kwamba keshowe matunda yamewafikia watu

wengi zaidi (2002:91). Kinaya ni kwamba kiongozi huyu amezungukwa na waimbaji ambao hutunga tenzi mpya na kuzikariri kama sala ya bwana eti kwa sababu yeye hupenda kusifiwa. Huyu kiongozi anajulikana kama Musa wa leo na watu wakiwemo watoto wa shule wamefunzwa hivyo.

Inasemekana kwamba yeye ni kila kitu na akiondoka ataliliwa sana. Huyu kiongozi anafananishwa na Musa wa Biblia aliyewaongoza na kuwatoa Wanaisraeli utumwani Misiri. Baadaye usiku Jagina anaanza safari yake tena baada ya kupumzika kwa muda mrefu. Babu yake Zakongwe anamletea mkoba wake mlimokuwemo na utu.

Anapopita karibu na ziwa fulani anashuhudia watalii ambao wamezivua nguo zao huku wakicheza na wasichana wadogo sana wa Kiafrika waliovaa visketi vinavyofika magotini na viblauzi vinavyoning'inia tumboni. Aidha, kunao wazungu wengine wanaonasa matukio hayo kwa kamera zao za video. (2002:108).

Mkondo wa mwisho wa safari ya Jagina unaanza. Anafahamishwa kwamba hatafanikiwa kuwapata wale huntha na kurudi nao pale kijijini basi hakuna matumaini ya kijiji chao. Ikiwa hatawapata anaambiwa ahakikishe angaa amewajua, kwa sababu hawa wasichana-wavulana si dhahiri bali ni vielelezo vya matatizo makuu yanayozikabili nchi za Afrika. Ndio maana anaambiwa kuwa hata kama hataweza kuwashika kwa sababu mwandishi anajua si dhahiri au halisi, hayashikiki wala kubebeka ahakikishe kwamba ameyajua matatizo hayo. Sababu ni kuwa amezuru mahali kwingi na kuona mengi. Sasa anaweza kufikia uamuzi fulani kuhusu shida hizo (2002:110).

Jambo hili linadhihirika zaidi wakati Jagina anapoambiwa ni muhimu waukubali uhalisia wao na kujaribu kubadilisha hali zao badala ya kukimbilia ng'ambo kwa sababu wasipopata suluhu kwa matatizo ya nchi yao, watakimbia milele kama vile Jagina anavyofanya. Katika safari hii anapitia karibu na bahari na anawaona watu wavua samaki kwenye *international waters* ili wawauze wakiwa kwenye mikebe. Aidha, analiona jahazi lililo na maandishi **AMISTAD I.**

Anakumbuka kwamba hili ni jina la meli iliyotumiwa kuwabebea watumwa kuwapeleka nchi walikokwenda kuhudumu katika mashamba ya mamwinyi zama za utumwa (2002:116). Historia inaletwa mbele ya macho yake. Aidha, historia hii inawasilishwa kwa muhtasari na kuonyesha kwamba utumwa umerejeshwa upya katika majoho mapya.

Inambidi Jagina kuvuka bahari tena ingawa si ya kweli bali ya ishara kama vile Hanna amwambiavyo ili kutoka nchi ya jana (Afrika) na kwenda nchi ya leo (Marekani). Anapofika Edeni ya pili (Marekani), anawaona wanaume na wanawake wanaokaa wakiwa uchi. Anapowauliza kwa nini wako hivyo wanamwambia kwamba wanakaa hivyo ili kuhisi kama wako 'jana' kwa sababu leo yao haina furaha.

Kwa kukaa uchi wanatafuta furaha kwa kujikurubisha na maisha ya kitamaduni ya kiAfrika. Ili kusisitiza jambo hili, mwandishi anatusawiria baadhi yao wakiwa wanakaa juu ya miti kama wanyama.

Wanahisi wako pweke na hawana mahusiano ya kibinadamu kwa sababu wametupa mkoba wao kama ule Jagina alipewa na Zakongwe na babu. Hawana utu au ubinadamu wowote. Hata Jagina anaogopa kwamba watauona mkoba wake na kudai ni wao. Msafiri anapotembelea katika kijiji cha wakazi Waafrika, anawakuta watoto wakicheza kandanda makaburini na hakuna anayejali kuwakanya. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa wanataka wageni waone na kupigia swali jambo hilo. Kwa sababu watu wa nje hawajui kwa nini kuna makaburi mengi hapo. Watu waliozikwa hapo ni watu weusi waliokufa baada ya kutumiwa kama panya wa maabara katika majaribio ya dawa fulani. Watafiti hawa wa Kimarekani hawakufanya majaribio na watu wa jamii yao bali na Waafrika. Jambo hili linaonyesha jinsi Waafrika wametumiwa na wanavyotumiwa hata leo na Wamagharibi ili kutimiza malengo yao kwa manufaa yao tu! Jagina anaambiwa kwamba watu hawa wanaishi katika urazini wa kuwili na wao hujijua kupitia macho ya wengine na pia kuishi pembezoni. Kwa bahati mbaya, hiyo ndiyo tanzia ya rangi.

Kinyume na Wamarekani wazungu wanaoishi jana, Wamarekani weusi wanaishi leo. Hawaishi katika ndoto bali kwa ulimwengu wa kweli-uhalisia.

Msafiri anaporudi mjini anaingia katika kiwanda kimoja cha utafiti. Mwanasayansi mmoja anamweleza kwamba wanaishi kesho na mtondo. Hawaishi kwa matumaini bali kwenye uhalisia wa kisayansi huku wamesahau jana kabisa. Kwa mujibu wa maelezo ya Mwanasayansi huyu, ulimwengu unaweza tu kuokolewa na shujaa ambaye atakuwa amejitegemea na anaishi kivyake. Binadamu huyu atakuwa amejikomboa na minyororo ya historia na 'uchafu wa utamaduni'. Huyu ni binadamu aliye na ujasiri wa kuasi jana.

Hata hivyo, sauti iliyomo katika akili ya binadamu inakataa kauli hii na kumwambia kwamba jamii inayosahau historia yake inashindwa kujieleza. Hiyo ni jamii ghibu ambayo haipo na inayotajika kwa jina tu (2002:129).

Hatimaye, Msafiri anatokea mahali kuliko na uwazi. Hapo anaona jamaa fulani akiwa ameketi. Alikuwa ameiweka mikono yake kwa namna iliyowafanya watu wengine wajazane katika duara iliyoundwa na mikono yake.

Watu hawa ni kimo na rangi tofauti. Baada ya muda lile pande linakunjua mikono yake lakini wale watu wanabakia pale pale walipokuwa (2002:147).

Butwaa isiyomithilika inampata Msafiri anapogundua kwamba lile jamaa ni toto tu! Linakula *humburger* huku vipande vipande vikiwaangukia wale wanaokuwa wakiliimbia. Linakula kwa pupa huku likitiririkwa na nyute pande zote mbili za mdomo.

Hatimaye sauti fulani inamwuliza Msafiri kama anamjua huyo anayejulikana kwa majina mengine kama 'Mjomba' au *Peter Pan*. Hiyo ndio sababu yeye hutupa mawe. Anaambiwa kwamba watoto wote wako sawa lakini kuna tofauti moja kuu kwa sababu watoto wote hukua isipokuwa *Peter Pan*. Yeye atabakia mtoto milele (Wamitila 2002:151).

Baada ya muda mfupi lile toto linasimama na kumwambia Msafiri kwamba linafahamu kwamba alikuwa akimtafuta. P.P anamuuliza atafanya nini kwa sababu sasa amemjua.

Bina-Adamu anamwambia kuwa atawaambia wenzake wasifanye kosa la kumpa uungu. P.P. anamjulisha Msafiri kwamba atakuwa anapoteza wakati kwa sababu tayari amewaingia akilini kabisa walimwengu. Anaendelea kumwambia kuwa anahisiwa kwingi hata asikokuweko. Kwa kweli, P.P anamwambia Jagina, kutokuweko kwake ndiko hasa kuwako kwake (2002:153).

### 3.4 SEHEMU YA TATU

Sehemu hii inaanzia sura ya ishirini na tatu ambayo ni ya mwisho katika riwaya ya Bina-Adamu! Baada ya P.P. kutoweka, Msafiri anasikia vicheko vya wale huntha anaowatafuta na ambao hawaoni ila kusikia sauti zao tu. Anapotaka kuwakimbiza babu anamkataza. Anamwambia kwamba ni kazi bure kuwakimbiza kwa sababu hawapo na hutokea katika matendo na fikra tu.

Huyu ni yule babu wa Zakongwe. Anamwambia Msafiri ni bure kuwafukuza huntha wasioonekana. Anamjulisha kwamba wamekwenda kila mahali alikopitia na kwinginekо wamezaa watoto na kuwaacha huko.

Bina-Adamu anapomwuliza ikiwa anayajua majina yao, babu anamwambia kwamba itabidi yeye na wenzake wawasake. Hata hivyo, babu anamjulisha kwamba baadhi ya wanaojulikana ni kama Mwanakabila, Binrangi, Mkengeushi na wengine wengi. Ni hawa ambao ni lazima waangamizwe ikiwa kijiji chao kitapata fanaka. Babu anamjulisha Jagina kwamba jamii inahitaji kuelimishwa upya kuanzia chini hadi juu, mtoto hadi mzee na watu wote kwa jumla.

Kwa kufanya hivyo, kila mtu atajua kwamba hakuna huntha waliosababisha matatizo yao bali ni jukumu lao, wenyewe kujitazama na kujirekebisha pale inapohitajika. Bina-Adamu anasikia sauti nyingine ikimwarifu kwamba wanahitajika kuungana kiuchumi, kisiasa na kijamii. Sauti hiyo inaendelea kumwambia kwamba umoja ni nguvu na wanaweza kumfunga yeyote yule wakishirikiana kama vile tusomavyo katika hadithi ya Gulliver (2002:154-155). Kwa kufuata

njia hii wataacha kuishi pembezoni mwa kijiji. Itabidi wawe nguli kupambana na hasidi wa kijiji ambaye ni Global villain, yaani mhalifu wa kijiji/dunia. Baada ya kuipitia riwaya ya Bina-Adamu! kwa kifupi, sasa tutatoa muhtasari wa riwaya ya Musaleo!

### 3.5.0 MUKHTASARI WA RIWAYA YA MUSALEO!

Riwaya hii inahusu hadithi ya mtu mmoja, Mugogo Wehu ambaye ni mhudumu wa Ombaomba. Huyu mhudumu anajiwa na hamu ya kufumbua kitendawili kisichoteguliwa. Hadithi hii inasimuliwa sambamba na nyingine inayosimuliwa na Mzee kiongozi wa nchi ambaye anapambana na wakati asiouelewa.

Hii ni riwaya iliyojaa tashtiti, ucheshi na ukweli unaokata maini. Kazi hii inaangazia matatizo yanayozikumba nchi changa za bara la Afrika. Hii riwaya ni mfuatano wa Bina-Adamu!. Inashughulikia masuala ya serikali dhalimu za bara la Afrika. Mwandishi anayajadilia masuala hayo kwa njia ya kejeli na dhihaka. Mwandishi ametumia elimu ya visasili kuelezea mianzo ya matukio mengi katika kazi yake. Wamitila, katika riwaya hii, ametabiri hali ya maafa makubwa yakayotokea siku ya kiama.

Mwandishi ameigawa kazi yake kwa sura ndogo ndogo kufikia arubaini na mbili. Sura ya kwanza hadi thelathini, mwandishi amezungumzia dhana za ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Ameangazia jitihada wenyeji wa Afrika walifanya ili kujikomboa kutoka minyororo ya mkoloni. Mkoloni alipofika katika bara lao alianza kuwaandalia makazi wenzao ambao baadaye walianza kufurika barani kama nzige. Mwanzoni wazungu walitumia mbinu mbalimbali ili kuwateka wenyeji, kama elimu ya kikasuku, dini na hata vishawishi kama vile nguo, peremende hata kuwahidi ulinzi dhidi ya maadui wao. Sehemu ya thelathini na moja hadi arubaini na mbili, mwandishi ameyamulika matokeo ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

Viongozi walioshika hatamu ya uongozi kutoka kwa Mzungu walianza kuwatesa na kuwadhulumu wenyeji wenzao. Waliaanza kujilimbikizia mali na basi wakawa makabaila na mabepari weusi.

Mwandishi vile vile ameangazia dhana ya utandaridhi na matokeo yake katika bara hili la Afrika. Masuala kama vile ya uchumi, siasa na kijamii yote yametandarishwa na hivi karibuni dunia yote itakuwa kijiji kimoja.

Jina Musaleo! lina maana ya Musa wa leo, yaani mkombozi wa leo atakayewakomboa wenyeji (Waafrika) kutoka dhuluma na mateso ya viongozi wao. Huyu Musaleo ana sifa nyingi mno: Yeye ni shujaa, kila kitu, akiondoka tutamlilia, mwenye uwezo, mkombozi na ana uwezo wa kuona kila kitu. Sifa hizi zote zinarejelea nchi ya Marekani ambayo imebaki ikiwa askari wa Ulimwengu mzima baada ya kuanguka kwa Urusi ya zamani. Marekani sasa ndiyo inaamuru kila kitu Ulimwenguni kote. Wamezua mbinu mpya ambazo wanazitetea kuwa ni za kuleta maendeleo bila kukadiria madhara yazo kwa wanaohusika. Katika riwaya hii mambo yote yamejadiliwa kwa kejeli ili kusuta hali halisi iliyomo katika jamii. Matukio ya kiajabu ajabu, yanayoambatana na ndoto na uhalisia, yameshugulikiwa sana katika kazi hii. Kuna uduara wa wakati na kuvunjwa kwa mipaka ya mahali, maeneo na hata bara. Mwandishi anaonyesha kuwa watu wametandaridhika na kwa hiyo hawana haja ya kupanwa na mipaka. Hali kadhalika kuna visasili vinavyoelezea chimbuko la masuala mengi katika jamii. Mwishoni mwa riwaya, Mzee anapendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya matatizo yanayozikumba nchi za Ulimwengu wa tatu. Anapendekeza kwa kusema kwa sauti moja na kuungana ni njia mojawapo ya kujikomboa na kujijua hasa.

### 3.5.1 SEHEMU YA KWANZA (SARA YA 1-19.

Hadithi inaanza pale ambapo upepo mkali unapiga kwa nguvu za ajabu na kuangusha matawi ya mti yaliyokwaruza paa moja na kutoa sauti ya kuchukiza masikio. Kulikuwako na mgunga mkubwa uliokuwa ukiyaangusha majani yaliyopukutwa na upepo.

Mgunga ni mti uotao porini wenye miba miba, ambao ni chakula cha tembo. Chini ya mti huo palikuwa na watoto wengi waliokuwa wanajifunza kuvuta bangi huku wakicheza kwa msisimko mkubwa. Huu mchezo ulifuatwa na vicheko vilivyojaa nguvu na matumaini. Hapa mwandishi anatuonyesha kuwa kizazi kipya ndicho kitacholeta mabadiliko ya kweli katika jamii.

Mzee amechanganyikiwa pamoja na Mugogo Wehu ambaye ni nusu mwendawazimu.

Wakati kizazi hiki kipya kinapojaribu kuleta mabadiliko na maendeleo, kinashtuliwa na mlipuko wa bunduki (2004:1). Kwa sababu ya kutokuwa na usalama na amani katika nchi zao, watoto hawa wanatawanyika kundi moja huku lingine kule. Mazingira ya aina hii hurudisha maendeleo nyuma.

Katika sura ya pili Kingunge ana hamu ya kuandika riwaya mahsusi itakayosomwa na kusaidia usomaji wake. Riwaya yenyewe ni Musaleo! Musaleo! ni ufupisho wa maneno haya matatu Musa wa leo, yaani mkombozi wa leo. Musa wa zamani alikuwa Musa ule wa Biblia, aliyewaokoa wana Waisraeli kutoka Misri na kuwapeleka katika nchi ya ahadi na mane mane. Musa wa leo anatarajiwa kuwakomboa watu kutoka mateso na dhuluma wanazotendewa na viongozi wao wadhalimu. Mwandishi anahofia kuwa hata kama riwaya ya Musaleo! Itaandikwa, haitapata wasomi kwani watu siku hizi hawana haja ya kusoma. Watu wengi sana wametamaushwa na masomo. Kuhusu suala la ufisadi, Mzee anajiuliza maswali mengi kama vile nani asiyeiba nchi hii, nani anaweza kuaminiwa kwa kusema ukweli? Mzee mwenyewe anakuwa jibu kwa maswali haya, anadai kuwa yeye ndiye anayenena ukweli na anafaa kuaminika.

Suala lingine linalojitokeza katika sura hii ni lile la njaa. Njaa ilimfanya mwandishi ahame kwao. Hata aliporudi bado njaa ilikuwepo, kwa hiyo hatua aliyochukua ya kutoka kwao kwa sababu ya njaa siyo mwafaka. Angejaribu kukabiliana na janga lenyewe akiwa kwao.

Mara nyingi historia hutukumbusha mambo mengi. Hatuwezi kusahau historia yetu kwa sababu jana yetu ina la kusema leo na leo ina la kusema kesho. Kila kitu kina historia yake.!

Mwandishi alipoondoka kijijini alikuwa haujui umri wake wala umbo lake. Jambo analokumbuka fika ni kuwa watu wamwita "kizee." Alizaliwa akiwa na sifa za kishujaa kama vile kuzaliwa mapacha, yeye na dada yake, alitoka tumboni amekunjia mbegu za kuwangia kiganjani.

Siku chache baadaye waliamka watu na kukuta mengine nje, akaitwa **Fumbia Kiganjani.** Meno yake yaliotea tumboni, alizaliwa kigego na kichwa kinene ajabu, masikio makubwa na uwezo wa kunusa kila kitu. Ukame ulichukua nafasi ya njaa. Mzee aliporudi alirudi na chembe chembe za nafaka. Alijifunza uganga na aliweza kujaza gunia kwa kufanya chembe kadha mazingaombwe.

Dunia ya wajanja hii! Mzee alikaribishwa na wenyeji na kitendo cha kurudi ni cha uzalendo, kwani mwacha mila ni mtumwa. Mzee aliwahakikishia kuwa ilikuwa lazima arudi kwa kuwa alikuwa ameacha kondo yake nyuma.

Wakati mzee aliporudi, alikuta kijiji kimeongezeka kwani watu walikwa wamezaana kama walivyoamrishwa na mzazi wao wa kwanza: **YUNGA MWAMBA**..Kijiji hakikuwa kijiji tena bali nchi, labda hata bara! Hali hii inaweza kulinganishwa na enzi ya ukoloni. Mkoloni alipoondoka, nchi nyingi za Afrika zilijipatia uhuru wa bendera. Viongozi wao walishindwa kudhibiti nchi hizi changa, na kushindwa kujiamulia masuala yao ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Basi viongozi hawa wakawa wabaya zaidi kuliko Wakoloni wenyewe na kwa hivyo wakaanza kuendeleza ukoloni mamboleo.

Mzungu alipoona kuwa Mwafrika ameshindwa kujimudu kisiasa, uchumi na kijamii, ilimbidi arudi na mbinu ya ujanja mpya na mara hii alikaribishwa na wenyeji. Baadhi ya mbinu mpya mzungu alikuja nazo: utandaridhi, misaada, kubinafsishwa kwa mashirika ya serikali na kutoa mikopo kwa mataifa machanga.

Mashirika yanayotoa mikopo hiyo ni mefu (IMF) na *World Bank*. Vishawishi hivyo vimevutia sana mataifa yanayokua na kwa hivyo kulazimishwa kuwakaribisha.

Jambo kuu linalojitokeza katika sura ya tatu, ni lile la amani na usalama. Wananchi wanapolalamika kuwa hakuna usalama na amani katika nchi yao, viongozi wanajibu kwa kusema kuwa labda wanaota, pengine ughaibuni, nchi za mbali ndiko kunaweza kuwa na uchafuzi huo.

Askari hutumika kuwanyamazisha wale wanaopinga mfumo na sera za serikali. Askari huua bila kufikiria bora ameamrishwa. Jambo hili latufanya tusione mpaka kati ya ndoto na ukweli katika nchi zetu. Kingunge aliendelea kuandika riwaya yake katika sura ya nne. Yeye hakufungwa na mipaka katika uandishi wake. Anaona uhalisia na ndoto kuwa sawa. Aliyakubali mabadiliko na akawaona wale wanaopingana nayo wacha wabakie na fikira zao kongwe na zilizopitwa na wakati.

Hatua ya kwanza yeye alikubali jina lake mpya, yaani Mzee! (uk.4). Yeye ametandaridhika na kwa hivyo hana budi kuyakubali mabadiliko yanapofika. Mzee, hakuzaliwa, alitokana na kupasuka kwa mgumo mkubwa wa kijiji. Lugha alikuwa nayo, alichofanya ni kulainisha msamiati tu. Siku alipotoka mtini, mvua kubwa ilinyesha ajabu. Miti ilianguka na hata jua kukaribia kupatwa. Jina la baba yake lilibadilishwa na kuwa Mjukuu hasa wa Yunga Mwamba. Alikuwa mzazi wa kabila fulani la Wachonga vinyago. Alikuwa mwanamume. Inasemekana aliishi kule juu milimani alikokuwa akijitambulisha na magoma yake makubwa ajabu. Uzeeni alikuwa mkiwa na kuamua kuzaa watoto aliowaamuru nao wazaane.

Mzee alitungiwa tenzi za wasifu wengine wakaghani sifo, wachache ngoma wakamgeuza kipokeo. Basi Mzee akapata sifa nyingine *Mzee Mvumbua Usomi.* Wenyeji walianza kuwa waoga wakawa hata kusema jambo dhahiri ni vigumu. Msimulizi anajipa matumaini licha ya matatizo yaliyomo. Igizo la *Eugene Ionescu la Rhinocerous* ambako watu wanageuka vifaru, linaonyesha uwezo mkubwa viongozi walionao wa kuweza kujibadilisha nafsi zao na zenye uwezo mkubwa.

Kingunge alikuwa kiongozi anayetokana na kizazi cha Yunga mwenye uwezo hata wa kuathiri majira ya ukame na mvua (uk.7). Tangu alipotokeza hali ya hewa ilikuwa nzuri, mavuno yakawa mazuri ajabu, kwa hivyo akawa Mzee Mleta mvua. Mzee anatushauri kuwa kila mmoja azichunguze nyendo za mwenzake, kulipima na kulipiga darubini kila neno.

Mzee anaendelea kusema kuhusu kazi yake: "ukinisoma tua na kuwaza. Ukitaka unaweza hata kunipindua nilivyowashauri washairi na marafiki zangu. Mara nyingine utalazimika kurudi ulikosoma." Mzee anasema kuwa hakuna shughuli ambayo inaweza kuchukuliwa bila idhini yake, yaani idhini ya kila kitu ilikuwa yake. Mzee pia alichukua hatua muhimu ya kupenya katika kila upembe na kuhakikisha anatambuliwa na kila mtu. Aliamua kuyatembelea maeneo mbalimbali katika nchi nzima. Hii ilikuwa hatua muhimu ya kuuweka msingi wa woga. Mahali alipozuru ilikuwa, Mzee, anakuja! Mzee yu njiani" "sasa hivi anafika!" (uk.8).

Hadithi hii ya Mzee inaisuta hali halisi iliyomo katika nchi zetu, Kenya na bara nzima. Viongozi hupenda kutembelea maeneo mbalimbali nchini mwake kwa kudai kuwa wanakagua miradi ya maendeleo ilhali wanataka kuwanyamazisha maadui wake wa kisiasa. Wanapofanya hivyo, umaarufu wao unaimarika miongoni mwa raia wake.

Ili kufanikisha hofu miongoni mwa watu, ilibidi ajihusishe na asasi nyingine. Alijua kuwa nguzo moja haisimiki jengo. Asasi hiyo ni utamaduni. Hii ni asasi ya raha. Profesa aliona kuwa nzuri ya kuhakikisha kuwa umejizikia katika bongo zao ni kujitosa kwenye kiwiliwili cha utamaduni na kukwamia hapo kama ruba!

Hali hii imefanana wakati mkoloni alipofika barani Afrika alizua mbinu nyingi za kuweza kutawala wenyeji. Alitumia dini, misaada, propaganda na ahadi nyingi za kuvutia ili kuweza kutawala. Mkoloni aliposhika mizizi alijiona kama mkombozi ambaye amekuja kuikomboa jamii kutokana na pingu za maisha. Kwa hivyo, aliamua kuja kwa uganga wa kugeuza chembe chembe, alidai kuwa alikuwa na uwezo wa kukomba, basi tangu wakati huo akawa pia: Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mara tatu!

Katika utabiri, mkombozi wa jamii alipaswa kuzaliwa katika mazingira ya ajabu. Alitakiwa kuwa na uwezo m'kubwa! Mwendo wake haukuwa wa kawaida. Sifa hizi zote Mzee alikuwa nazo.

Msimulizi anatufahamisha kuwa jina la riwaya yake ni "Mzee." Hadithi ya riwaya hii inahusu Mzee, yaani kisa cha Ukolonge na Musaleo!, (ukoloni mkongwe na ukombozi wake). Zamda, mkewe wa Mzee, alishangaa na maadiliko aliyoyaonyesha mumewe kwa miaka inayokaribia kumi na tano. Ni kama ameingiwa na wazimu. Ili kulinda utawala wake, Mzee alijiundia kikosi cha vijana. Kikosi hicho ni "vijana wa Mzee." Licha ya umri wao waliridhika na uamuzi wake. Jambo la ajabu ni vipi kuitwa vijana na mtu anayejua maana ya kila neno? Si ajabu neno hili likawa na maana tofauti na ile tunayoijua. Hawa walikuwa walinda usalama wa Mzee. Wote hawa waliapa kuwa watakuwa tayari hata kumfia.

Ili aweze kuendeleza ukoo wa baba yake Yunga Mwamba, wazee walimshauri aoe. Mzee hakuwa na wazo hilo lakini akawakumbusha kisa cha babu yake aliyejifungua watoto alipokuwa uzeeni bila ya kuoa.

Utafiti unahitajika kufanywa kuhusu tatizo la watoto wa mitaani. Mwandishi analiona kuwa janga !ubwa ambalo lahitaji kutolewa suluhu. Kitungule alimtambulisha msimulizi kwa kundi lau jamaa waliokuv a wanahitaji mtafiti wa kushirikishwa katika utafiti wa vijana waliokosa makao mijini.

Kisa cha Ukolongwe kinajadiliwa katika sura ya 12-14. Tunaona kwamba Mzee hakulipenda jina hilo na hamna aliyeelekea kuijua maana ya jina kama hilo. Lakini alijua, hata hivyo, jina lenyewe lazima lilikuwa na maana, kwani majina yetu yote yana maana. Mzee alikutana na wazee wakongwe, waliochongwa na ala za maisha ya dhiki. Hawa ni wakongwe walioifanyia nchi hii kazi kubwa! Ni wapiganiaji wa uhuru, *War vetarans*. Wazee hawa waliahidiwa mengi kama mashamba, nishani pamoja na kujengewa minara katika uwanja wa uhuru na majina yao kuigizwa katika orodha ya waandika historia lakini bado wanasubiri. Mzee anawalaumu waliotangulia kwa kutotambua nafasi ya wazee muhimu kama hawa. Tunapoichunguza historia ya Ukolongwe, tunaona kuwa jamii ya Mzee iliamini katika kuzaliwa kuwili. Kufariki kwa mtu na kujitokeza kupitia kwa jamaa yake.

Mkoloni anaporejea kwa mara ya pili, anakuta hali mbaya ya masuala mengi barani Afrika. Barabara ya kuelekea sehemu ya 'Government Quarters' ilikuwa na mashimo mengi ajabu. Enzi ya wakoloni, barabara hizi zilikuwa za kuvutia sana lakini siku hizi zimezorota. Watu wengi wamehamia mijini kutoka mashambani, hali ambayo imeathiri huduma nyingi za miji. Wakazi wa mijini wanahimizwa mara nyingi warudi mashambani kutarazaki.

Katika sehemu hii pia tunampata mhusika mmoja, Ngwena. Alikuwa mwalimu na mtaalamu wa historia ambaye alisifiwa kwa kipaji chake cha kuchunguza historia na utaratibu wake wa kuyaandika matokeo ya utafiti wake. Ngwena alifanya kazi katika chuo kikuu cha pekee nchini kisha akaachishwa kazi kwa madai kuwa kapoteza makaratasi ya mitihani ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kitaifa.

Kisha baada ya kutoka chuoni, aliamua kuanzisha matbaa yake ya kibinafsi na kuendeleza utafiti wake katika maakabu kuu. Ngwena pia alifanya utafiti kuhusiana na historia ya nchi hii kuanzia ukoloni hadi hivi leo. Baadaye alienda uhamishoni, nchi nyingine.

Kisa cha Ukolongwe kilianza mmano mwaka 1884 katika mji wa Berlin, Ujerumani (uk.20). Kisa hiki kinasimulia jinsi ukoloni ulianza. Mataifa ya Afrika yaligawanywa miongoni mwa

madola kama vile Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, Ureno miongoni mwa zingine. Kuna wenyeji waliowakataa na wengine kuwakaribisha.

Wazungu walipofika Afrika kwa mara ya kwanza, hawakuonyesha heshima hasa kwa wenyeji. Lakini Waafrika kwa ukarimu wao waliwakaribisha na kuwapa mahali pa kujenga pamoja na jamaa zao. Walipiga marufuku biashara iliyotegemea kubadilishana kwa bidhaa. Badala yake sarafu za pesa zilianza kutumika. Kuja kwa watu weupe, anavyodai Wamitila, ni mwanzo wa dhiki kubwa iliyowafanya wazee waanze kuimba nyimbo za kujikomboa katika ngoma na sherehe zao.Katika sura ya 15-19, mwandishi anaichora dunia kama mahali pabaya pa kuishi kwa sababu kuna mambo mengi ambayo hayaleweki. Kwa maoni yangu, matatizo anayoyapitia binadamu ni matayarisho ya mambo makuu yajayo.

Kwa mfano, tutapata maendeleo, uhuru wa kusema na kutembelea maeneo mbalimbali bila kuwekewa vikwazao. Hakuna jambo lisilo kuwa na mwisho. Matatizo mabimbali yanawakumba wenyeji. Kwa mfano, ukosefu wa taa, umeme, na kuzuka kwa ukame. Msimulizi anasema kuwa hatuna uwezo wa kupata umeme wa kutosha kama zamani. Hata ugavi, (ugawaji) wa umeme "*Rationing*" unafanywa kwa mapendeleo ya kimaeneo na kitabaka. Ugari *(rationing)* unafanywa kwa kukata umeme katika maeneo fulani asubuhi, adhuhuri mengine, na jioni mengine vile vile. Kuna uwezekano kuwa kuna mengine yaliyokosa umeme muda huo wote.

Kwa maneno ya wakurugenzi, kila eneo lilipaswa kuonja uhalisi huu. Kulikuwa na maeneo mengine watu hawakukosa umeme kabisa. Kwa mfano, walioishi maeneo ya kitajiri na wenye nasaba, hawakukosa umeme hata siku moja, si mchana si usiku (uk.21).

Tatizo lingine ni watoto wa mitaani. Watoto hawa maisha yao yanaendelea kuwa mabaya kila kuchapo. Wanavuta bangi na kunusa gundi na hakuna mtu anayewajali. Mwandishi anatuonyesha kuwa hamna haki na usalama katika jamii.

Mahali ambako tunastahili kupata usalama na ulinzi, kama vile vituo vya polisi, watu wanazomewa na kutusiwa kwa kila aina ya maneno (uk.22). Swali tunalojiuliza ni kwa nini basi askari wanajiita walinda usalama, walinda watu na wanalipiwa nini?

Kuhusu dini, mwandishi anasema kuwa watu wengi wameacha kuhudhuria hekalu. Hekalu ni mahali pa kufanyia toba, mahali kuna amani na upendo. Lakini imekuwa nadra sana kuwaona watu wakiingia makanisa, watu hasa! Wale wanaoingia ni wanafiki tu, wanaodai sadaka kutoka kwa waumini na kuwahidi miujiza ya urongo. Wafanyabiashara wa kiAsia wenye uhusiano wa karibu sana na wanasiasa nchini wamekuwa maarufu.

Vile vile mwandishi anaonyesha kuwa ukweli hauna maana siku hizi. Anauliza (uk.25): "kwa nini ukweli hauna maana nchi hii siku hizi?" Wanasiasa wamekuwa wezi, wachapishaji wezi, na kila mtu.

Mwandishi anaona kuwa ukweli siku hizi hauna maana katika nchi yake, kwa sababu watu wanaotunukiwa majukumu makubwa katika jamii, kama vile viongozi, wanasiasa, watu wa kawaida, wafanyakazi, wote ni wezi! Tunaona kuwa jambo hili limewavunja moyo raia na kuathiri hamu ya kufanya kazi. Wote wametamauka katika kutekeleza wajibu wao. Kwa jumla Wamitila anajaribu kukejeli uhalisia uliyomo katika jamii yetu.

Anamulika maozo yaliyomo kama vile ufisadi wa kila aina katika kila sekta, usalama, watoto wanaorandaranda mitaani ambao huwavamia watu. Tatizo hili la watoto mitaani latokea kila mahali ulimwenguni. Mji wa Rio de Jenairo, nchini Brazil ni mfano mzuri. Hali hii ni sawa hasa kwa mataifa yanayoendelea.

Ukoloni uliendelea kukua na kushika mizizi. Mkoloni aliyapenda mazingira mapya (Afrika). Alianza kufanya mabadiliko ya kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Hali hii iliwafanya wenyeji kuanza kulalamika kuhusu vitendo vya mkoloni. Wenyeji walianza kuzua mbinu za kukabiliana na mkoloni. Walitunga nyimbo za kumkebehi mkoloni. Lakini mkoloni mjanja naye, alikuwa na mbinu zake.

Kwa mfano, kila aliloshindwa kulijua aliamuru lipigwe marufuku. Alisisitiza kuwa lazima watoto waliokuwa wakizaliwa wakati huo wafundishwe nyimbo mpya. Aliteka nyara lugha na kubadilisha maana ya maneno:

> "Kuna wengine wanaosema kuwa alikuwa na tatizo la masikio, kwa hiyo kila aliposikia neno **"UHURU"** akilini lilisikika kama **"KUFURU."** Neno **"UZALENDO"** ndo likawa kitu kama **"UVUNDO.** " (uk.26).

Hali kadhalika uwezo wa mkoloni ulimfanya kutamka maneno yaliyowashangaza wengi. Kwa mfano, katika (uk 26) anasema:

> "Sasa – kuanzia leo, na wala si kuanzia leo ni tangu zama na azali, kuna **MIMI** na **WENGINE** tu.

Anaendelea kusema kuwa "mimi ndimi msingi wa kila kitu. Mimi si kama nyie!" Mkoloni alishikilia kuwa kauli zake zilikuwa misingi imara na Sayansi.

Inasemekana siku moja alijitokeza hadharani huku amekishika kitabu kimoja kiitwacho "*The Wild Man's* pedigree" yaani asili ya vizazi vyote. Humo aliwasomea watu sehemu fulani aliyodai kuwa alizieleza sifa za watu weusi kama: ". . . wasiochangamka, watulivu, wenye pua pana, wajanja, wazembe na wanatawaliwa na ugeugeu!" ( uk. 27).

Ajabu ni kwamba mwenyewe alikuwa na sifa hizo hizo za kubadilikabadilika kama kinyonga. Suala lingine ni lile la ardhi au mashamba. Mkoloni alipofika barani Afrika, alianza kuwatafutia wenzake ardhi ya kulima. Wakoloni walitumia ujanja wao wa kuchukua ardhi yote iliyokuwa na rutuba. Waliichukua na kuwakabidhi jamaa zao. Wenyeji waliokuwa na tabia ya kuhamahama walilazimika kuishi pahali pamoja tu hasa sehemu kame na kavu.

Ardhi ambayo wenyeji hawakuwa wanaitumia kutokana na mfumo wao, ilichukuliwa na mkoloni na jamaa zake na kubatizwa **"Ardhi haribifu."**

Waafrika, walichukuliwa na kupewa kazi ya vibarua katika mashamba haya. Mzungu aliamua kuwafanya watu kadhaa aliowajua kwanza alipofika Wakuu, akawaita "*Paramount chiefs.*" Huu ukawa mwanzo wa uchifu na uchafu na udufu wake!

Mkoloni aliwahimiza machifu wapendekeze watu wa kufanya kazi katika mashamba makubwa ya wazungu. Wazungu waliona kwa njia hii watapunguza uzembe wa wenyeji, kwa sababu watakuwa na kazi ya kufanya badala ya kujizungukia majiani tu!

Wafanyakazi wenyeji waliruhusiwa kukaa kwenye mashamba ya jamaa za wazungu ili kuweza kufanya kazi vyema. Baada ya wazungu wajanja kufanikiwa kumiliki ardhi ya wenyeji, hatua ya pili iliyobakia ni kuviiba na kuvimiliki viungo vya wenyeji.

Mwandishi pia amemulika hali ya ukengeushi. Waafrika walianza kuiga na kutenda tabia za Kizungu. Kila mtu akawa anavalia masuti na kubeba mikoba ambayo ina magazeti ya zamani!. Uzungu ukaanza kuvaa wenyeji, watu, nawe wazungue na kuwazungua kwa uzungu wao wenyewe!

Wazungu walitumia makachero kuweza kusikiliza maongezi ya watu, hasa wale waliokashifu mifumo yao. Hali hii iliwafanya wenyeji kuogopana kutokana na hofu iliyojengwa na mazingira ya aina hiyo. Makachero hawa waliwekwa kila mahali hata vyuoni. Beberu alizidi kuwa mjanja. Kadiri siku zilivyosonga ndivyo alivyoendelea kuwa na kiburi na kuwa mjuzi wa kila kitu. Aliamuru wanyama waliokuwa wakifugwa na wenyeji wapunguzwe kwa sababu ya uharibifu wa mazingira. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa uchukivu dhidi ya mzungu. Ujitambuaji wa wenyeji ulishika nguvu kwanzia wakati huo. Mbeberu alibadilisha mambo ya kimsingi aliyoyakuta siku hizo. Ni wazi kwamba kabla ya mkoloni kuingia katika bara letu, wenyeji hawakuwa na mipaka ya taifa lao, kila mtu alijiona nyumbani akiwa popote pale. Mzungu alifanya hivi kama njia ya kuhakikisha kuwa aliwamiliki watu wenyewe.

Lugha nayo kama chombo cha mawasiliano haikuwachwa nyuma.

Ili kuvimiliki viungo vya wenyeji, mzungu aliwapendekezea njia mpya za kutafutia elimu na maarifa juu ya mambo mageni. Watu walisusia kwa kusema walikuwa na njia zao za jadi zilizowafaa kwa miaka na dahari. Baadhi yazo ni kama: Jando, unyago, miviga na ngomezi. Mbinu hiyo ilipingwa vikali na wazee wenyeji. Ususiaji huu uliwabidi wazungu kutafuta njia nyingine ya kuvutia. Wazee hawa hawakuwa na hamu ya mambo mageni tena, kwani umri wao ulikuwa unaelekea machweo. Basi wazungu waliamua kuwatuma watoto wao kwenye vituo vya kuelimisha mambo mageni, yaani mashule. Kwenye shule walimu wazungu waliwasimulia vijana hawa visa na hadithi mbalimbali. Dhamira yake ilikuwa ni kuwaingiza katika ustaaarabu mpya na uliodaiwa kuwa bora. Vijana hawa walifunzwa visa na hadithi nyingi, kama vile: *Sinbad the sailor, Ali Baba and the forty thieves, King solomon Mines, Treasure Island* na *Robinson Crusoe* (uk. 31).

Hadithi na visa hivi vilikuwa na athari kubwa kwa vijana hawa. Jinsi walivyoendelea kuvikariri visa hivi ndivyo walivyoanza kuvisusia visa walivyotambiwa na wazee na mababu zao, kama vile ngano za fasihi simulizi.

Jamii ya kizungu ilishikilia kuwa mafunzo hayo yalikuwa hatua muhimu na baadhi ya wenyeji wakaishia hata kuyakubali. Ushindi huu ulimfanya mkoloni kufurahia sana.

Mwandishi anaendelea kumulika maovu yanayotukumba katika jamii. Anatumia mfano wa filamu *"Her Alibi."* Kuonyesha hali halisi iliyomo katika jamii. Filamu hii inahusu nchi ya Romania enzi ya Nicolae Caesecu ambako nusu ya raia wa nchi hiyo inachunguza matendo ya nusu nyingine. Hakuna mtu anayemwamini mwingine.

Tatizo lingine katika miji mkubwa ni utaratibu mzuri wa kuendesha magari. Magari yameendeshwa kwa kasi mno. Madereva hawazingatii ishara za barabara na sheria za trafiki.

Hii ndio sababu iliyomfanya msimulizi kulazimika kuangalia huku na huku kuhakikisha hapakuwa na gari ndio aweze kuvuka barabara.

Mwandishi anakejeli tatizo la ufisadi kwa kutumia istiari ya kipofu. Nchi inapopewa msaada kutoka kwa wafadhili kama vile Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia, kuna watu wafisadi wanaopora nchi hela hizo zote kama vile kipofu yule anayeibiwa pesa zake kutoka ule mkebe.

Kuhusu suala la watoto mitaani, Wamitila anawalaumu wale watu wanaozaa watoto na kuwatupa kuwa machokora mijini. Vile vile katika sehemu hii tuna uduara wa wakati. Msimulizi alienda safari ya matope, wakati wa mvua. Hii iliuwa safari ya kujitafuta. Msimulizi anatembea kwa muda mrefu ambao hawezi kuujua kama ilikuwa siku nzima, mwongo mmoja au miaka kadha. Anachokumbuka ni kuwa njia aliyoitumia ilikuwa moja tu.

Hakuwa na wasiwasi ya kupotea njia. Hiyo njia iliishia kuungana na nyingine kwenye sehemu iliyokuwa wazi. Safari yote ilikuwa ya kuteremka chini tu, hapakuwa na mipando wala miinuko. Kadiri tunavyotafuta ukweli ndivyo njia pana tuliyoitumia ilivyoanza kuwa nyembamba. Kwani kunatokea vizuizi vingi, majaribu na matatizo. Hapa tunaona ukweli haupatikani kwa urahisi. Upepo wa bahari unaashiria uchafuzi na matatizo yaliliyomo katika safari ya kutegua kitendawili cha ukweli. Giza kuu ajabu linaashiria kuchanganyikiwa kwa msakaji.

Sauti ya bundi (uk. 35) inampa bahati njema msimulizi. Katika nchi yao, sauti ya bundi inaashiria bahati mbaya. Hapa msimulizi amevunja mipaka ya tamaduni. Maeneo mengine sauti hiyo inaashiria dua njema kama vile Ulaya.

### 3.5.3 SEHEMU YA PILI (SURA 20-30)

Jamaa ya wazungu iliongezeka kupindukia, baada ya viongozi wao kuwaandalia makao. Wahindi pia hawakuachwa nyuma. Walianza kuzuru barani Afrika. Walivutwa sehemu hizi na uwezekano wa kuja kufanya biashara na matumaini ya kuyapata maisha mazuri. Walitarajia kupata ulinzi wa ufalme na kulindwa na himaya ya Waingereza hapa nchini Kenya na kwingineko barani Afrika.

Wazungu waliwaruhusu na kuwakaribisha Wahindi. Walipewa makazi nao pia wakawaalika jamaa zao, ambao walikuja kwa wingi. Walipofika barani walianzisha biashara ndogo ndogo, basi wakaitwa ***dukawallah***. Biashara zao zilipanuka na hata wakajipatia hela za kununulia ardhi na kujijengea makao yao.

Mzungu alipoona kitendo hiki, aliharamisha ununuzi huo. Ununuzi wote wa ardhi kati ya watu tofauti haukuruhusiwa. Wahindi walikasirishwa sana na uamuzi huo. Wale waliokuwa na wafanyikazi wa kiafrika, waliamua 'kutupa' hasira yao kwao. Wengine walianzisha kijarida kilichojulikana kama ***'Tangazo.'*** Humu walianza kupaaza sauti zao kulalamika kuhusu usaliti wa himaya. Waafrika wenyeji nao hawakuachwa nyuma. Walikuwa na hasira ajabu. Wakaanza kujiuliza maswali mengi. Mkoloni alivamia nchi yao kisha akawaalika jamaa zake kama fisi wanaochangamkia mzoga. Akawaita na hata na Wahindi. Walilalamika na kujiuliza kwa nini waishie kushika mkia kwao? Damu ya hasira ilianza kuwatembea mishipani kwa kasi ya ajabu. Mkoloni alikithiri kiburi tu. Siku moja aliposikia tetezi za wenyeji aliangua kicheko kilichosikika majimboni. Inasemekana kuwa siku iliyofuatia alielekea sehemu iliyokuwa na mkuyu mnene ulioota kijiji. Aliamwamuru jamaa mmoja wake auchongechonge vizuri kisha asimike kitambaa huko juu. Hiyo ikawa bendera ya ufalme! Hiyo ikawa ishara ya uwezo wa himaya yao juu ya kila kitu. Mzungu alisema haya huku akijigamba. Kwa upande mwingine, wenyeji wakaja juu na kuteta. Mti wa mkuyu ni uhai wao. Inawezekanaje mzungu akate uhai wao? Walimwambia hawezi kuing'oa mizizi ya kuwako kwao! Ukolongwe akasema kwa sauti "kata..a!" "Sasa unavuka mipaka; huu ndio mwanzo wa mwisho!" Ukolongwe akaguta "Kataa! Kataa! Kataa!" Watu nao wakakataa. Hayo yalikuwa magharibi ya jua jingine (uk.38).

Tunapopiga darubini, tunaona kuwa wajinga wakubwa ni wale watu wanaopenda kuamini vitu ambavyo hawakuwa hakika navyo. Ujinga wao unawafaidi wengine. Wajinga ndio waliouwa!

Mzee alimwonyesha yule jagina kuwa njia ya ukweli siku zote ni ngumu. Kumejaa vicheko, dhihaka katika sura hii. Jagina anamfahamu Mzee.

Kumbe ana watoto kila mahali. Zipo mimba chungu nzima zinazotunzwa na zoote ni zake! Mzee alikuwa ni mjukuu wa Yunga Mwamba. Hana kaka wala dada. Huyu ndiye kiongozi aliyechaguliwa na Mungu mwenyewe.

Katika (uk.41), mwandishi amelijadili suala la usasa na usasa leo. Watu hawapendi mabadiliko, bali huyapenda mazoea na ukale. Na hilo ndilo kosa kubwa. Maendeleo hayamo katika ukale. Uhalisi wa siku hizi umevunjikavunjika hauna pa kujishikilia; hauna mshikamano imara. Lazima tudadisi kila kitu: Siasa, uchumi, mapenzi hata miundo ya hadithi pamoja na hata lugha yenyewe!

Meli ilikuwa ishara kuu nchini kuwekwa picha ya Rais wa nchi kwenye fremu zilizofanana na meli. Hii ilikuwa njia nzuri ya kumtambulisha Mzee kama nahodha wa meli ya taifa. Jagina aliendelea kuongozwa na yule ndege, bundi. Ile hofu yake aliyokuwa nayo hapo awali kuhusu hawa ndege ilianza kumwondokea. Jagina alishangaa "hivi huku ni wapi ambako watu wanaongozwa na ndege wa ajabu kama hawa?" (uk. 44).

Jagina alipita kwenye sehumu iliyokuwa na giza ajabu. Alitembea kwa muda mrefu katika hali hii hadi aliposhtukia ameingia kwenye sehemu iliyokuwa na maji maji na matope mengi. Aliivuta miguu yake kwa taabu kama wafyatua matofali. Alikumbuka maneno ya mwisho ya yule Mzee "Shika njia na kumbuka njia ya ukweli siku zote ni ngumu."( uk.44).

Alipoanza kutamauka, alisikia sauti fulani akilini mwake ya kumhimiza, "Usife moyo. Jikaze kumbuka ahadi uliyotoa kwa yule kijana!"

Mashamba ya mawe yanaashiria maisha ya kudumu. Hapa kinacholimwa ni uhai! Haya ni mashamba ya uhai . Unajua uhai ni kama haya mawe, unadumu (uk. 47).

Mwandishi anatusimulia kisa cha Mamanchi. Jagina anaongozwa na huyu Mamanchi badala ya yule ndege, bundi. Mamanchi alikuwa dada yake Mzee ambaye aliaminika kuwa hakuwa na ndugu hata mmoja. Mamanchi alimwongoza Jagina kupitia karibu na sehemu iliyokuwa na kaburi wazi. Kutoka kaburini kulitokea maneno haya:

> "Mzee! Mtukufu Mzee! Kiongozi, Mwalimu namba moja, mganga, msomi Wahedi Mleta mvua. Musa wa leo! Wewe ni kila kitu. Kama si wewe, nisingekuwa" (2004:48).

Jambo la kushangaza ni kwamba inawezekanaje maneno kutoka kaburini? Mwandishi anakejeli hali halisi iliyomo katika jamii ya Kenya. Hali hii inafananishwa na ile ya enzi ya chama cha KANU, ambako wanachama sugu waliweza kukariri kikasuku manifesto ya chama chao. Waliweza kumpa kiongozi wao majina mengi ya sifa kama vile Mzee, mtukufu Rais, mkulima namba moja, Profesa wa siasa, n.k.

Katika sehemu hii mwandishi ameeleza kifo kama hatima ya maisha. Hata hivyo anasema kuna wengi ambao tayari wamekufa ingawa wana uhai. (uk.49). Maisha mjini ni ya kutafuta riziki. Kwa mfano, watu wengi walijitokeza majira ya jioni wakati bidhaa zao zilipohitajika na watu waliokuwa wakitoka kazini kukimbilia mitaani.

Wakati kama huu, askari wa Halmashauri ya Jiji, walipambana nao mchana-wangekuwa wameondoka na kuwapa fursa ya kuzitandaza bidhaa zao kila mahali penuni mwa maduka na kando ya barabara.

Katika jumba la makumbusho au makavazi, palijaa tungo za wasifu wa kiongozi wa nchi na tafsiri za hadithi nyingi za kizamani kutoka Ulaya, visasili vya Uyunani na mashairi ya *Ki-urdu*. Palikuwa pia na matoleo mbalimbali na nakala ya tafsiri ya Biblia. Lakini ajabu ya ajabu; hapakuwa na kitabu hata kimoja cha Historia.

Mkoloni alipoona wenyeji wanakazania kumgomea, aliamua kutumia nguvu. Inasemekana kuwa alipitisha amri fulani zilizowakataza watu kwenda huku na huku. Pili, alikuwa na jamaa aliowapaka mafuta kwa mgongo wa chupa wakaishia kuamini kuwa alikuwa rafiki yao wa kufa kuzikana. Hawa ndio waliompenyezea na kumfichulia ni akina nani waliokuwa wakiwachochea wenzi wao.

> "Mzee! Mtukufu Mzee! Kiongozi, Mwalimu namba moja, mganga, msomi Wahedi Mleta mvua. Musa wa leo! Wewe ni kila kitu. Kama si wewe, nisingekuwa" (2004:48).

Jambo la kushangaza ni kwamba inawezekanaje maneno kutoka kaburini? Mwandishi anakejeli hali halisi iliyomo katika jamii ya Kenya. Hali hii inafananishwa na ile ya enzi ya chama cha KANU, ambako wanachama sugu waliweza kukariri kikasuku manifesto ya chama chao. Waliweza kumpa kiongozi wao majina mengi ya sifa kama vile Mzee, mtukufu Rais, mkulima namba moja, Profesa wa siasa, n.k.

Katika sehemu hii mwandishi ameeleza kifo kama hatima ya maisha. Hata hivyo anasema kuna wengi ambao tayari wamekufa ingawa wana uhai. (uk.49). Maisha mjini ni ya kutafuta riziki. Kwa mfano, watu wengi walijitokeza majira ya jioni wakati bidhaa zao zilipohitajika na watu waliokuwa wakitoka kazini kukimbilia mitaani.

Wakati kama huu, askari wa Halmashauri ya Jiji, walipambana nao mchana-wangekuwa wameondoka na kuwapa fursa ya kuzitandaza bidhaa zao kila mahali penuni mwa maduka na kando ya barabara.

Katika jumba la makumbusho au makavazi, palijaa tungo za wasifu wa kiongozi wa nchi na tafsiri za hadithi nyingi za kizamani kutoka Ulaya, visasili vya Uyunani na mashairi ya *Ki-urdu*. Palikuwa pia na matoleo mbalimbali na nakala ya tafsiri ya Biblia. Lakini ajabu ya ajabu; hapakuwa na kitabu hata kimoja cha Historia.

Mkoloni alipoona wenyeji wanakazania kumgomea, aliamua kutumia nguvu. Inasemekana kuwa alipitisha amri fulani zilizowakataza watu kwenda huku na huku. Pili, alikuwa na jamaa aliowapaka mafuta kwa mgongo wa chupa wakaishia kuamini kuwa alikuwa rafiki yao wa kufa kuzikana. Hawa ndio waliompenyezea na kumfichulia ni akina nani waliokuwa wakiwachochea wenzi wao.

Hata hivyo, hali haikutulia alivyotarajia Ukolongwe. Watu walipata nguvu mpya baada ya kutoka kwenye Vita vya Fyuraa. Vita vyenyewe vilipiganwa huko mbali na wenyeji wengi walishawishiwa kujiunga na jeshi kwenda kupigana upande wa jamaa za Ukolongwe. Huko ndiko walikotambua kuwa nyuma ya figu la ujasiri aliovaa Ukolongwe kulikuwa na woga wa kujinyia nguoni. Sasa walichachawa na hata kuanza kuimba nyimbo za kuhimizana:

Ukolongwe aondoke, tule wimbi wa mayungwa.
Ukolongwe aondoke, tulime ngano na kahawa.
Ukolongwe aondoke, tupate sisi kupuwa,
Ukolongwe aondoke, siri yake tumejuwa. (Wamitila 2002:50).

Alipowasiliana na jamaa zake huko Ulaya, walimshauri aondoke. Kabla ya kuondoka walimshauri ahakikishe kuwa amejipenyea katika bongo za wenyeji wa sehemu hiyo, ahakikishe kuwa amepenyeza kabisa katika uboho wa mifupa yao; ahakikishe kuwa amezama katika kiini cha *seli* zao. Ilikuwa lazima mkoloni awe uhalisi na ndoto wakati mmoja. (uk. 51).

Baada ya Waafrika kushiriki katika vita vikuu vya ulimwengu, huko Burma na kwingineko ulimwenguni, walipata ujasiri. Walijiona bora kuliko weupe wenzao. Jambo hili liliwapa motisha ya kutaka kudai uhuru wao. Makundi ya uasi yaliundwa ili yaanze kupigania uhuru wao. Kundi la Mau Mau lilikuwa maarufu sana wakati huo. Washiriki wa kundi hili walijificha msituni na walikuwa wakimvamia mkoloni kwa njia ya siri. Watu wengi walikufa na kupoteza makazi na hata ardhi yao, lakini lengo lao lilitimia. Wazungu waliondoka na wale waliobakia walianza kujiondoa mmoja mmoja. Wengine waliapa kuwa hawataondoka kabisa, kwani hapo ndio nyumbani. Katika hotuba ya msimulizi, aliwaeleza watu umuhimu wa kuyawazia mambo ya leo tu. Jana imepita na haina maana tena. Nchi inayotawaliwa na jana ina matatizo. Muhimu ni leo, leo tu. Hata kesho tusiiamini sana! tuiwaze leo sana! Kesho, tutaikabili ikifika. Daraja huvukwa baada ya kufikiwa!"

Profesa alifanya utafiti kuhusiana na kisa cha mwanamke fulani aliyedai kuwa dada ya Mzee. Wiki tatu baadaye Profesa alikufa katika ajali ya barabarani.

Mzee aliongoza nchi nzima katika maombolezi ya kifo cha Profesa. Aliwakumbusha pengo kubwa aliloliacha ambalo halikuweza kuzibika. Aliwaahidi kuwasaidia jamaa zake. (uk. 52).

Katika sura ya ishirini na sita, mwandishi anatufahamisha kuwa giza halitandi milele, yaani matatizo hayawi milele. Msimulizi aligundua jambo ambalo halijangunduliwa na wengine. Mamanchi alimwambia kuwa ana bahati kwa ung'amuzi wake unafanya kazi. Unafanya kazi ndio maana unaona kitu ambacho wengine hawakukiona. Lakini akamtahadharisha kuwa waonao hawatakiwi katika jamii. Mkoloni ni kiumbe kisichoeleweka kwani mwandishi anadai kuwa anatumia mafumbo magumu yasiyoweza kufumbuliwa. Utamaduni wa mzungu bado upo milele. Ukoloni haukuzikwa, kaburi lake bado li wazi. Msimulizi anatufahamisha tujifunze kutokana na historia, tusiche tukalaaniwa kuyarudia makosa ya jana, yaani makosa ya historia yenyewe.

Baada ya wenyeji wa Afrika kupata uongozi kutoka kwa mzungu, walianza kulegea kwa madai kuwa yote yamekwisha. Watu walianza kulala kwa miaka na mikaka, usingizi wa pono. Maneno matamu ya ukombozi yalitolewa kwenye sherehe za kusherehekea uhuru wa Mwafrika. Wale wenyeji ambao walishukiwa kuwa waasi, wasaliti walishtakiwa kwa kosa la uhaini na kuteswa kwa vijumba vya nchi kwa chini.Taswira tunayoipata katika sura hii ya ishirini na sita ni kuwa hakuna mahali pa usalama duniani.

Hadithi ya Mzee inaendelea (uk. 56), yeye ana matumaini ya kuwa kiongozi wa muda mrefu sana. Alijifunza mbinu za kuwanyamazisha wapinzani wake. Vijana wa Mzee walipelekwa kwa mafunzo maalum ya kuweza sio tu kutambua mienendo inayoishia kuwa ya kiuasi bali pia kuweza kuwaza kiakili walioenda kombo. Walijifunza mbinu mpya za kutia hofu. Basi ikafikia kilele wakati huu walipoanza kupendekeza Mzee ajitangaze kiongozi wa maisha.

Wafuasi sugu wa Mzee walimdanganya kuwa umma wote ulikuwa nyuma yake. Maana yao ni kuwa umma wote ulimwamini kwa sababu yeye ni kila kitu, bila yeye nchi yao haipo. Yeye ni jana, leo na kesho.

Vile vile katika sura ya ishirini na saba, mwandishi anayapinga maoni haya ya wafuasi sugu kwa kusema kuwa katika nchi yao hata mchana hauaminiki tena. Hali hii ni ya vinyume, mchana huweza kuwa usiku na usiku mchana.

Katika sura ya ishirini na nane, tunapata watu wanaotoka upande wa chini wengi wao walikuwa wakiimba nyimbo za maafa. Mamanchi anasema kwamba kila mara wanasumbuliwa na mawazo, kuteswa na Ukolongwe na kinyonga. Sauti zao zilibakia hai kwani kilio cha haki hakifi. Wafao ni watu wenyewe. Katika sura hii pia mwandishi anatufunza kuwa subira huvuta heri. Mamanchi anamwambia msimulizi kuwa kuna johari muhimu za kuvumbua ikiwa atakuwa na subira. Akisubiri atakuwa shujaa wa kisawasawa (uk. 59).Msimulizi anamuuliza Mamanchi kama anaamini kuzaliwa mara ya pili.

Kuzaliwa kisha kufa na kuzaliwa tena. Mzee anadai kuwa yeye amezaliwa na kufa, akazaliwa na kufa na kuzaliwa upya:

> "Mara zote wananiua lakini wameshindwa kuniondoa tamaa ya kuwako
> Kila nikija huwa na sura mbalimbali, anaweza kuwa dadake, kinyonga
> na mamake wakati ule ule. Alipozaliwa alikuwapo. Hata Ukolongwe
> alipofika huku alimkuta lakini kutokana na dhiki alizozipata wakati
> wake alishia kufa."

Ukoloni ni suala la kudumu. Upo huku na mwingine upande wa pili. Ni kama kitu kusema kuwa amekufa na kuishi wakati huo huo. Lakini siku moja ataweza kuishi bila ya kufa. Ukoloni utaishi milele, enzi zote zitapita kama moshi na kuyeyukia katika anga ya mapito na mapisi. Ukoloni utabakia ukichanua na kutoa rihi kama ua la mti usiosikia kiangazi. Tumaini la kesho limefumbwa kwenye mwili wa mkoloni. Wana wa kesho watanyonya maziwa yake. Mkoloni aliwafunza wenyeji wa bara la Afrika njia za kuishi na wao wakapuuza. Sasa wanamlilia kwa misaada ya kufutilia mbali madeni.

Sura ya ishirini na tisa, Kitungule alitoka kazini mapema siku hiyo. Kingunge alikuwa amempigia simu waende pamoja mahali fulani. Alikuwa anataka wakutane karibu na Maakaba Kuu. Mkuu wa Kitungule alimpa ruhusa ya kuondoka mapema ingawa ilimbidi asiseme ukweli.

Hakusema ukweli kwa sababu si yeye wa kwanza kusema uwongo. "Shirika la umma hili unafikiri tutaliua sisi?" Nchi imekufa hii, hatutaifufua sisi! . . . Hadi kesho bwana," alisema mkuu wake kwa bashasha. Walipokutana na Kitungule na Kingunge mjomba wake Kitungule, alimweleza haja ya kumuona yule kijana aliyekuwa akimhoji yule Ombaomba! Mjomba alimtaka yule kijana kwa sababu ya hadithi aliyokuwa akiandika.

Walishika njia moja kwa moja kutembea penu za maduka yaliyokuwa katika barabara ya Mzee. Hiyo barabara ilipewa jina hilo kama makumbusho ya kusherehekea miaka kumi ya uongozi wake. Hii ilikuwa barabara ya kibiashara na ilifahamika na karibu kila mtu mjini. Inasemekana kuwa zamani barabara yenyewe ilijulikana kama barabara ya *Chandri*. Waliofanya kazi katika maduka hayo walilalamika kila mara kuhusu malipo na mazingira yao ya kazi. Wachuuzi wa nguo, saa, mboga, bidhaa za plastiki kutoka Uchina na India walitapakaa kila mahali. Barabara ilijaa sokomoko la wachuuzi waliokuwa wakiimba tungo za bei zao.

Wenye maduka walikijunyatia kwenye maduka yao kwa usununu wakisikiliza bei zilizotangazwa na wachuuzi wale. Wenye maduka walidai kuwa wafanyakazi wao ndio walioiba nguo na bidhaa zingine zinazoishia kuuzwa kwa bei za kutupwa mita chache kutoka ilipo milango ya vyuma vya maduka yao. Hali hii haikuendelea kwa kipindi kirefu kabla wale wachuuzi kuanza kusakwa na askari wa Halmashauri ya Jiji.

Kitungule anaona kuwa kuna nafuu baada ya wachuuzi kufukuzwa jijini, lakini, anatambua kuwa wamenyang'anywa huduma muhimu kama vile bei ya nguo. Wenye maduka waliziuza nguo kwa bei ghali ilhali wachuuzi waliuza kwa bei ya chini kabisa. Kwa mfano, shati mpya dukani ni shilingi mia nne lakini shati hiyo nje ni shilingi sitini pekee. Kutofautiana kwa bei za bidhaa ndiko kulilifanya Halmashauri ya jiji kuanza kuwatorosha wachuuzi kutoka penuni mwa maduka ya Wahindi.

Hadithi inaendelea huku Mzee akiendelea kupanga mipango yake ya kuwa kiongozi wa kudumu. Alikuwa ashatafuta jina la kufaa: **OmniMzee**.

Kwa upande mwingine, mzee anaona kuwa uongozi unaenda sambamba na ugumu. Mzee alifanya mazoezi kadha jinsi ya kujieleza upya ili aweze kukubalika na umma. Aliandaa maneno maalum ya kuwalainisha watu pamoja na kuwashawishi wengine waliokuwa wameanza kutoa maneno yao chini kwa chini (uk 65).

Mwandishi pia amelizungumzia suala la utandaridhi. Suala hili linavunja mipaka. Utandawazi umeangusha kuta zilizojengwa zamani kati ya imani na ndoto. Anasema kuwa ni kupitia utandawazi ambapo nchi za Ujerumani ziliungana pamoja kwa sababu za kiuchumi, kisiasa, na kijamii.

Utandaridhi ulianzia huko Ulaya na sasa unaenea kote duniani kwa kasi sana. Ulianzia Uingereza, Ujerumani, Ureno, Uhispanialo, Ubelgiji, Ufaransa na Uholanzi.

Kimbunga cha utandaridhi kiliangusha kuta na majengo kadha imara; makasri hasa ya wafalme maarufu. Serikali za kiimla ziliangushwa barani Afrika na sehemu zingine za Asia. Hazingeweza kuhimili kimbunga hiki cha mabadiliko.

Wakati majanga (Tsunami) yamefika katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, mataifa yaliyoendelea yanatuma misaada ya kwa ukarimu wa kutosha ili kulinda biashara zao

Mwandishi (uk.67) anatusimulia kisa kuhusu ulimwengu. Inasemwa zamani ulikuwa pande moja tu, bara moja lililotanda huku na huku kisha kukazuka tetemeko na kugawa mapande mengi. Yalikuwa na majina mengi lakini yeye anakumbuka mawili tu, lile la Godi-Wana na Huraa-Asi! Hali iliendelea hivyo, yaani tetemeko, tetemeko; kizalizali mpaka. Uropa. Asia. Afrika and Australia.

Watu nao walizaana na kuongezeka. Miaka ikaenda na kupita. Siku moja katika pande moja nadhani Huraa-Asia, palizuka jitu kubwa. Wanasema lililiwa na miguu miwili lakini mikono mingi na vinywa visivyohesabika kama majini ya Alladalin. Kwa kifupi, lilikuwa lafi lililopenda kula, kubugia na kumeza kila kitu. Ilibidi lianze kwenda huku na huku mradi lipate cha kutia kwenye vinywa vile lukuki.

Wakati mwingine lilisukumwa na nia au hamu ya kula tu, kutafuta bizari na iliki kukifanya chakula kipendeze. Mikono yake ilizoea kushikashika na kupakatapakata vitu vya wengine; huku kwetu tunasema ukimwona mtoto anafanya hivyo ujue umezaa mwizi. Wazee wanaosimulia kisa cha jitu hili wanasema kuanzia siku hiyo lilijulikana kama jivi. Kitabia lilijaa kiburi na lilijiona bora. Basi jivi lilianza kujiendea huku na huku: likavuka kwake na kuhamia kwa jirani. Kila lilichopata lilitwaa na kubugia kinywani. Lilipokatazwa lilitumie ile mikono mingi likabinya, likasongoa, likaua. Haukuwa muda mrefu likawa limesababisha maafa, watu wakatoroka makwao. Mwili wake ukawa mkubwa.

Sasa; likashindwa kutembea na kuishia kuagiza lifanyiwe kila kitu. Kazi yake ikawa kukaa tu kusimulia visa vya mashimo ya Mfalme Suleiman, Robinson Crusoe na kuimba wimbo wa Arya na mwingine wa Bora-mimi-Kitovu._Wakulima walilima na walipovuna kila mmoja kulileteа kipeto cha mavuno; likakaa tu. Wakwea nazi walikufa wakifuatia madafu kulipelekea. Watu walipoliangalia wakasema hili limezidi sasa. Likapewa jina lingine **MWINYI**.

Watu wakalikumbusha umuhimu wa kufanya kazi likagoma; unajua tena aliyezoea twaa . . . sasa lilikuwa limekusanya vitu vingi. Maendeleo nayo yalikuwa upande wake kukazuka viwanda sasa liliweza kuyapeleka mazao viwandani. Likawashikia watu shokoa kufanya kazi viwandani . . . jasho, jasho nalo linawanda na kunenepeana. Kazi nao wakamenyeka viwandani. Akazuka mfanyikazi mmoja wa kayahudi na kuanza kuwahemasisha waungane kuupinga ubepari wa Mwinyi. Jitu likapata jina lingine: **BEPARI**. Wakati huu nalo lilishajieneza kila mahali, kule ambako halikuhitaji kwa sababu ya malighafi ya viwanda lilihitaji kwa sababu ya soko-kuuza bidhaa zake. Mzee, unajua tena kimya kingi kina kiembeza. Halikuweza kula kila kitu.

Hatimaye liliihsia kuwa na ufalme mkubwa sana. Likashindwa kuumiliki. Uzee nao ulikuwa ukitafuna ndani kwa ndani kama fuko. Walishikiwa shokoa nao walihasirisha kulishikia miundu. Sasa likageuka majini ya Aladdin hasa na kuingia kwenye akili za baadhi yao.

Inasemwa kuwa lenyewe lilipotea hivi hivi lakini harufu yake. ikabakia kama ya beberu. Kuanzia siku hiyo likapewa jina jingine: **BEBERU**. Harufu yake bado imetanda ulimwenguni mpaka leo. (67-68).Hadithi ni njia mojawapo ya kuelimishana na kurithishana maarifa na ujuzi tangu zama na azali. Hadithi ni sehemu ya utamaduni wa jamii zote.

### 3.5.4 SEHEMU YA NNE (SURA YA 31-42)

Msimulizi alikuwa karibu kukata tamaa aliposikia sauti ya binadamu. Yeye yumo katika hali ya utatanishi, kwani wakati huo giza lilienea kila mahali. Hakuweza kujua kama lilikuwa giza la jana au la leo.

Sauti ya pili ilimpa matumaini kwa sababu ilimwelekeza alipokuwa kijana. Kijana alikuwa mahali ambapo kila mtu alimwamini, kijijini, mijini, nchi na bara zima. Mahali hapa ni Marekani. Kila mtu aliikumbuka dhiki ya jana, visa vya kufungwa kwa wenyeji kwenye kungwa na kusafirishwa kwenye meli kama **AMISTAD 1** vilikumbukwa na kila mmoja. Dhiki ya kuwa manamba kwenye mashamba ya makonge ya wazungu, kufia migodini, kurithisha Wareno, watu kuliwa na simba wakijenga reli an umma kucharazwa *djambok*.. Vyote vilikumbukwa na kila mmoja. Nakumbuka jinsi kila mmoja alivyotokwa na machozi kisa Mamanchi kiliposimuliwa . . . mengine hayasemeki.

Sauti ya tatu ilitoa hotuba ya matumaini. Baadhi ya maneno yaliyotutia matumaini ni kama vile ujamaa wa Kiafrika wenye misingi ya ubinadamu, ujamaa, *Pan Africanism* na Unegritudi. Watu walishangilia ufufuo huu mpya.

Mzee alipewa jina mpya: Musaleo! Musaleo! Musaleo! Kutokana na huu ufufuo mpya, Marekani ikapewa jina mpya la **Musaleo!**

Wakati huo Marekani ilikuwa inategemewa lakini baada ya kuwa askari wa ulimwengu, ikaanza kujidai kuwa mvumbua kila kitu na kujipa Uungu. Neno lake likawa kila kitu! Kukosolewa kukawa uhaini. . . Mamanchi kikamshika kichomi.

Baada ya kipindi kirefu cha amani, Marekani ilijawa na kiburi na kuanza kugonganisha mataifa baina ya mataifa. Ilianza kuangusha serikali mbalimbali hasa zile waliokataa sera ya ukabaila. Kukaanza kutokea shida, kipindi kirefu cha tanzia. mitutu ya bunduki!, ajali za uongo na kweli! Kwa njia hii watu walikufa. Masefule wengi mpaka na maaskofu. Hukumu za kifo! Jela ya milele ni baadhi ya matatizo yaliyotokea na kiburi cha Wamerikani.

Ukoloni mkongwe (Ukolongwe) uliweza kuwaathiri viongozi walioshika hatamu ya uongozi baada ya nchi mbalimbali kujinyakulia uhuru wao. Hata wakawa wabaya zaidi kuliko wakoloni wenyewe. Wakiambiwa kuwa wana chembe chembe za ukoloni, wao huja juu na kusema kuwa mabaya yaliyopo yanatokana na jana, msinilaumu, mimi ndiye mwanzo wa ufanisi huu. (uk.70). Na hayo ndiyo matatizo yetu sisi. Unajisamehe kwa kuwalaumu wengine. Udhaifu wetu wa kuamba na kuambizana kuwa zimwi likujualo halikuli likakwisha. Siku hizi halikuli tu bali linakufuta na kukufagilia kabisa. Hapa uhalisi uligeuzwa, meno ya mbwa yakaanza kuumana!

Msimulizi aliendelea kutafuta kitendawili chake. Alisikia sauti kama ya Amina ikisema; Jikaze! Jikaze! Jikaze! na hiyo sauti ikampa msimulizi matumaini ya kuendelea na safari yake ya kutegua kitendawili.

Kijijini watu wameacha kuyakosoa maisha kama wanavyopaswa na badala yake wanaimba tenzi tu kuhongera miradi ndoto. Tanzia wanazoigiza kimya kimya zimewatawala. Mwandishi anatufahamisha kuwa japo duniani sote tu katika ngazi mbalimbali. mbinguni sote huwa sawa, sote ni binadamu.

Katika sura ya thelathini na mbili, wahusika watatu Anima. Kitungule na Kingunge wanasimama nje ya mlango wa kuingia kwenye chumba cha wagonjwa mahututi (ICU). Kulikuwa na saa kwenye mlango yaelekea iliwekwa pale kuwasaidia waliokuwa pale kuyajua majira au kuhesabu nukta na dakika za uhai.

Mlango ulipofunguliwa, Daktari M'mati Mort, alitokea. Aliwafahamisha kuwa kulikuwa mgonjwa mmoja katika hali mahututi (uk.72). Anima alipomuuliza "ana nini?", Daktari alimwambia bado wanafanya uchunguzi lakini anavyoendelea kuna sumu.

Naye Kingunge akamuuliza "sumu ya aina gani?" Daktari alimwambia ni vigumu kujua. "Labda ndio... lakini hapa itabidi tufanye uchunguzi", daktari akaongezea.

Nesi alimfahamisha daktari kuwa maabara ya hospitali hayana vifaa vinavyopasa kufanyia uchunguzi wa aina hii. Vingine vimo katika chumba cha daktari mkuu lakini amekwenda likizo.

Baadaye kulitokea mahojiano miongoni mwao:

| | |
|---|---|
| Anima: | Amekwanda likizo na funguo? |
| Daktari : | Njia tulinayo ni Wazito Nursing Home lakini ni ya kibinafsi wataka pesa kabla ya kufanya lolote! |
| Kitungule: | Kiasi gani? |
| Nesi: | Rubuni ya shilingi elfu ishirini wakati mwingine zaidi? |
| Kingunge: | Mpelekeni huko tutalipa! |

Yule Nesi alimwaashiria wamfuate. Swali la kwanza alilouliza ni kama walikuwa na gari. Nesi aliendelea kuwaelezea hali ya magari katika hospitali hiyo. Magari ya hospitali hii hayafanyi kazi.

Moja liliuzwa tupate pesa za kununulia vitanda zaidi. Ambalanzi mbili hazifanyi kazi; iliyokuwa nzuri imechukuliwa na Waziri wa Afya kwa ajili ya dharura ya kibinafsi.

| | |
|---|---|
| Kingunge: | Ya nini? |
| Nesi: | Watu wanasema inatumiwa kupeleka wanawe kutazama wanyama kwenye mbunga za wanyama. Wengine wananong'ona kuwa inasafirisha madawa ya kulevya! |

Mjomba alisema kuwa alikuwa na gari. Waliondoka kuelekea Wazito Nursing Home. Akili ya Anima ilikuwa katika hali ya vuta ni nikuvute kubwa, sehemu moja iking'ang'ania kubakia alipokuwa rafiki yake na nyingine ikitamani kujua matokeo. Kingunge alilipa pesa alizokuwa nazo.

Kitungule na Kingunge waliandamana kwenda alikoishi Mugogo Wehu. Hali yake ilikuwa bado mbaya lakini daktari alikuwa na matumaini. Alipomwuliza daktari kama angekufa! Daktari alimwambia "sio leo,"

Anima na Kitungule waliondoka hospitalini jioni kabisa. Ilikuwa vigumu kupata usafiri kwa sababu magari yalikuwa haba wakati huo wa jioni. Zamani haikuwa shida kupata usafiri kutoka hapo kwa sababu yalikuwako kwa wingi. Baadaye madereva walianza kulalamika kuwa walisumbuliwa an majambazi jioni katika maeneo hayo.

Waziri wa Masuala ya usafiri na ujenzi alipoulizwa ashughulikie suala hilo, alisema, "Wenye magari ni kama nyinyi, hawana uzalendo. Wanachochewa na wageni. Nchi hii haina tatizo la usalama, hiki ni kisiwa cha amani katika bahari iliyochafuka!"

Sura ya thelathini na tatu, Ngwena anatufahamisha kuwa tulianza kupata uhuru wa Afrika tangu mwaka wa hamsini na nane mpaka miaka ya themanini na tisa (1989's). Profesa wa kisiasa, alikuwa na ufundi mkubwa na kuyasokota maneno. Alizimudu kunga na semi zetu. Tena alikuwa fundi hasa wa kujua kipi wanataka watu na kipi walichukia. Lakini lazima mtu awe imara, asinywee tu, haitoshi kushika fimbo tu. Lazima uitumie na mara hii sio kupasulia maji! Njama za leo zinahitaji kuchangamkiwa! Ilikuwa ni lazima mbinu mpya zibuniwe. Mifano yazo ni kama vile mashtaka bandia, mapatano maalum na idara ya sheria. Sheria mpya zikabuniwa kama vile *dentention without trail*, na *preventative dentention act*. Hatua hizi zilibidi kwa sababu Mzee aliona hakuna haja ya kuharibu wakati kwa kesi zisofaa hasa enzi hii ya kujenga nchi.

Ililazimu kila matu awe mzalendo; ajue Mzee ni **Osagyefo** (Musa), Jogoo anayewaandama makoo wote; Simba mwangusha Falme, na Mjukuu wa Solomon; shujaa Mfumua-ufalme wa Uingereza. *Life President*, Alpha na Omega.

Kilele kilikuwa pale Profesa alipopendeleza apewe jina mpya kutokana na wasifu wake wa kutowezekana. Jina alilopendekeza yeye. ***Jini-Hadiri-Boko Hasa!*** Damu ya uhuru ilianza kutiririka wakati huo katika jahazi la taifa. Matokeo ya umwagikaji huu wa damu yalikuwa mapindizi (coup d' et al ukabaila, Ethnic Cleansing, tanzia, wazazi wakafa, wakabakia watoto, waliolazimishwa kushika bunduki. Watoto walisusia shule na umaskini ukashika mizizi. Msisimuko wa vyama vingi vya kisiasa ukazuka. Zilianza vuguvugu. Vuta nikuvute ya upinzani. Wanafunzi wakalalamika kuwa elimu imekosa mwelekeo. Wanawake nao wakaanza kudai wanapuuzwa kwenye nyadhifa kuu serikalini na wakapinga tamaduni za jadi (uk.76).

Profesa anaita hali hii ushindi wa *consciousness*, kujua jema na baya, bivu na bichi. Siku nne baadaye mke wa msimulizi mwenyewe akapigwa risasi ya kifuani akitoka *supermaket*. Polisi waliapa kufanya kila kitu . . . hatutatulia hadi wahalifu wapatikanae; mawe yote tutayabirua.

Sura ya thelathini na nne, mwandishi anazungumzia siku kuu ya Leba Dei. Ilikuwa Mei mosi, Leba Dei, siku ya wafanya kazi. Anima hakwenda kazini wala hakuandamana na wafanya kazi wenyewe kwenda kusikiliza hotuba ya kiongozi wa taifa katika uwanja wa mafanikio. Alilazimika kwenda kuitazama hali ya rafiki yake aliyelazwa katika hospitali ya *Wazito Nursing Home*. Hali yake bado ilikuwa mbaya.

Madaktari na manesi wachache walikuwa kazini siku hiyo kwani wengine walienda kuhudhuria siku kuu ya Leba Dei na kusahau wagonjwa. Kitungule alihudhuria sherehe hiyo ya Leba Dei. Kulikuwa na tamasha za kila aina,.

Watoto walikariri mashairi, misafara ya madaktari na maguo yao meupe na *stethiskopu* nyingi, kuvyatuliwa kwa mizinga na majeshi na hatimaye hotuba zilizoishia kwa watu kusema Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mkombozi Mzee! Mara tatu.

Sura ya thelathini na tano, Joto kubwa lilienea kila mahali. Sehemu hiyo ilikuwa na mteremko mkubwa, chini kulikuwa bonde lililofunikwa na ukungu. Kulikuwa na baridi upande wa juu na kulikuwa na joto jingi kuliko chini. Swali, lilitokea wapi? Kutokana na somo la jiografia, huko chini, kwenye kiini cha ardhi kuna joto kubwa . . . ndipo inapotokeza *Magma*, yaani zaha, inayotapikwa huku juu milimani na kuishia kuwachoma walioko.

Mwandishi anasimulia kisa cha kasuku. Huyu ni mnyama mwenye mkia kisha anajiuma mwenyewe kwenye mkia wake. Kisa hiki kilitajwa na Mamanchi. Mzee alipozaliwa alikuwa na kipawa fulani maalum cha kuiga. Yeye alipokuwa kijana aliwapiku wenzake kwa kuiga milio ya wanyama kama mbweha, fisi, duma, kiboko na kima. Pia waliwaiga ndege kama shorewanda, kitwitwi na hasa kabisa kasuku. Maeneo ya kwao hapakuwako na kasuku lakini watu waliiga tu. Watu waliamini vitu ambavyo hawajaviona na wanaishia kuwa stadi.

Mzee alimteua msimulizi katika kamati ya kuzua mbinu za kuyazambaza mawazo yake vijijini, mijini, nchini, na barani. Na huu ukawa msingi wa ***Dogmazee.*** Huu ni mfumo wa imani unaofundishwa, imani ya kukubali bila kusaili. Viongozi hawa walipendekeza mafunzo hayo yaanzie mashinani hadi vyuoni. Ilibidi waanzie shule za malezi. Ili kuendeleza propaganda hii, mabango makubwa na makaratasi makubwa yaliandikwa kila mahali: shuleni ofisini, hotelini, viwanjani, barabarani na vyuoni.

Msimulizi aliteuliwa Waziri wa Taarifa na Utangazaji. Wafuasi walipendekeza Mzee ateuliwe kupewa tuzo ya *"Nobel Peace Price"*. Wakuu wa Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, Ureno, Uhispanialo walipendekezewa kumteua Mzee apewe tuzo hiyo ya *Nobel.*

Wilayani na mikoani ilibidi watumie chifu, Akida na vijana wa Mzee kuwahimiza wachangie kufanikisha mfumo huo. (uk. 83). Wafanya kazi vile vile walikatwa asilimia kumi ya mishahara yao kugharamia mradi huu.

Sura ya thelathini na saba, Mamanchi anaanza kwa kuwahimiza wenzake Komba na Anima. Anasema "Usikate tamaa! Jikaze! Jikaze! Jikaze!" Kazi ya kasuku na Komba ilikuwa

kuzunguka huku na huku wakisomba waliokwenda kinyume na matarajio ya **Dogmazee**. *Intelligence Network* ilikuwa nzuri. Kulikuwa na mfumo ulioundwa kama bao kuu la kugawia umeme. Mfumo huo uliwekwa kila mahali kama vile vyuoni, shuleni, mitaani, hospitalini na hata chooni. Ilikuwa kazi muhimu kuhakikisha kila mtu anaogopa na muhimu zaidi anaogopa kila kitu asichokiona.

Dkt. M'mati Mort alikuwa mzalendo na kwa hivyo alituzwa tuzo ya kuwa raia mheshimiwa mkuu nchini, *distinguished citizen*

Mkuu wa maktaba kuu alikuwa na kazi kubwa. Katika mahali pa kuhifadhiwa nyaraka maalum vitabu vilivyopigwa marufuku, magazeti ya zamani, mabuku ya historia kuanzia zama za mamwinyi wa kiarabu, visa vya Timbuktu, Vita vya Pili vya Ulimwengu mpaka *Cold war*. Jumba lenyewe liliitwa mkomozi kwa maana walipotaka kumkomoa mtu yeyote sugu walielekea huko. Vijana wa Mzee walitumika kama jeuri ya chama, tegemeo kwa taifa ya kesho na miegemeo ya leo.

Katika kufaulisha ufisadi, nyaraka muhimu zilizohifadhiwa maktabani zote zilibadilishwa, ili kuzuia ushahidi. Viongozi wengi hujaribu kuizika historia.

Siku ilipotangazwa rasmi kuwa mpaka kati ya utaifa na ubinafsi umevunjwa, binadamu alianza kuteta. Basi hali hii ikaendela hivyo hadi ikawa ukiota ndoto unaweza kuhukumiwa hata kifo. Mbinu ya saikolojia iliweza kutumiwa kuyatawala na kuyaongoza mawazo ya mtu katika vyumba vya rumande kujua nani kaota kuwa kiongozi wa kijiji, mji, nchi au hata bara.

Katika sura ya thelathini na nane mwandishi analizungumzia suala la utandaridhi na sababu za mataifa kuungana pamoja na kuwa kijiji kimoja. Chanzo cha kukaribiana na kusongeana kimeelezwa na nadharia mbalimbali; kwanza wapo wanaodai kuwa kwenye kiini cha ardhi kulikuwa na mvuto kama sumaku. Mvuto huo ndio ulioyavuta yale mapande yakaanza kukaribiana. Sababu yao ni kuwa mwisho ndio mwanzo. Wengine wanadai kuwa uhusiano wao na Jivi ulikuwa wa kidugu ati.

Wataalamu nao walikanusha madai yaliyotolewa kama vile sumaku kuvuta mapande ya ardhi. Wanakana madai haya na kusema kuwa mapande (mataifa) mengine yalikubali kwa hiari kujiunga na mapande mengine na mengine yalilazimishwa.

Kuna kundi lingine la watu wanaodai kuwa mabadiliko yanayoletwa na utandaridhi yaliletwa na upepo wa mwisho unaoitwa *Ikti-Saad* ya masoko Huria. (2004: 90). Hata wengine zaidi wanasema kuwa mabadiliko haya yamesababishwa na sayansi, kwa sababu yanavunja mipaka na kuvuka majimbo na kufanya ulimwengu kuwa Kijiji kipya kinachongozwa na ***Yanguis***. sura ya meli.

Hiki ni kijiji kinachoelea majini. Jina lake ni Yanguis! Ana uwezo wa kushusha winchi, kufumbua msuko wa tanzia. Watu kutoka maeneo mbalimbali wanahitilafiana kwa majina wanayoyatumia watu kuhusiana na Yanguis. Watu wa Marekani ya Kusini wanatumia Yanguis, wa kutoka Iran au Iraq wanatumia ***Shai-Tani*** na wa kutoka Hindi wanatumia ***Amrika*** na huku kwetu wanamwita ***Mjomba*** kwa kuwa wanaamini ana roho nzuri. Sehemu hizi zote maneno yake yanasikilizwa sana na hata nyendo zake zinaigwaigwa (uk. 91).

Marekani sasa ni ***'Super power'*** baada ya kuangusha tawala na mifumo ya kisoshalisti kote ulimwenguni. Wameanzisha mfumo wa ukabaila kote ulimwenguni. Kwa sababu ya sifa za kiajabu za nchi hii ya Marekani, Mzee alipendekeza aitwe Mzee Yanguis! (uk. 91).

Suala la utandaridhi lilikuwa katika maeneo mengine duniani sasa yamefika barani Afrika, ndipo Mzee anasema:

> "*. . . kimbunga alichosema hapo kabla kilikuwa kimefika huku.* "(Uk.92*)*.

Utandaridhi umesababisha mambo mengi katika bara la Afrika. Mwandishi anayarejelea matokeo haya kwa njia ya kistiari kwa kusema:

> "Majengo kadha yaliyokuwa na mashirika ya umma
> yalikuwa yameanguka na mafaili yake kutapakaa
> kila mahali na kusomwa na kila mtu." ( uk.92).

Wataalamu nao walikanusha madai yaliyotolewa kama vile sumaku kuvuta mapande ya ardhi. Wanakana madai haya na kusema kuwa mapande (mataifa) mengine yalikubali kwa hiari kujiunga na mapande mengine na mengine yalilazimishwa.

Kuna kundi lingine la watu wanaodai kuwa mabadiliko yanayoletwa na utandaridhi yaliletwa na upepo wa mwisho unaoitwa *Ikti-Saad* ya masoko Huria. (2004: 90). Hata wengine zaidi wanasema kuwa mabadiliko haya yamesababishwa na sayansi, kwa sababu yanavunja mipaka na kuvuka majimbo na kufanya ulimwengu kuwa Kijiji kipya kinachongozwa na ***Yanguis***, sura ya meli.

Hiki ni kijiji kinachoelea majini. Jina lake ni Yanguis! Ana uwezo wa kushusha winchi, kufumbua msuko wa tanzia. Watu kutoka maeneo mbalimbali wanahitilafiana kwa majina wanayoyatumia watu kuhusiana na Yanguis. Watu wa Marekani ya Kusini wanatumia Yanguis, wa kutoka Iran au Iraq wanatumia ***Shai-Tani*** na wa kutoka Hindi wanatumia ***Amrika*** na huku kwetu wanamwita ***Mjomba*** kwa kuwa wanaamini ana roho nzuri. Sehemu hizi zote maneno yake yanasikilizwa sana na hata nyendo zake zinaigwaigwa (uk. 91).

Marekani sasa ni '***Super power***' baada ya kuangusha tawala na mifumo ya kisoshalisti kote ulimwenguni. Wameanzisha mfumo wa ukabaila kote ulimwenguni. Kwa sababu ya sifa za kiajabu za nchi hii ya Marekani, Mzee alipendekeza aitwe Mzee Yanguis! (uk. 91).

Suala la utandaridhi lilikuwa katika maeneo mengine duniani sasa yamefika barani Afrika, ndipo Mzee anasema:

> "*. . . kimbunga alichosema hapo kabla kilikuwa kimefika huku.* "(Uk.92).

Utandaridhi umesababisha mambo mengi katika bara la Afrika. Mwandishi anayarejelea matokeo haya kwa njia ya kistiari kwa kusema:

> "Majengo kadha yaliyokuwa na mashirika ya umma
> yalikuwa yameanguka na mafaili yake kutapakaa
> kila mahali na kusomwa na kila mtu." ( uk.92).

Watandaridhi wanadai kuwa wataondoa umaskini na kuleta uhuru wa kila aina na hatimaye kuwepo kwa maendeleo. Wamerekani sasa wameleta mambo ya wimbo wa Mefu, haki za kibinadamu, demokrasia, kuzuka kwa vyama vingi na mabadiliko ya lugha.

### 3.5.4 HITIMISHO.

Katika sura ya tatu tumetoa mukhtasari wa riwaya ya Bina-adamu! na Musaleo! Katika mukhtasari wa kazi hizi mbili tumemulika masuala kama vile Ukoloni mamboleo na harakati za ukombozi wa Waafrika. Vile vile tumeangazia maozo mbali mbali katika jamii. Sura inayofuata tutazihakiki kazi hizi mbili.

Mihimili tutakayotumia ni kama vile matukio ya kiajabuajabu, kigezo cha uhalisia na ndoto, uduara wa wakati, uvunjaji wa mipaka ya mahali, mtindo na nafasi ya visasiii katika uhalisiajabu

## SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tulishughulikia muhtasari wa kazi teule, Bina-Adamu! na Musaleo! Tulitoa maelezo ya hadithi katika kazi zote mbili kuanzia mwanzo hadi mwisho wao ili kutoa mwanga wa hadithi hizo kwa jumla. Tulianza na riwaya ya Bina-Adamu! na kuhitimisha na ile ya Musaleo!

Katika sura hii ya nne, tutahikiki kazi zenyewe kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu ifuatayo: matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida pia, huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya; uhalisi na ndoto, mipaka ya kijamii, kitaifa huvunjwa; wakati wa mahali vina uhusiano wa kiduara badala wa kistari; kufungamana na sanaa ya uhalisiajabu kama vile visasili na hadithi, mitindo ya kazi hizi mbili, mazingira na husiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano, ni baadhi ya mihili itakayotuongoza katika uhakiki wetu.

Ni muhimu kutaja hapa kwamba katika uhakiki huu si mihimili yote itakayotumiwa. Itakayotumika ni ile itakayofaa zaidi kufafanua riwaya hizi mbili, ili kuweza kuangazia hali zetu za kijamii, kisiasa, kiuchumi na vile vile kihistoria.

### *4.1 MATUKIO YA KIAJABU.*

Mojawapo ya ishara ya uhalisiajabu ni matukio ya kiajabuajabu yanayoogofya, kuduwaza na kushangaza. Matukio haya hata hivyo husawiriwa kama ya kawaida tu. Riwaya hizi mbili zinazungumzia matukio ya kweli yanayotokea katika jamii. Kwa mfano, riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo! zinatumia stiari ya kijiji, kisiasa na chumi zinazodhibitiwa na upebari wa mataifa yanayoendelea. Riwaya ya Musaleo! ni riwaya inayojaa tashtiti, ucheshi na ukweli unaokerakata maini. Mhusika Bina-Adamu anatujulisha:

> Nilipozaliza niliwakuta watu wakikiogopa kiini cha kijiji chetu na mpaka leo unapoisoma hadithi hii bado wana kiogopa (2002:7).

Kwa mujibu wa Bina-Adamu, mtu ambaye angedhubutu kwenda kwenye kiimi chake angeishi kupatwa na madhara makubwa. Kwa mfano, mwanamume anayekwenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa lazima alizunguke jabali lililoko hapo.

Walifunzwa hivyo wakiwa watoto na wakakua wakiamini hivyo. Jambo hili si kweli mbali ni mbinu ya utawala. Ili wanajamii wawatawale wanajamii wengine, wanaotawala huunda usemaji unaowawezesha kuendelea kushika hatamu za uongozi.

Bali na imani na onyo hii, hapo kwenye kitovu cha nchi ndipo Bina-Adamu anaanza safari yake na ndipo anapomalizia. Mwandishi hapa anatuonyesha kuwa matatizo yanayozikumba nchi za Afrika, suluhisho itapatikana hapa hapa. Mwafrika mwenyewe ndiye atakayetatua matatizo yanayomkumba. Kwa sababu ya watu wa kijiji chake wanaishi pembezoni kwa kuwa wanaogopa kiini hicho. Jambo hili ndilo asili ya riwaya hizi mbili Bina-Adamu! na Musaleo!. Bertoncini (2004:8) anasema kwamba mwandishi anasisitiza utengano kati ya asili ya kijiji na pembezoni. Kuna maswali yanayopaswa kujibiwa. Kwa nini watu wanogopa kiini cha kijiji chao wenyewe? Katika safari za Bina-Adamu katika mojawapo ya nchi za Afrika, mzee mmoja wa nchi hiyo anamwambia:

> Mji wetu unahusishwa na mwingine unaoitwa Syria na Macedonia; yote ilikuwa na ufalme uliofanana na ki-hellenism. Wakati huo ndipo ustaaarabu ulipowekwa msingi kwenye kitovu hiki. Huu ndio ukweli ingawa sasa wanaukamisha watu wengi (2002:75).

Mzee huyu anatupa jibu la swali letu. Ikiwa Afrika ilikuwa kitovu cha maendeleo ulimwenguni, kulitokea nini hata Waafrika wakaanza kuogopa. Anaendelea kumwambia Bina-Adamu:

> Lakini ndivyo maisha ya siku hizi yalivyo. Uwongo umechukuwa kiti na kuketi kijijini. Picha za uwongo kuwahusu wakazi wa miji yote zimesambazwa, na ajabu watu wengi wetu wanazikubali! Wanakubali kuwa wao ni watu wa pembesoni tu! (2002:75).

Hapa ndipo jibu lipo. Ukweli ni kwamba watu wa kijiji chao Bina-Adamu wamekataa kukaa katika kitovu cha kijiji na kukaa pembezoni kwa sababu ya uwongo na kuamini waambiwavyo na wengine ambao labda wangetaka kukaa kwenye kiini wenyewe.

Jukumu kubwa la Bina-Adamu katika hadithi hii, ni kuwatafuta huntha ambao walilaaniwa (haijulikani na nani) na lazima waondolewe ulimwenguni, ili kuiondoa laana inayotanda juu ya kijiji (2002:8).

Baaada ya ya kumwona P.P., Bina-Adamu anawasikia wale huntha wakicheka kama alivyokuwa amesikia mara nyingi safarini mwake na anataka kuwafuata. Babu wa Zakongwe anamwambia kwamba hao huntha wako katika matendo na fikra. Matendo na fikra kama vile ya kibepari, ubaguzi wa rangi na ubinafsi ndio huntha. Aidha, huntha hawa wako kila mahali Bina-Adamu anakopitia:

> Dhana ya kijiji kama tuijuavyo ni mahali ambapo wanakijiji hupendana wala sio baadhi ya wanakijiji kuwatumia wengine kwa manufaa yao, ni mahali ambapo watu huheshimiana bali sio kutumia wengine kama wasio na utu na heshima yao, ni kushirikiana na kufaana kama ndugu wa kijiji kimoja wala sio baadhi ya wanakijiji kutumia dhana ya uanakijiji ili kuwadhulumu na kuwanyanyasa wenziwe kwa kuwapora kiuchumi na kuwafanya maskini wa kutegemea! (2002 :154).

Jambo hili ndilo linalomuudhi mwandishi wa <u>Bina-Adamu</u>! na <u>Musaleo</u>!. Itakuwaje ulimwengu ni kijiji huku baadhi ya wanakijiji hawana haki ya kuvua samaki katika maji ya kimataifa? Itakuwaje ulimwengu ni kijiji ilhali baadhi ya wanakijiji wanawatisha wengine kwamba wasipowanunulia bidhaa zao watanyimwa misaada wanayoihitaji? Dhuluma kutoka nchi za kimagharibi na zile za ulimwengu wa tatu inajitokeza zaidi tunaposikia jinsi ambavyo watu katika nchi za Afrika zinapolalamika:

> Lile ni jahazi au meli. Si neno tu? Kwani lugha ni nini? si makubaliano tu! Sisi si watumwa wa lugha, yaani hatupo kwa sababu ya lugha bali ipo kututumikia. Leo tutayapa maneno maana mpya?hii ndiyo sifa kubwa katika maisha ya leo!. Katika ulimwengu wa leo maana za maneno zimebadilika.chukua maneno yafuatayo: kijiji , uzalendo,na uhuru. Sote tunajua maana

ya kijiji. Wakoishi watu kwa ujirani na mapatano ndugu , mama baba, babu, na nyanya, mifugo na mizimu yao. Lakini kwingine kijiji ni kitu kingine kabisa. Tena mara hii kinaongozwa na sio na babu bali na mjomba!.( 2004:95).

Vile vile mwandishi anaendelea kusema:

> Wamemwaga mafuta hapa samaki wafe wapate sababu
> ya kutuletea makopo. Huko juu wanatupa mabaki ya nyuklia (2002:88).

Malalamiko zaidi yanasikika kuhusu shirika la fedha la ulimwenguni na benki ya ulimwegu. Haya mashirika mawili yana athari kubwa kwa nchi za Kiafrika na kiuchumi. Nchi za kiafrika zimekosa uhuru wa kuamua kesho na hatima yao. Uwezo huo umeingiliwa na mtaji unaoweza kuingia na kutoka utakapo. Jambo hili linadhihirika zaidi katika wimbo wa **MEFU** (*International Monetary Fund*):

> Shusa, shusha--.thamani yahela shushaa!
> Bana, Bana. ugavi wa hela banaa!
> Kata kataa . . . matumiz ya hela kataa!
> Hurisha, hurisha. . .. soko la hela hurisha!
> Punguza, punguza. . . mishahara duni punguza! (2002:87).

Wimbo huu wa MEFU, pia mwandishi ameurudia katika Musaleo!:

> Wimbo wa MEFU,
> Kushoto. Kulia. Nyuma. Mbele.
> Kila mahali, wimbo wa MEFU,
> Lugha imebadilika. (2004:99).

Utegemeaji wa kiuchumi kwa nchi za kimagharibi unamaanisha kwamba nchi za Afrika haziwezi kujiamulia masuala yao wenyewe.

Wanapanga mambo ya nchi zao kwa kutegemea pesa kutoka nje. Mipango hii inaweza kuwa ya kuimarisha elimu, kuongeza wafanyakazi mishahara na mengine mengi. Hata hivyo, mipango hii mara nyingi haifanikiwa kwa sababu ya vikwazo wanavyowekewa.

Vikwazo hivi vinaweza kuwa kupunguza idadi ya wafanyakazi, kuanzisha viwanda vinavyozifaidi nchi za kigeni au ununuzi wa bidhaa zao iwe ni samaki au ala za vita. Masharti

mengine ni kama vile kuanzisha sera ya vyama vingi vya kisiasa na ubinafsishaji wa mashirika ya kiserikali, kama njia ya kuleta uhuru na haki miongoni mwa raia.

Wasipofanya hivi msaada waliokuwa wameahidiwa husimamishwa. Mwandishi analalamikia ugandamizi wa 'ndugu' na 'wanakijiji' na nchi za Magharibi ambao huhakikisha kuna taratibu fulani wanazozitaka zitekelezwe.

Bina-Adamu anatujulisha alivyosikia maombolezi safarini mwake yanayofanana na ya watu wa kwao (Afrika):

> Shilingi inafifia. .wamcinyonga. . hizi SAPS zinatusapa uhai. .
> .kijiji cha wizi hiki . . . Dola inatukaba shingo . . .
> Yen ni kamba ya kitanzi (2002:137).

Katika safari yake, Msafiri anajulishwa kwamba uchumi wa ulimwengu unategemea dollar. Anajulishwa kuwa kuna kitu kama mizani hivi ya kupimia vitu. Mizani hiyo imeundwa kiajabu. Upande mmoja kuna uzito wa dollar. Fedha nyingine zinawekwa katika sehemu hiyo yingine. Hapo huwa na mtu ambaye kazi yake ni kuangalia uzani unavyoelekea; akiona unainuka upande usio wa dollar, unawaarifu wakuu wake wa kazi. Wakubwa wake huarifiwa ili "wasawazishe uchumi" kwa sababu kuongezeka kwa uzito kuna matokeo mengi sio tu ya kiuchumi, bali pia ya kisiasa na kijamii.

Msafiri anajulishwa kwamba P.P. hapendi kuongezeka kwa uchumi upande usiokuwa wa dollar kwa sababu kunaathiri *'balance of power'* bina-Adamu anapouliza inaathiri vipi anaambiwa kwamba "ukitaka aliyokuomba chakula leo arudi kesho, usimfundishe upishi!"

Uchumi wa soko huru wa kibiashara ni jambo lingine ambalo linaandamana na utandaridhi na ambalo Wamitila analilaani. Analilaani kwa sababu masoko na biashara hizo hutawaliwa na Wazungu. Soko huru na uhuru wa kibiashara huziwezesha nchi mbali mbali kuuza bidhaa zao kwa nchi zingine bila vikwazo vyovyote. Mwandishi anatujulisha jinsi viwanda vinauliwa na

hata bidhaa chapwa kuuzwa. Umma unapolalamika kuhusu jambo hilo, kwa sababu ya ukengeushi viongozi hao huwajibu:

> Haya ni maendeleo, hatuwezi kuyakwepa! Ulimwengu sasa ni kijiji!
> Hii ndio maana ya Free Market na liberalization. Tuko mbioni, nchi
> hii iko mbiioni! Hapana haja ya kupitia hatua zote za ukuaji,
> tunaweza kuruka nyingine ili twende sambamba na wakati! (2002:51 na 2004:90).

Mwandishi ametumia dhana ya kijiji kuelezea jinsi Waafrika walivyokosa kujiendeleza kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wanakijiji wanaweza kutoka pembezoni na kuanza kukaa katika kitovu cha kijiji ikiwa watayamaliza haya maovu na kuwa na umoja, waache kusikiliza uwongo na wajiamini. Umoja ni nguvu na wakiwa na amani waafika wanaweza kumfunga yeyote japo awe mkubwa.

Babu anasema:

> Kwa njia hii mtaacha kuishi pembezoni mwa kijiji!
> Itabidi tuwe nguli kupambana na hasidi wa kijiji
> Global villain (2002:155).

Mwandishi anapowasawiri Bina-Adamu na Kingunge katika <u>Musalec!,</u> wanapoanza safari zao katika kitovu cha kijiji kinachoogopwa wanamalizia pale pale. Mwandishi anakusudia kuonyesha kwamba matatizo ya bara la Afrika yamo tu Afrika na si kwingine. Ikiwa bara hili litaweza kushiriki kiuchumi, kisiasa na kijamii katika shughuli za kijiji (ulimwengu) lazima bara lijikague na kutoa suluhu.

Mwandishi amefanikiwa si haba kuwasilisha ujumbe huu wake kwa kutumia uhalisiajabu. Amefanya hivi kwa kuwasafirisha wahusika Bina-Adamu na Mugogo Wehu, kimawazo ambapo anazuru nchi na bara mbalimbali na kurudi. Ni katika uhalisiajabu tu jambo hili linawezekana.

Bina-Adamu Msafiri anapokuwa akiendelea na safari yake ya kuwasaka wavulana-wasichana (huntha) ananusa harufu ya beberu. Hii harufu inajitokeza kila mahali panapokuwa na alama ya maafa iliyosababishwa na P.P., ambaye ni kiwakilishi cha Marekani. Beberu ni mbuzi dume.

Kwa kawaida hutoa harufu mbaya na kali hivi kwamba mtu aliyemkaribia hata yeye hubaki na hiyo harufu.

Maana ya beberu katika muktadha wa riwaya ya Bina-Adamu na Musaleo! Ni mkoloni ambaye pia aliitwa beberu. Harufu yake ni maafa yaliyofanywa na mkoloni bado yapo ingawa aliondoka.

Bina-Adamu na Musaleo!, wanapopitia kwa majengo yaliyobomolewa, mashimo ya migodi na maafa mengine, harufu hii inajitokeza kumkumbusha msomaji kwamba beberu ndiye aliyeyafanya hayo (2004:68).

Binadamu anapokuwa akienda nchi ya Zakongwe ambayo ni kielelezo cha 'jana' ambapo kuna utu, upendo na waliohifadhi utamaduni wao na mengineyo, mkondo wa maji unawarudisha nyuma. Hali kadhalika Msafiri alitembea kwa hadhari hadi akatokeza upande mwingine wa pili uliokuwa na mteremko. Kusema kweli kutoka huko nyuma alikuwa akiteremka tu. Ilikuwa kama alikuwa akitoka juu kwenda chini. Alishangaa alikokuwa akienda lakini akakumbuka kuwa zamani walifundishwa kanisani kuwa ahera ni juu na jehanamu ni chini. Na ndipo alijiuliza swali: "je inawezekana nilikuwa nikielekea jehanamu?"alijitahidi hata kujivuta nyuma lakini akahisi kuwa anavutwa mbele na nguvu fulani (2004:45).

Mwandishi ametumia mtindo huu wa kihalisiajabu ili kuonyesha kupitia kwa Msafiri na Musaleo (Mzee) kwamba zamani kulikuwa na maadili hayo. Huko bado kuna ubinadamu kwa mujibu wa wenyeji wa huko. Kwa mfano, ni kweli Zakongwe ni kuzuri kwa sababu hata Msafiri anasema alikuwa amekupenda sana hivi kwamba hakutaka kuondoka huko. Pia Msafiri anapitia mahali kwingi sana katika safari yake ambapo watu wamesahau maadili haya. Bina-Adamu anapokwenda Zakongwe anabadilika na kuwa mtoto mdogo. Mwandishi anakusudia awe hivyo makusudi kwa sababu yake ya imani yake kwamba ikiwa mtu hatajifunza kuwa kama mtoto mdogo, hana popote atakapofika. Anaamini kwamba ulimwengu utaangamia siku ambapo

utakapompuuza mtoto mdogo. Mwandishi ana matumaini kuwa kizazi kipya ndicho kitakachoondoa uozo uliopo barani Afrika.

Mfano mwingine ni wa Zakongwe, ambapo Bina-Adamu alipokuwa akienda mahali, hapo, mkondo wa maji unamrudisha nyuma. Ni muhimu msafiri aone yaliyo nyuma kwa sababu anaelekea mbele ambapo hakuna mambo ya jana. Tunasikia mzungu mmoja akimwambia msafiri:

> "Tunaishi hivi kwa sababu hatuna jana. Inasemekana kwamba kuna mkoba fulani tulioupoteza" (2002:19).

Mkoba ambao unarejelewa na wazungu hawa ni kama ule Msafiri alikuwa amepewa na babu huko Zakongwe. Mzee anamwambia autunze vizuri kwa sababu kwenye mkoba huo mna utu, mapenzi na ubinadamu na kiini cha kuwako kwake.

Aidha mkoba huo utamfaa sana siku zijazo,kwani mwacha mila ni mtumwa. Msafiri anaondoka Zakonge kwa njia ya ajabu anapokuwa akicheza na watoto wenzake mchezo wa mwajificho. Msafiri anapokuwa amejificha anamwona nyoka mkubwa sana na katika harakati ya kumkimbia anaanguka mtoni. Anapotumbukia majini tena akienda nchi za ulaya anaibuka akiwa hana tone la maji. Hata hivyo, safari hii mkondo wa maji unakwenda mbele kuonyesha kwamba wametoka jana wakielekea kesho.

Anapokuwa katika safari ya kwenda Marekani anaona mto mkubwa. Ingawa Bina-Adamu hajui kuogelea, hakuna wakati ambapo anazama. Kwa kufanya hivi mwandishi anatumia uhalisiajabu kwa ufasaha kabisa. Maji ni kipengele muhimu cha uhalisiajabu na kutozama ni mojawapo ya maajabu ya uhalisiajabu.

Mwandishi anakusudia mhusika wake afike anakotarajiwa kufika na kwa hivyo hawezi kuzama. Ndio maana akatumia uhalisiajabu ili kumwezesha msafiri kutoa mantiki ya ushindi anaouona huko Marekani na nchi zingine za ulimwengu.

Mbali na kuzama, njia zingine za kiajabu za kuondoka sehemu moja hadi nyingine ni kupitia mawasiliano ya kimiujiza. Kwa mfano, anapokuwa katika safari ya kurudi bara la Afrika kutoka nchi za Uingereza, Bina-Adamu anapitia msitu wenye giza totoro. Anahisi kama ameangukiwa na kinyesi cha ndege kipajini. Anapokuwa anajaribu kuangalia juu ili kujitahadharisha, kinywa chake kinafunguka na kuangukiwa na rundo fulani analolitema nje haraka. Baada ya kufanya kitendo hiki anaanza kukohoa sana. Baadaye anatapika na kuzirai. Hatimaye anapopata fahamu anajikuta katika bara lingine ambapo anaona magofu makubwa (2002:83-85).

Tukio lingine linalodhihirisha matumizi ya uhalisiajabu ni kule kuongozwa, kupigwa mateke na ngumi na watu wasioonekana, kuongozwa na vimuri na hata mwanamke anayefanana na Binadamu. Aidha, msafiri anasikia akionywa, kushauriwa au kuongozwa na sauti asizoziona. Vile vile Msafiri katika Musaleo! Ameongozwa na sauti, na ndege aina ya bundi na mwanamke kwa jina Mamanchi.

Kisa cha babu mwenyewe kujifungua watoto alipokuwa uzeeni bila ya kuoa, kinadhihirisha uhalisiajabu uliomo kwenye kazi hizi (2004:13).

Kuzaliwa Mzee, hakuzaliwa lakini alitokana na kupasuka kwa mgumo mkubwa wa kijiji (2004:4). Uzeeni alijiona ukiwa na kuamua kuzaa watoto aliowaamuru nao wakazaane. (2004:5). Msafiri katika <u>Musaleo</u>! Aliongozwa na ndege, bundi, katika safari yake.

Katika bara la Afrika, watu walisema kuwa ndege hawa walitanguliza maafa, na kwa hiyo walikuwa ndege wabaya. (2004:39). Msimulizi hakuweza kuogopa kwa sababu alikuwa na hamu ya kutaka kumwona Bina-Adamu.

Maneno kutoka kaburini ni mfano mwingine wa kuonyesha matumizi ya uajabu katika kazi hizi. Wakati Msafiri alipopitia njia iliyopitia karibu na sehemu iliyokuwa na kaburi wazi maneno haya yalitoka kaburini mfululizo:

> "Mzee! Mtukufu Mzee! Kiongozi, Mwalimu Namba moja, Mganga, Msomi Wahedi, Mleta mvua, Musaleo! Wewe ni kila kitu kama si wewe, nisingekuwa!" (2004:48).

Mwandishi alitumia uajabu huu kueleza kuwa hata kama mkoloni aliondoka barani Afrika, bado nyendo, tabia na nguvu zake bado zinasikika. Mzungu alirudi kwa joho tofauti na kuendeleza ukoloni mamboleo kupitia kwa viongozi wenyeji.

## 4.2 NDOTO NA UHALISIA

Ndoto na uhalisia ni kigezo muhimu sana katika uandishi wa uhalisiajabu. Inawezekana hii ndio Wamitila (2002) anaita mandhari ya ki-nelibini *(kaleidoscopic)*. Mandhari ya aina hii huonyesha sifa ya utokaji kwenye ulimwengu halisi na kuingia kwenye ulimwengu wa kimawazo kisha labda kurudi kwenye ulimwengu halisi. Hii ndiyo mandhari iliyotumiwa katika riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo!. Mwandishi hupatwa na aina ya lepe. Mhusika akiwa katika hali hii huweza kusafiri kutoka hali moja hadi nyingine. Anaweza kuishi maisha yake ya baadaye au akarudi nyuma kwenye maisha yake ya awali. Mtu anapokuwa katika hali hii, hawi kwenye ndoto tu kwa minajili ya kuwa kwenye ndoto bali huwa njia ya kumwonyesha msomaji anayoyakusudia. Hii ni mojawapo ya safari za jagina.

Katika uhalisiajabu kuna matukio yanayofanyika ambayo huweza kuonekana kama ndoto labda kwa sababu ya uajabu wake kumbe ni "uhalisiajabu linaweza" au "uhalisiajambo linaweza." *Uhalisiajambo linaweza* ni dhana inayotumika kumaanisha hali ambamo jambo linaloaminika kutendeka hutendeka. Aidha, jambo linaweza kuonekana kama halisi na kumbe ni ndoto. Riwaya za (Bina-Adamu! na Musaleo!), ni ndoto anayokuwa nayo mhusika Msafiri katika kazi zote mbili.Kwa mfano, Bina-Adamu anapokwenda katika kitovu cha kijiji chao kinachoaminika kuwa hatari na kuwaza kuhusu jambo hilo, anapatwa na usingizi na katika usingizi huo ndipo mwandishi anapotunga hadithi yake.

Mhusika Kingunge katika riwaya ya Musaleo!. Alikuwa na hamu aliyokuwa nayo kwa miaka sita ilielekea kutimizika:

> "Ninaota siku moja kuiandika riwaya. Na sio riwaya tu lakini riwaya mahsusi ambayo haitakaa tu isomwe bali yenyewe itasaidia usomaji wake" (2004:2).

Mfano mwingine ni mazungumzo kati ya Mzee na Mugogo Wehu:

> Niliwauliza jamaa kadha waliokuwa upande huo. Niini? Hapana, hamna kitu kama hicho!" "Risasi sehemu hii? Mugogo una nini? Polisi kuua watu? Nchi hii? Labda huko ughaibuni. Hiki ni kisiwa cha amani. . . tena cha amani katika bahari yenye machafuko ya kila aina! Labda hukulala jana! Lazima unaota wewe!" Walikana. Lakini nilikuwa macho wazi inawezekana kuwa ni ndoto. Katika nchi hii mipaka kati ya ndoto na ukweli haipo" (2004:3).

Watu wanapouawa na kupigwa risasi na polisi, viongozi wanakana ukweli huo. Wanasema kuwa nchi yao haiwezi kuwa na machafuko kwani ni nchi ya amani katika bahari ya machafuko. Hali hii ni ya kweli lakini mwandishi anaikejeli kama ndoto. Katika ndondoo hii mwandishi aliota ndoto ya kuandika riwaya siku moja. Riwaya ambayo itakuwa mahsusi. Na hiyo riwaya itajulikana kama <u>Musaleo</u>! Itajisoma yenyewe. Mzee vile vile aliota kuwa kiongozi wa kudumu. Alitafuta jina la kufaa: **OMNIZEE**. Alifanya mazoezi kadha ya jinsi ya kujieleza upya, ili aweze kukubalika na umma. Katika ndoto yake aliona kama anajitayarisha kuzaliwa kwa mara nyingine na jamii nayo ilipaswa kujiandalia kuzaliwa huko kupya, katika ndoto yake pia aliimba wimbo huu:

> Mimi ni mwezi utaoangaza giza la ukiwa wenu,
> Mimi ni mvua itakayoyeshea jangwa la umaskini wenu,
> Mimi ni rutaba itakapotea mimea ya matumaini yenu (2004:65).

Mara kadha alisimama na kuangalia hadhira ghibu, isiyokuwako. Aliweza hata kuwaona wafuasi wake sugu waliokuwa nusu wamelala wakiruka juu kama mikizi wakishangilia. Walisimama na kuitikia kwa vishindo vinavyoweza kuwategua vifupa vya shingo. Watapaaza sauti na kuiuliza hadhira: "Je, mmesikia maneno ya busara hayo?" mmoja atakatiza kwa kuuliza: "kweli-urongo?". . Amekanusha habari za dhuluma.

Tunateremka katika Kanaan ya ufanisi.. kweli-urongo? Je, tungekuwa wapi kama si kuwa naye?" wakati huo hadhira itadakia kwa kusema: **Omonimzee! Omonimzee! Omonimzee!** (2004:65).

Hii ni hali ya kweli ambayo inatokea miongoni mwa nchi zinzaotawaliwa na viongozi dhalimu. Lakini mwandishi ameyarejelea kama ndoto ili kusuta hali halisia iliyomo katika jamii. Bina-Adamu, anapokuwa bado yuko katika mojawapo ya nchi za kiafrika anapewa kijana mmoja ambaye anamtembeza. Wanapopita kutoka nyumba moja hadi nyingine wanakwenda nyumbani (nchini) mwa huyo kijana anamwambia kwamba kiongozi ana wafuasi wake ambao wamemtungia tenzi ambazo wanamkariria kama sala ya Bwana. Hapa ndipo mwandishi anakumbuka hata kwao mambo huwa hivyo. Kijana anasema kwamba huko shuleni mwao wao huimba sifa za kiongozi wao hata kabla ya kusoma Biblia na kuomba.

Hapa ndipo mwandishi anasema kwamba matukio hayo yanamkumbusha ndoto aliyokuwa nayo siku moja na anauliza: "Je, kuna mpaka wo wote kati ya ndoto na uhalisi kweli?" (2002: 93).

Jambo ambalo mwandishi anataka kuonyesha hapa ni kwamba, viongozi wa Afrika hupenda kusifiwa na kuabudiwa hata kumzidi Mola mwenyewe. Katika kuabudiwa, wanajiweka katika tabaka la kipekee na kujitenga na umma kubwa ulio maskini. Ndipo mwandishi anaona kuwa kwa kweli ndoto inaweza kuwa uhalisia.

## 4.3 UDUARA WA WAKATI

mwanda-wakati au Kronotopu ni dhana muhimu inayohusishwa na uhakiki wa Bakhtin. Mtaalam huyu anaitumia dhana hii kuzieleza sifa maalum au bainifu za wakati na mwanda au mahali katika tanzu mbali mbali. Kwa mfano, riwaya za Bina-Adamu an Musaleo! Zina mianda-wakati ya kijasira. Kazi zingine za Kiswahili ambazao zina sifa hizo ni pamoja na: Nagona (1990), Mzingile (1991), Babu Alipofufuka (2001) na Ziraili na Zirani (1991).

Mianda-wakati hii inaakisi wakati wa kidhahania usioelekea kuwa na athari za kisaikolojia au kibiolojia kwa wahusika.

Wahusika wanaopatikana katika riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo! Wanafanya matendo yao kwa kipindi kirefu sana na wanabakia katika hali zao (2001:156).

Carlos Fuentes akinukuliwa na Cooper (1008:32), anasema kwamba wakati katika uhalisiajabu si wa kistari bali ni wa kiduara. Fuentes anaamini kwamba wakati wa kihistoria ukiwa unawanyima vitu vingi ambao huelezea jamii yao ya Marekani kusini ambayo ni mchanganyiko wa jamii nyingi na tamaduni tofauti tofauti. Hata hivyo, uhalisiajabu unaweza kuielezea hali hii vyema.

Kwa mujibu wa Kumkum Sangari (1998), mwingiliano wa wakati wa kistari na ule wa kiduara huwezesha uhalisiajabu "kuzalisha na kumudu aina mbali mbali za migogoro, ufungamano/mfuatano kati ya wakati unaofululiza" (Cooper 1998:33).

Anaendelea kusema kwamba wakati katika uhalisajabu ni mahuluti na pia hujaribu kutokuwa au wakati wa kistari kama ilivyo katika historia. Sangari anaeleza:

> Wakati unaelea katika masafa yasio bainifu. Ni wakati wa
> katikati ambao kwa sababu sio wa kiduara au kistari,
> hiubua nafasi na wakati mwingine tofauti (Cooper 1998:33).

Kwa kifupi, Sangari anaeleza kwamba wakati wa uhalisiajabu ulioko huwa kati ya wakati wa kistari na wakati wa kiduara (Cooper 1995:33).

Masafa kwa mujibu wa Wilson, ni hali ambapo ulimwengu halisi huingiliana na hukaa katika hali sambamba na "yasiyowezekana, yasiyo ya kawaida na yasiyoweza kuthibitika."

Eva Luna katika Allende (1989) anasema:

> Huku mimi na wewe tukizungumza hapa nyuma yetu Christoper Columbus anagundua Marekani na wahindi fulani bado wako uchi nyikani kusiko mbali kutoka hapa, na watakuwepo miaka mia kutoka sasa (Allende 1989:300-301). Katika hali hii tunaona kwamba mambo mbalimbaliyanayohitilafiana yanatokea
> katika wakati mmoja.

Mawazo haya ya Allende (1989) yanatiwa mkazo na Leach katika Danow (1995) anayesema yafuatyo katika Rerthinking Antrhropoogy:

> . . . kwa kupendekeza kwamba wakati ni lazima upite kwa njia moja tu isiyobadilika, hatupaswi kufikiria wakati kama kitu kinachofululiza moja kwa moja. Mbona wakati usipungue mwendo au kusimama mara kwa mara, au hata kurudi nyuma? (Danaw 1995:74).

Leach anasisitiza kwamba si lazima wakati ufululize moja kwa moja. Wakati unaweza kupita kwa kasi au ukapita pole pole. Hii ni sifa ya wakati katika uhalisiajabu.

Mwandishi hutumia mbinu hii ili kutumia wakati bila kikwazo na kuwasilisha ujumbe wake bila pingamizi. Jambo hili la uduara-wakati limejitokeza katika kazi hizi zetu mbili (Bina-Adamu! na Musaleo!)

Kwa mfano, Bina-Adamu Msafiri anapokuwa akienda Ujerumani pamoja na mwanasayansi na mhubiri anatujulisha kwamba walifuatana kwa muda mrefu kwa siku, miezi au hata miaka (2002:53).Vile vile katika riwaya ya Musaleo!). Msafiri katika safari yake akiongozwa na Mamanchi, walikutana na mwanamume mmoja akawaambia:

> Nilimwonya akakataa. Ilikuwa lazima siku moja atafanya jambo la kumwudhi Mzee!" . . . nilisema yule ni kizalia cha ukolongwe wakataa?! Sasa wanayaona haya! Watu wanalala kwa miaka na miaka; usingizi wa aina gani huu?"

Hali kadhalika, katika (uk54), mwandishi anatufahamisha kuwa katika hadithi yake amekuwa akiisimulia kwa miaka mingi. Kwa mfano, utangulizi wake ulichukua miaka kama kumi kumaliza.

Msafiri Musaleo (uk.34) anatufahamisha: "Ambacho siwezi kujua kama ilikuwa siku nzima, mwongo mmoja au miaka kadha. Ninachokumbuka ni kuwa njia niliyotumia ilikuwa moja tu."

Katika Bina-Adamu! Msafiri Bina-Adamu anatembelea bara la Afrika ambapo anapewa chakula na kuonyeshwa pahali pazuri pa kumpzika. Anasema kuwa alipumzika humo barani kwa kipindi kirefu na hakujua ni siku ngapi, miezi au miaka mingapi.

Kwa kawaida, binadamu hawezi kulala kwa miaka na mikaka. aidha hawezi kuwa alikaa huko kwa miaka na miaka, aidha hawezi kuwa alikaa huko kwa miaka mingi.

Vile vile, utangulizi wa hadithi ya msimulizi hauwezi kuchukuaa miaka kumi kumaliza. Mwandishi ametumia mbinu hii ya uhalisajabu ili kuonyeha kwamba wakati katika uhalisajabu unaweza kuwa mrefu kupita kiasi. Wakati hupita tu katika mtindo huu na unaweza kurudi nyuma au kwenda mbele, kwenda kwa kasi au kujikokota. Kwa jumla, Msafiri anapokwenda kutoka nchi moja hadi nyingine mwandishi hatuambii anachukua muda gani katika bara moja au anachukua muda gani katika safari zake, kwa sababu safari yenyewe ni ya kimawazo. Msafiri anatembea nchi mojawapo ya Afrika ambayo inaonekana imebaki magofu. Mzee mmoja anayekuwa pale anamjulisha kwamba alikuwa amewaonya na wakapuuza:

> Niliwaambia wataharibu kila kitu. Niliwakanya wasikubali kushirikiana na mtu bila ya kujua ana nia gani wakasema sijui nikisemacho! Niliwakanya kuwa baada ya kuisha kwa biashara ya Ali Baba na Wezi Arubaini ya kuwandadi watu itakuja hatua nyingine; sasa akili zimelanguliwa. Wapumbavu wamebakia kula hamburger, kunywa Coke na kutazama mipira ya NBA katika televisheni (2002:85).

Wazo hilo la kutadharisha pia mwandishi amelirudia katika <u>Musaleo!.</u> Vijana walifunzwa visa mbalimbali kwa nia ya kuwaingiza katika ustaarabu mpya na mzuri. Walisimuliwa visa vingi lakini vilivyokuwa maarufi ni <u>Sinbad the Sailor.</u> <u>Ali Baba and the Forty thieves,</u> <u>King Solomon's Mines.</u> <u>The Treasure Island</u> na <u>Robinson Crusoe.</u> (Wamitila 2004:31). Walivikariri wakavikariri na kuvikariri. Jinsi walivyoendelea kuvikariri visa hivi ndivyo walivyoanza kuvisusia visa walivyotambiwa na wenyeji. wazee na mababu zao kama vile ngano za fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa maelezo haya, tunaona maafa yanayozikabili nchi za kiafrika kwa sababu ya kupapia mambo ya kigeni. Waafrika wanadharau amali zao na badala yake wanayoyafanya ni ya Kimarekani.

Katika riwaya ya Bina-Adamu! Kama vile tumeona katika Musaleo!, mwandishi amefanikiwa kutumia mtindo wa kuwepo na tajriba zinazoyeyuka na kuwa zingine bila onyo kwa kutmia urejeaji, mbinu rejeshi na mtiririko wa urazini.

Kwa mfano, Bina-Adamu Msafiri anapokuwa katika nchi ya Zakongwe anabadilika na kuwa mtoto. Anafurahia hali hii sana kwa sababu hana cha kuogopa au kufikiria kama watu wazima. Mwandishi anatuambia kuwa Msafiri anatamani kukaa huko. Kusudi la mwandishi kumpeleka huko ni kumwonyesha jinsi watu wanafaa kuishi kwa upendo, ushirikiano na kuwajali wenzao. Babu mmoja wa huko anawasimulia hadithi nyingi jioni kama ilivyo kawaida ya watoto na babu zao. Babu anamjulisha binadamu:

> Ikiwa hujajifunza kuwa kama mtoto huna popote utakapofika.
> Ulimwengu utaangamia siku utakapompuuza mtoto (2004:17).

Nia ya mwandishi ya kumbadilisha Msafiri kuwa mtoto na kukaa kitoto kwa muda alipokuwa Zakongwe ni kwa ajili ya kutaka aweze kuangalia jinsi maisha yalivyo katika sehemu zingine anazozizuru. Huko Zakongwe anapewa mfuko anaoambiwa una utu na kiini cha uhai wake. Pia umuhimu wa mtoto ukilinganishwa na utu uzima ni kama kiumbe ambacho akijajua kusoma wala kuandika, yeye ni bikira na hana uozo wo wote.

Riwaya ya Bin-Adamu! inaanza na Msafiri akiwa amekwenda kwenye kitovu cha kijijini mwao. Baada ya hapo, ingawa ni katika ndoto, anakwenda Zakongwe na kutembelea nchi mbalimbali za ulimwengu. Haya matembezi hayana mpango maalum. Kwa mfano, tungetarajia azizuru nchi za Afrika na akimaliza aende Uropa, kisha Marekani na hatimaye arudi nyumbani. Ingawa ni katika ndoto, hadithi ya kazi hizi mbili vitushi na matukio hayafuatani moja kwa moja kama tujuavyo katika riwaya zingine. Jambo hili linawezekana katika uhalisiajabu kwa sababu ya upekee wake wa kuweza kuvunja mipaka ya mahali na pia kwa sababu wakai si wa kistari.

## 4.4 KUVUNJWA KWA MIPAKA YA MAHALI

Katika uhalisiajabu matukio hayajikiti katika mukhtadha finyu wa jamii moja, nchi au hata bara moja. Hii ndiyo tofauti kubwa sana na mitindo mingine ya uandishi. Katika aina nyingine za uandishi mhusika hawezi kutoka katika nchi moja hadi nyingine na kurudi kama ilivyo katika uhalisiajabu. Hii ndio mojawapo ya upekee wa uhalisiajabu. Mwandishi wa uhalisiajabu hufanya hivi ili kuondoa ufinyu wa ujumbe wake. Hataki ujumbe wake uwe na watu au jamii moja tu, bali uwe ambao unaweza kuzinufaisha jamii zingine, nchi zingine au hata mabara mengine pale inapofaa. Uwezekano wa wahusika wa kihalisiajabu kuvuka mipaka ni kwa sababu ya vile wanavyoumbwa. Aidha tuna ule uajabu ambao, tunatarajia katika kazi za kihalisiajabu. Wahusika wafu kama tuonavyo katika Bina-Adamu! na Musaleo!.

Faida ya kutumia kipengele hiki cha uhalishajabu ni kuwa mwandishi anaweza kuwasilisha ujumbe bia usio na vikwazo vya kitamaduni vya sehemu moja finyu.

Wamiltila anamsawiri Bina-Adamu akitoka kwao kijijini na kupitia misituni na mto ulio na mkondo unaorudi nyuma na anajikuta Zakongwe. Baada ya muda usiojulikana kwa sababu hivyo ndivyo uhalisiajabu ulivyo (wakati haupimiki), anajipata Ujerumani akilitazama jengo lililoangushwa wakati wa vita. Baada ya muda mhusika anatokeza nchini Japani na tunamkuta akishuhudia madhara ya mabomu yaliyoangushwa huko na P.P. pasipo kukawia anashika njia na mara anafika Urusi na tunamwona akiwa na wakulima mashambani mwao.

Muda si muda, Bina-Adamu anarudi barani Afrika tena. Huko Afrika anatembea kutoka nchi moja hadi nyingine kikawaida kabisa. Kutoka huko anakwenda Marekani na hatimaye tunamwona akiamka kutoka ndotoni.

Ngwena mtaalamu wa Historia, alihamia nchi nyingine na kuhakikishiwa usalama na ubalozi wao nchini humo (2004:19). Vile vile ukoloni ulipoanza pale Mji wa Berlin, Ujerumani mwaka wa 1884, ulisambaa kama moto kote ulimwenguni.

Hali kadhalika mwandishi anasema kuwa kizazi cha Yunga Mwamba kilihamia huko Ujerumani kutoka upande wa kusini na kuja kutua penye jiwe kuu la mboni karibu na mlima wenye jina sawa na jiwe lenyewe. Baadaye watu hawa walisambaa sehemu mbali mbali (2004:20).

Mfano mwingine ni ule wa **MEFU**. Wimbo wa mefu unaimbwa kila mahali; kushoto, kulia, nyuma na mbele. Vile vile masuala ya haki za kibinadamu, demokrasia na vyama vingi vya kisiasa ni masuala ya kimataifa.

Hatimaye Mzee alijitenga na kuhamia milimani. Huko ndiko alikoishi akicheza magoma yake, akiwa na uwezo wa kukiangalia kijiji, nchi, bara na kijiji tena. (2004:99).

Kutokana na mifano hii, tunaona kuwa kuna uwezekano wa mhusika kukaa mahali kihalisia na kuwaza kuhusu mambo haya yote. Kiwiliwili chake hakisongi bali fikra zake zinatambaa ko kote mwandishi atakako na kutambua vizingiti vingi vya hali mbalimbali za maisha ya binadamu.

Faida ya kutumia mbinu hii ni kwamba viwango mbalimbali vya maisha vinaweza kulinganishwa na kutofautishwa kwa wakati mmoja na kwa haraka. Badala ya kuiandika ripoti kuhusu nchi anazozuru, mhusika mkuu anazitembelea kimawzo na kumkabidhi msomaji anayoshuhudia.

## 4.5 VISASILI

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:91) kisasili ni hadithi ambayo haihusishwi na mwandishi maalum bali hupatikana katika imani zilizopo katika jamii fulani. Aghalabu visasili huhusisha matukio ya kiajabu au yasiyotarajiwa katika maisha ya kawaida au hata ya miungu. Huweza kuhusisha pia wahusika wa kishujaa wa kihistoria au wa kuaminika ambao wanatenda matendo yanayokiuka uhalisia wa kawaida.

Visasili huakisi muundo wa kitamaduni wa jamii inayohusika. Kwa kuwa kimsingi visasili huhusishwa na hatua ambapo upokezi wa kimdomo unachukua nafasi kubwa, inawezekana

kusema visasili huonyesha juhudi za jamii fulani kujaribu kuhifadhi maarifa fulani kujihusu. Hapana lazima ya kisasili kuwa na misingi ya kihistoria inayotambuliwa au inayodhihirika waziwazi.

Katika riwaya ya Musaleo!, tunapata visasili vingi. Kisasili cha kwanza kinahusu Ukolongwe na Musaleo! Kisa hiki ndicho mwandishi amekitumia kama msingi wa hadithi yake katika riwaya hii. Kisa cha Ukolongwe kina maana ya ukoloni mkongwe. Mwandishi anatusimulia vile nchi za Afrika zilinyakuliwa na Wazungu. Ukoloni mkongwe uliendelezwa na Wazungu wenyewe. Walitumia mbinu anuwai ili kuweza kuwatawala wenyeji zikiwemo elimu, dini na hata nguvu. Wenyeji waliwakataa wakoloni na ujanja wao. Walipewa uhuru wa bendera na wenyeji wakashika hatamu za uongozi. Viongozi wenyeji walianza kujinyakulia mali na basi wakaanza kuwa majitu, mabepari, mamwinyi na kuwa mabeberu weusi. Kwa hiyo wakawa wabaya zaidi kuliko wakoloni wenyewe na basi wakaanza kuendeleza ukoloni mamboleo.

Hali hii mbaya na dhuluma iliendelea hivyo hadi imefikia kiwango cha kuhitaji ukombozi wa kujikomboa hasa kutoka minyororo ya viongozi hawa dhalimu wa kiafrika. Hii nafasi inahitaji shujaa / jagina. Mtu Jasiri atakayewakomboa waafrika kutoka janga la maozo yanayotendwa na viongozi wenzao. Kunahitajika Musa wa leo (Musaleo) atakayewakomboa wenyeji kutokana na mateso ya viongozi wa kiafrika.

Visasili vingine katika riwaya ya Musaleo! Ni kama vile kuzaliwa kwa mzee mwenyewe.. Alizaliwa kama shujaa. Kwa mfano, (uk.3) alipozaliwa alitoka tumboni akiwa amekunjia mbegu za kuwangia kiganjani. Siku chache baadaye waliamka watu na kukuta nyingine nje, akapewa akafumbia kiganjani. Meno yake yaliotea tumboni kwa hivyo alikuwa kigego. Alikuwa na kichwa kinene ajabu. Kisa cha kijiji kipya kuongoza, kingine ni kile cha Yanguis ambaye anatumbulika kwa majina mbalimbali kutegemea maeneo kwa mfano, Waafrika wanamwita **Mjomba**, wahindi **Amrika,** watu kutoka Iran au Iraq walimwita **Shai-Tani** na kijiji kipya (global village) kitaongozwa na Mjomba (Marekani) ambaye ana nguvu ajabu. Katika riwaya ya

Bina-Adamu!, tunapata visasili viwili. Kisasili cha kwanza kinahusu jabali moja kubwa ambalo ndilo kiini cha kijiji cha msimulizi. Iliaminiwa kwamba mtu akienda kwenye kitovu cha kijiji kulikuwako na vituko/utaishia kupatwa na madhara makubwa.

Kwa mfano, mwanamume atayekwenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia/menke na kuwa mwanamke kwa kuwa lazima alizunguke jabali lililoko hapo (2002:9).

Suala la kisasili katika jamii huwa ni imani tu. Kisasili kinaweza kutumiwa na kikundi au jamii moja ya watu kuwaogofya na kuwabadilisha ikiwa jambo ambalo hawataki hao watu walijue.

Katika riwaya ya Bina-Adamu!, mwandishi ametumia kisasili cha jabali la Nzambani *(ivia ya Nzambani)* katika jamii ya Wakamba:

> Nzambani Rock ni jabali kubwa sana ambalo linapatikana katika wilaya ya Mwingi. Jabali lenyewe ni kiini cha imani za kila aina. Kwa mfano, inasemawa kuwa ukilizunguka mara saba jinsia yako itabadilika na kuwa nyingine. Kwa mfano mwanamume kuwa mwanamke. Hamna ambaye amethubutu kufanya jambo hili, hasa kwa kuwa jabali lenyewe ni kubwa mno na liko sehemu hatari sana. Pili, wakazi wa eneo hilo hudai kuwa hutokea siku ambapo huamka wakaona maandishi ya kila aina kwenye jabali lenyewe. Ni kiini cha visa na vitushi vya kuogofya na hata kuchangamsha (Bertoncini 2004: 10).

Kisa hiki ndicho Wamitila ametumia kama msingi wa hadithi yake katika riwaya ya Bina-Adamu! Katika kiini cha kijiji ndipo kuna lile jabali. Hakuna mtu anayedhubutu kukaribia pale kwa sababu ya woga. Ikiwa hivyo, basi kunahitajika jagina (shujaa) ambaye atafika pale kwenye kiini cha kijiji. Mwandishi anagundua kwamba hadithi za kuogofya ni mbinu tu, ya kuwafanya Waafrika wakae pembezoni huku wengine wanafurahia manufaa ya kukaa kwenye kiini cha kijiji.

Kisasili kingine kinachotajwa katika riwaya ya Bina-Adamu! ni cha *WOTAN*. Huyu ni Mungu wa vita na mfalme wa mashujaa wafu wa Kijerumani.

Muhimu zaidi ni mganga. Kiumbe huyu ni kama jini linalozama pahali pamoja na kuibukia pahali pengine. (2002:35). Katika vita, huyu wotan aliogopwa sana kwa sababu iliaminika angewasaidia Wajerumani kushinda.

## 4.6 MITINDO YA RIWAYA HIZI

Kipengele kingine kinachotumiwa kuonyesha uduara wa riwaya hizi mbili ni jinsi usimulizi wao ulivyoumbwa. Katika uandishi mwingi wa kazi za fasihi, matukio hufuatana moja kwa moja hivi kwamba msomaji anaweza kufuata vitushi bila utata wowote. Hata pale ambapo mbinu rejeshi hutumiwa, mbinu hiyo hutumiwa kwa lengo maalum linalohusiana na muwala wa riwaya husika. Kinyume na haya, katika uhalisiajabu matukio hayafuatani moja kwa moja, kwa kuwa hakuna mantiki iliyozeoleka. Jambo hili hufanyika kwa kutumia mbinu ya urejeshi na mtiririko wa urazini na kujenga wahusika wenye nafsi mbili. Tajiriba zinayeyuka na kuwa zingine bila onyo wala utaratibu.

Mugogo Wehu, mhudumu wa Ombaomba, anajiwa na hamu ya kufumbua kitendawili asichoteguliwa. Hadithi yake inasimuliwa sambamba na nyingine inayosimuliwa na Mzee, kiongozi wa nchi ambaye anapambana na wakati asiouelewa. Vile vile kisa cha Ukolongwe, kinatusimulia maisha ya jana, enzi ya wakoloni na vile waliwatesa Waafrika, kwa utumwa na kutumia malighafi yao. Mbinu ya urejeshi imetumiwa kuwasilisha kisa hiki.

Katika riwaya ya Bina-Adamu! Msafiri Bina-Adamu anapokuwa akienda nchi ya Zakongwe ambayo ni kielelezo cha 'jana' ambapo kuna utu, upendo na waliohifadhi utamaduni wao na mengineyo, mkondo wa maji unawarudisha nyuma. Vile vile Musaleo! (uk 45) mwandishi anasema kuwa anakumbuka kuwa zamani walifundishwa kanisani kuwa ahera ni juu na jehanamu ni chini.

Mwandishi ametumia mbinu hii ili kuonyesha kwamba zamani kulikuwa na maadili na utu.

## 4.7 HITIMISHO

Katika sura ya nne tumehakiki riwaya za Bina-Adamu! na Musaleo!. Katika uhakiki huu tumechunguza jinsi Wamitila alivyotumia vipengele vya uhalisiajabu katika uwasilishi wa ujumbe wake. Mihimili aliyoitumia ni kama vile matukio ya kiajabuajabu, kigezo cha uhalisia na ndoto, uduara wa wakati, uvunjaji wa mipaka ya mahali na nafasi ya visasili katika uhalisiajabu.

Katika sura inayofuata tutatoa hitimisho ya tasinifu hii. Vile vile tutaelezea matatizo tuliyoyakabili katika utafiti huu, mchango wa tasnifu hii katika fasihi ya Kiswahili na hatimaye kutoa mapendekezo yetu.

## SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza uhalisiajabu ulivyotumika katika riwaya za Bina-Adamu! (2002) na Musaleo! (2004). Dhamira nyingine ya tasnifu hii ilikuwa kubainisha ni vipi uhalisiajabu unavyoashiria na kuzungumzia uhalisia wa matukio ya nyakati zetu. Mwishowe tulilenga kuchunguza vile mtindo wa uhalisiajabu unavyotuwezesha kuzielewa riwaya hizi mbili zaidi.

Jambo lililotuhamazisha kufanya utafiti wa aina hii kugundua kwamba baada ya mapitio ya awali, ilitujia kuwa kuna aina za kazi za fasihi ya Kiswahili ambazo zinaonyesha tofauti fulani katika uandishi. Tofauti hii ni kwamba zimeandikwa kwa mtindo wa kiajabu ambao zikisomwa kikawaida hazieleweki. Mapito zaidi yalionyesha kuwa huu ni mtindo wa uhalisiajabu. Hapo ndipo tuliona kwamba kazi hizi zinahitaji usomaji mpya.

Utafiti wetu umeonyesha wazi kwamba uhalisiajabu umo katika riwaya ya Bina-Adamu! na Musaleo!. Uchunguzi wetu pia umethibitisha kwamba uhalisiajabu unatumiwa kutalii masuala nyeti yanausibu ujirani wetu. Kinadharia, tumetumia nadharia ya uhalisiajabu. Kwa jumla, nadharia hii huhusisha mkondo wa uandishi ambapo matendo na matukio ya kifantasia na kiajabu husawiriwa kama ya kawaida. Wanaoitumia nadharia hii hudai kwamba ingawa mambo huwasilishwa kwa njia ya kiajabu, hutokea katika maisha ya kila siku. Mihimili ya nadharia hii ni mingi. Tumetumia mihimili inayojitokeza katika riwaya tulizosoma. Pia tulitaja na kufafanua mihimili mingine mikuu kwa sababu nayo vile vile inaingiliana na kuimarisha ile tuliyoitumia. Kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu tumeweza kuzichambua riwaya zetu mbili na kudhihirisha kwamba ni za kihalisiajabu.

Kutokana na usomaji wetu, wa riwaya za Bina-Adamu!na Musaleo!, tumegudua kwamba zinafanana na ni kazi mfuatano katika kuangazia baadhi ya maswala katika jamii. Wamitila ameangazia masuala ya uongozi mbaya katika nchi za Kiafrika, utandaridhi na athari zake kwa mataifa ya Afrika. Vile vile amezungumzia suala la ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Mwandishi anawalaani viongozi walioshika hatamu za uongozi baada nchi zao kujipatia uhuru wa bendera kutoka kwa Mzungu. Walianza kujilimbikizia mali na wakazua mbinu mbalimbali za kuyaendeleza maongozi yao ya kiimla. Basi wakawa wabaya kushinda hata Wazungu wenyewe. Hawa viongozi wanajijali wao binafsi.

Wao hutumia nguvu zao za kisiasa kushirikiana na wazungu na kushiriki kwenye miradi ambayo huwa sio kwa manufaa ya nchi bali ni kwao tu. Wamitila anaonyesha uozo wanaoshiriki wengi wa viongozi hawa wanapotekeleza dhuluma, ufisadi na mabaya mengine. Hakuna madawa, njaa imekithiri, ukame umezidi, mifumo ya elimu ni duni na kuzorota kwa uchumi.

Hali kadhalika, mwandishi anachunguza dhana ya utandaridhi na kusisitiza kuwa kijiji cha ulimwengu ni zao la kimagharibi la kuwanufaisha wakazi wa nchi za kimagharibi.Hata hivyo ni muhimu tukumbuke hapa kuwa utandaridhi hutoa nafasi nzuri za kuendelea. Vile vile ni muhimu kuyaelewa madhara ya utandawazi na ukweli kuwa manufaa yake hayajasawasishwa na gharama yake hali kadhalika haijagawika kisawasawa miongoni mwa mataifa, kutoka upaqnde mmoja hadi mwingine. Jambo ninaloweka nguvu hapa ni kuwa, kwa jumla, kila uzuri wa utandawazi kuna ubaya wake. Baadhi ya manufaa yake ni kama vile ubunifu, na kuleta dhana ya elimumwendo. Madhara yake ni pamoja na kuvuruga, kuingilia na kutenganisha na kuweka mataifa machanga pembezoni.

Kwa kuchangai madai haya, shirika la (UNDP 1999:25) Linatoa ripoti kuhusu utandawazi kwa kumulika manufaa na madhara yake kwa njia ifuatayo:

| Manufaa | Madhara |
|---|---|
| Utandaridhi hutangamanisha maisha ya watu | Tamaduni zingine hufifishwa na zingine kuharibiwa na hata nafasi ya kueneza maozo huwa rahisi. |
| Vyombo vya kisasa vya mawasiliano vimerahisisha kutangamana kwa mataifa na watu kutoka maeneo mbalimbalikote ulimwenguni. | Ulimwengu sasa umegawanyika kimatabaka, maskini na matajiri, wanao na hawanazo, wanajua na wasiojua n.k. |
| Utandaridhi umeinua viwango vya biashara vya kimataifa, ubadilishanaji na uwekaji wa miradi na malighafi za kigeni. | Utandaridhi umefungua mianya ya kufanya biashara haramu kama vile madawa ya kulevya, ukahaba ponografia, uporaji wa watu na uharibifu wa mazingira, utupaji wa taka za kemikali hatari kutoka |

| | |
|---|---|
| | viwandani. |
| Utandaridhi umefanya wafanyakazi kusafirishwa kutoka pembe moja hadi nyingine. Jambo hili limeleta ubadilishanaji wa wataalam. | Umeendeleza uhamiaji wa wataalam kutoka mataifa machanga kwa hivyo kupunguza uwezo wa kuendelea au wa kuleta maendeleo. |
| Utandaridhi umebuni sheria mpya zinazojumuisha soko huria ya kimataifa. | Sheria hizo mpya zimeyatenga mataifa maskini kutoka bara la Afrika, watu wake hasa kwa upande wa kibiashara. |
| Kijiji cha ulimwengu kimeundwa kutokana na utandawazi. | Kumezuka matabaka: ya umaskini na utajiri. |

Matokeo ya utandawazi sio tu ya kiuchumi, pia yanajumuisha usambaaji wa maadili au mawazo ya kisiasa na matumizi ya mawazo hayo miongoni mwa mataifa; usambaaji wa tamaduni, imani za kidini, mazoea na kuyeyushwa kwa mila na itikadi zingine.

Utandaridhi umelete changamoto kubwa kwa mataifa ya Afrika kwa sababu mambo mengi kama vile uongozi, maarifa, elimu, mifumo mtandao, teknolojia na vifaa yote yanahitaji kupewa sura mpya. Masuala haya yamekuwa dhaifu na kwa hivyo yanastahili kubadilishwa.

Mtazamo mpya unahitajika kutoka kwa viongozi ili tuweze kulimudu suala la utandaridhi ipasavyo. Kunahitajika maono, ujuzi sahihi, maarifa na hekima ya viongozi wa kiafrika Pia

moyo wa kujitolea na misaada ya kiufundi kutoka wahusika wakuu wa utandaridhi kama vile shirika la UN, hasa jinsi ya kuboresha maongozi ya umma yanayohusiana na utandawazi. Ili kufanikisha utandaridhi, mataifa ya Afrika yanatakikana yakubali mabadiliko, kuwe na utendaji na uwajibikaji kama njia mojawapo ya kuwa na maadili ya kidemokrasia na kutatua matatizo ya raia au wananchi.

Mataifa ya Afrika yanastahli kutumia utandaridhi kuamua mwelekeo wa watu wake badala ya kuuwacha utumie nchi zao kuamulia mielekeo ya ulimwengu. Kwa kuwa mataifa ya ulimwengu wa kwanza yamejimudu kwa masuala yanayohusiana na uandaridhi, yamekuwa na uwezo mkubwa. Kwa mfano Wazungu hata huzua masharti ambayo huwafanya Waafrika kuondolewa kushiriki ipasavyo katika shughuli za kiuchumi na kisiasa kwa sababu wao waafrika huwa pembeni mwa Kijiji. Kwa kufanya hivi, wazungu huweza kudhibiti mbinu na nyanja zote za kiuchumi. Wazungu ndio huyauzia mataifa ya kiafrika magari, madawa, na bidhaa zingine nyingi. La ajabu zaidi wazungu ndio pia huuziuzia nchi hizi mizinga ya kupigana katika vita walivyosaidia kuchochea ili kupata soko la silaha hizo.

Aidha wao huyauzia mataifa haya samaki wa makombo ingawa nchi hizi za kiafrika zina bahari na maziwa mengi! Nasaha ya mwandishi kwamba, yafaa Waafrika wajiamini wenyewe na kushiriki kikamilfu katika maendeleo ya mataifa yao kiuchumi,kisiasa na kijamii. Vile vile ana matumaini kwamba tatizo la utandaridhi linaweza kutatuliwa ikiwa waafrika wataacha kujidharau, wajiamini na kujua kwamba wana uwezo wa kisiasa na kiuchumi kama bara lingine lolote lile. Aidha, anasema umoja wa nchi za kiafrika ni muhimu ikiwa zinataka kupambana dhidi ya uporaji wa nchi za kimagharibi.

Wamitila analaani soko huru la kibiashara kwa sababu matokeo yake ni kuwagandamiza waafrika kibiashara. Wanaokuwa na uhuru si waafrika bali ni wazungu. Ndio wanavua samaki na kuwauzia Waafrika kuuza magari yao mabovu Afrika na mengine.

Kwa mujibu wa mwandishi, nchi nyingi za kiafrika haziwezi kujiamulia kesho na hatima yao kwa sababu uamuzi huu umeingiliwa na mtaji anayeweza kuingia na kutoka jinsi atakavyo. Kuhusu suala la soko huru la kibiashara, mwandishi anaonya kwamba uhuru huo umewaruhusu wafanyi biashara haramu na kuingiza bidhaa mbaya na chapwa nchini. Kwa njia hii, wageni ndio tu wanaofaidika bali si waafrika.

## 5.2 MATATIZO

Safari nzuri aghalabu haikosi kasoro. Katika kazi hii, nilikabiliwa na matatizo kadhaa. Baadhi yao yametatuliwa na mengi hayajasuluhishwa. Kwanza, ilikuwa jambo jipya kuelezea wasomaji kuhusu uwili wa uhalisiajabu kama nadharia ya uhakiki ya fasihi ya Kiswahili na vile vile kama mbinu ya uandishi wa fasihi. Kutokana na utafiti huu imedhihirika kwamba baadhi ya nadharia za uhakiki zinaweza kutumika pia kama miongozo ya mitindo ya uandishi.

Tatizo la pili lilikuwa la istilahi. Kuna istilahi nyingi zinazohusishwa na nadharia hii. Baadhi yake ni za mpito na hazijasanifishwa. Jambo hili linaweza kuwa tatizo kwa wasomaji ikiwa istilahi zinazotumiwa zitakufa au hazitatumiwa na wahakiki wengine. Pamoja na haya, dhana yenyewe ya uhalisiajabu ilikuwa ngumu kwa sababu nadharia hii imeelezwa kwa lugha ya kiingereza, kifaransa na kihispania na tajriba inayoelezwa haifanani moja kwa moja na mazingira ya Kiswahili/Uswahilini. Hata hivyo, kazi hii ni mchango mkubwa katika taaluma ya uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

Kama tulivyotaja hapo awali, mchango mkuu wa kazi hii ni kwamba imeonyesha ya kwamba uhalisiajabu umetumika katika riwaya mbili za Kiswahili Bina_Adamu! na Musaleo! Uhakiki huu umetumiwa kumulika masuala ya wakati wetu yanayohusu hali halisi ya maisha yetu kama vile uongozi, ufisadi, ukoloni mamboleo na athari ya utandaridhi.

Utafiti huu pia umethibitisha kwamba njia zilizowekwa na za kimapokeo za kusoma na kuhakiki kazi za fasihi zina ufinyu fulani.

Tofauti na njia hizi za kijadi, tumeonyesha kwamba katika uhakiki wa uhalisiajabu binadamu anaweza kufikiria nje ya mipaka ya kihistoria na uhalisia wa kawaida. Jambo hili hutokea wakati mwandishi anapomuumba mhusika anayeweza kushiriki katika maisha kimawazo badala ya kushirikisha kiwiliwili chake kama tuonavyo wahusika Msafiri BinaAdamu na Msafiri Musaleo wakifanya. Uhalisiajabu unampa msomi ufunguo wa kuzihakiki kazi za fasihi kwa mitazamo tofauti ambayo si lazima ikinzane.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Kazi hii imehakiki riwaya mbili tu za fasihi ya Kiswahili, kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu. Ningependekezo kwamba watafiti wengine washughulikie kazi zingine za fasihi ya Kiswahili na kuzihakiki kwa kutumia nadharia hii ya uhalisiajabu. Utafiti huu unaweza kulenga riwaya zingine au tamthilia za Kiswahili. Aidha utafiti wa baadaye unaweza kutumia uhaliajabu kuzungumzia masuala ya kijinsia na kisayansi.

## MAREJELEO


Alexander, M. (1990) Flights from Realism. Edward Arnold, London.

Allende, I. (1985) The House of the Spirits. Anchor Brendon Ltd. London

Bertoncini, E (2004) Global Village or Global Pillage? K.W. Wamitila's novel Bind-Adamu! (Haijachapishwa)

Cooper, B. (1998) Magical Realism in West African Fiction, Routledge, New York.

Danow, K.D. (1995) The Spirit-of the Carnival; Magical Realism and the Grotesque, University of Kentucky Press. Kentucky.

Drouart (1993) Journal of the South Pacific Association for Commonwealth Literature and Language Studies. No.36, London.

Encarta Encyclopedia (2002) Microsoft Company Limited, New York.

Fische, E (1959) The Necessity of Art: A Marxist Approach, Penguin Books, Middlex.

Fokkema, D & Ibsch, I. (1995) Theories of Literature in the 20$^{th}$ Century: Structuralism. Marxism. Aesthetics. Semiotics, C, Hurst & Company, London.

Foster E. M. (1969) Aspects of the Novel. London: Edward & Arnold Publisher s Ltd.

Gorky, M. (1949) Mother. Moscow: Progress Publishers.

Gromov, M. (2002) Post Modernistic Elements in Recent Swahili Novels. Nairobi: (Haijachapishwa)

Harrow, K.W. (1994) Thresholds of Change in African Literature. Heinemann. London.

Hough. (1962) An essay on Criticism. Witt shire. Redwood press Ltd, Wittshire.

Hussein, E.N. (1971) Mashetani.. Oxford University Press. Nairobi.

Kagendo, J.M. (2004) Tasnifu M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haichapishwa)

Kezilahabi, E. (1990) Nagona. Dar- es- Salaam University Press. Dar-es-Salaam

__________(1991) Mzingile. Dar- es- Salaam University Press. Dar –es- Salaam.

Khaemba, S.S. (1999) Ulinganishi wa Maudhui Ya Mapinduzi katika Dunia Mti Mkavu na Kiza Katika Nuru Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kruisheer, (1997) "Nani Kaonja - A Social Political Interpretation of the play: Aliyeonja Pepo, Kiswahili." Juzuu Nambari 59.

Liman, A.R (1997) Post - Colonial Discourse, The Case of Ben Okri's. The Famished Road.

Marquez, G.C. (1972) Leaf Storm. Pan Books Ltd, London.

____________(1975) The Autumn of the Patriarch. Harper & Row Publishers, NY

____________ (1980) One Hundred Years of Solitude. Pan Books Ltd, London

____________ (1983) Chronicle of Death Foretold. Picador Ltd, London:

Mbatiah, M. (2001) Kamusi Ya Fasihi. Standard Text Books Graphics and Publishing, Nairobi.

Mbatiah, M. (1997) Commitment ni the Swahili Novel: An Appraisal of the Works of Said Ahmed Mohamed. (uk. 15). Kiswahili. Juzuu Na. 58:15

Mbatiah, M. (1997) Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi. Mulika Nambari 24. TUKI, Dar- es- Salaam.

Moh. F.C. (2002) Ben Oki. An Introduction to his Early Fiction. Fourth Dimensions, Enugu.

Mohamed S.A. (1980) Dunia Mti Mkavu. Longman. Nairobi.

__________ (1988a) Pungwa. Longman. Nairobi

__________ (2001a) Babu-Alipofufuka. Jorno Kenyatta Foundation. Nairobi.

Njogu, K (1997) Uhakiki wa Riwaya za Visiwaqii. University Press. Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) Ufundishaii'na Fasihi, Nadharia na Mbinu, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Okri, B. (1991) The Famished Road., Vintage, London.

Rio, F. (2002) Magical Realism: Definitions. (Mtandao wa Internet).

Rushdie, S. (1981) The Midnight's Children. Butler & Tanner Ltd, London.

Topan, F (1970) Aliyeonja Pepo. Tanzania Publishing House Limited, Dar-es-Salaam.

TUKI (2000) English - Swahili Dictiona!y. Dar- es- Salaam University Press, Dar-es-Salaam.

Wafula, R.M (1999) Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo Yake, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K.W (1997) Contemptus Mundi and CarN Diem Motifs in Kezilahabi's Works, Kiswahili Juzuu Na. 60, uk.15-24.

____________ (1998) Nagona & Mzingile: Kezilahabi's Metarphysics. Kiswahili juzuu Na. 60. Dar- es- Salaam.

____________ (1999) Nguvu Ya Sala. Longhorn Publishers, Nairobi.

____________(2002) Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake. Phoenix Publishers. Nairobi.

____________(2002) Zimwi La Leo. Sasa Sema Publications, Nairobi

____________ (2002) Bina-Adamu! Phoenix Publishers, Nairobi.

____________(2003) Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia. Focus Books, Nairobi.

____________(2004) Musaleo!.Vide-Muwa Publishers, Nairobi.

Williams, R. L (1995) The post Modern Novel in Latin America. Macmillan Press Ltd. London.

Wood, M. (1990) Hundred Years of Solitude. University of Cambridge Press, Cambridge.

Zamora P. L na Faris B. W. (1995) Margical Realism theory. History Community Duke University Press, London.